

# Wadhihirishaji Pacha



Taasisi ya Ruhi





Kitabu cha 4

# Wadhihirishaji Pacha

Taasisi ya Ruhi

Vitabu vilivyopo katika Mfuatano:

Hapa chini kuna majina ya vitabu vya sasa vilivyopo katika mfuatano uliosanifiwa na Taasisi ya Ruhi. Vitabu hivi vimekusudiwa kutumika kama mlolongo mkuu wa kozi katika jitihada ya hatua kwa hatua ya kuongeza uwezo wa vijana na watu wazima kuhudumia jumuiya zao. Taasisi ya Ruhi pia inaendelea kukuza seti ya kozi ambazo zinachepuka kutoka kitabu cha tatu kilichopo katika mfuatano kwa ajili ya kuwafunza walimu wa madarasa ya Kibahá'í ya watoto, hali kadhalika seti nyingine kutoka Kitabu cha 5 kwa ajili ya kuwainua wahuishaji wa vikundi vya vijana chipukizi. Hivi pia vimeainishwa katika orodha hapo chini. Sharti izingatiwe kwamba orodha hii inaweza kubadilika kadiri tajiriba ugani inavyoongezeka, na mada zaida zitaongezwa kadiri idadi ya vipengele vya mtaala vinavyoendelea kukuzwa vitakapofikia hatua ambapo vitaweza kupatikana kwa wingi.

| | |
|---|---|
| Kitabu cha 1 | *Mawazo Juu ya Maisha ya Roho* |
| Kitabu cha 2 | *Uinikaji kwa Kuhudumu* |
| Kitabu cha 3 | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 1* |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 2* (kozi ya mchepuo) |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 3* (kozi ya mchepuo) |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 4* (kozi ya mchepuo) |
| Kitabu cha 4 | *Wadhihirishaji Pacha* |
| Kitabu cha 5 | *Uachiliaji wa Uwezo wa Vijana Chipukizi* |
| | *Msukumo wa Awali: Mchepuo wa kwanza wa kozi ya Kitabu cha 5* |
| | *Duara Lipanukalo: Mchepuo wa pili wa kozi ya Kitabu cha 5* |
| Kitabu cha 6 | *Kufundisha Hoja* |
| Kitabu cha 7 | *Kutembea Pamoja kwenye Njia ya Huduma* |
| Kitabu cha 8 | *Agano la Bahá'u'lláh* |
| Kitabu cha 9 | *Kupata Mtazamo wa Kihistoria* |
| Kitabu cha 10 | *Kujenga Jumuiya Hai na Zenye Kupuma* |
| Kitabu cha 11 | *Nyenzo za Kimwili* |
| Kitabu cha 12 | *Familia na Jumuiya* |
| Kitabu cha 13 | *Kujihusisha katika Shughuli za Kijamii* |
| Kitabu cha 14 | *Kushiriki katika Mijadala wa Umma* |

Hakimiliki © 2001, 2023 ya Ruhi Msingi, Colombia
Haki zote zimehifadhiwa. Toleo la 2.1.2.PE zilizochapishwa Agosti 2025
ISBN 978-628-95545-5-7

Kilichapishwa awali kwa Kihispania kama *Las Manifestaciones Gemelas*
Hakimiliki © 1987, 1997, 2021 ya Ruhi Msingi, Colombia
ISBN 978-958-53332-2-2

Taasisi ya Ruhi
Cali, Colombia
Barua pepe: instituto@ruhi.org
Tovuti: www.ruhi.org

# Yaliyomo


Mawazo Machache kwa Mkufunzi ....................... v

Ukuu wa Siku Hii ................................................ 1

Maisha ya Báb .................................................... 15

Maisha ya Bahá’u’lláh......................................... 69

# Mawazo Machache kwa Mkufunzi

Hadi washiriki wanapoifikia kozi hii ya nne inayotolewa na Taasisi ya Ruhi, bila shaka watakuwa wamepiga hatua katika njia ya huduma inayofunguliwa na mlolongo wake mkuu. Bila kujali usuli wao pale wanapoingia katika Kitabu cha 1, sasa watakuwa wameshajikita katika muono wa mabadiliko ya mtu binafsi na ya jumuiya ulioelezwa katika Maandiko ya Bahá'u'lláh. Kufikia hapa, watakuwa wameanza kujenga tabia ya kusoma maneno Yake kila siku na watakuwa wanachota chakula cha kiroho, pote pawili katika mikusanyiko ya kiibada na katika nyakati za kudhukuru kwa ukimya, kutoka kwenye sala na nasaha ambazo Yeye amezifunua. Watakuwa wanajifunza kujihusisha katika mazungumzo na marafiki na jamaa juu ya kanuni za kiroho alizozielezea kwa uwazi na watakuwa wanafanya matembezi kwenye nyumba katika kijiji au ujirani wao ili kujadili juu ya maagizo Aliyoyaleta ya kuujenga upya ulimwengu. Baadhi watakuwa wanaendesha madarasa kwa ajili ya elimu ya kiroho ya watoto. Katika hatua hii ya njia ya huduma, basi, watakuwa tayari—kwa hakika, wenye shauku hasa—kufahamu kikamilifu zaidi maisha ya Yule Ambaye mafundisho Yake yamewaathiri kwa undani sana, na kupata utambuzi wa kina zaidi wa mazingira ya kihistoria yanayoambatana na kuzaliwa na ukunjukaji wa pole pole wa Ufunuo Wake. Vitengo vitatu vinavyounda Kitabu cha 4 vinakusudia kuwapa washiriki fursa hii.

Maisha ya Mdhihirishaji wa Mungu, bila shaka, kimsingi ni tofauti na yale ya wanadamu wengine, na Ukuu Wake hauwezi kueleweka kwa kusoma tu matukio Yanayomzunguka. Katika miaka ambayo anaishi duniani, uwezo Wake wa ajabu unatawanywa juu ya sayari nzima, na kuleta mabadiliko katika uhalisia wa vitu vyote vilivyoumbwa na kuisukuma jamii ya wanadamu kuelekea kwenye hatua mpya ya maendeleo. Ingawa kwa macho ya nje maisha Yake yanaweza kuonekana yamejaa mateso, macho ya kiroho huona katika kila tukio dalili za utukufu na fahari Yake. Ili kuwaandaa washiriki kujifunza juu ya historia za maisha ya Báb na Bahá'u'lláh, yaliyojadiliwa katika kitengo cha pili na cha tatu mtawalia, cha kwanza huwataka kufikiria kuhusu umuhimu wa Siku hii tunamoishi, Siku ambayo imeshuhudia utokeaji wa Wadhihirishaji wawili wa Mungu.

Kitengo hiki ni kifupi kiasi. Kinajumuisha vifungu kadhaa kutoka maandiko ya Kibahá'í vinavyozungumzia juu ya ukuu wa Siku hii, sanjari na mazoezi machache rahisi. Kwa pamoja, haya yatawawezesha washiriki kutafakari siyo tu juu ya asili ya wakati huu katika historia, pale ambapo umoja wa binadamu hatimaye sasa unawezekana, bali juu ya majukumu ambayo maarifa haya yameweka juu ya kila mmoja wetu. Wale wanaohudumu kama wakufunzi wa Kitabu cha 4 sharti watambue kwamba kitengo hiki kinachukulia kuwa washiriki tayari wana uelewa wa awali wa baadhi ya dhana za msingi za Imani, walioupata kutoka yote mawili usomaji wa kozi za awali na kujihusisha kwao katika maisha ya jumuiya yao. Kwamba vitabu vyote vya dini vya zamani vimeongelea Siku iliyoahidiwa ya Mungu ambapo amani na haki vingesimikwa duniani, kwamba Bahá'u'lláh ameinua bendera ya amani ya ulimwengu na amewaagiza wanadamu kukiri umoja wake wa lazima, kwamba Yeye ameyakazia macho ya jumuiya ya wafuasi Wake kwenye lengo la utaratibu mpya wa ulimwengu—hizi ni miongoni mwa dhana zinazojadiliwa katika kitengo, "Ukuu wa Siku Hii".

Vitengo viwili vinavyofuata vinaandika maelezo ya matukio ambayo yameipeleka Imani mbele tangu jioni ile yenye jaala mnamo 1844, wakati Báb alipotangaza Ujumbe Wake, hadi saa za mapema za alfajiri takriban miaka hamsini baadaye wakati roho ya Bahá'u'lláh' ilipopaa kutoka ulimwengu huu wa uwepo. Masimulizi haya yenye mfuatano wa matukio hususan katika kitengo cha tatu kuhusu maisha ya Bahá'u'lláh, yanakamilishwa na vifungu kutoka Maandiko yanayoangazia baadhi ya dhima za kiroho zinazohusu utu wa Mdhihirishaji. Baadhi ya vifungu hivi hufuatiwa na mazoezi; vingine vinahitaji tu usomaji wa mara kwa mara na tafakari binafsi. Wakati huo huo, mkufunzi atataka kuhakikisha washiriki wanapata ujuzi kamili na wenye mpangilio wa maisha ya Báb na Bahá'u'lláh kadiri wanavyosoma vitengo hivi, ni zile kweli za kina za kiroho zinazoweza kubugwa kutoka visa katika mfululizo wa matukio yaliyoelezwa ndizo zenye umuhimu mkuu.

Katika kujiandaa kukiwezesha kikundi kupitia kitengo cha pili na cha tatu, hapo, mkufunzi anapaswa kufikiria kwa umakini dhima za kiroho zilizozungumziwa. Kwa mfano, miongoni mwao zimo dhima hizi, kwamba kila Mwangaza mtakatifu hudhihirishwa katika ulimwengu wa wanadamu siyo kwa hiari Yake, bali kwa Mapenzi ya Mungu, na Ambaye humjalia na Yeye elimu ya kiasili; kwamba wa kwanza kutambua Daraja Lake huagizwa kufanya vitendo vya ushujaa mkubwa, vitendo vinavyoshuhudia uwezo ubadilishao wa Imani Yake; kwamba Yeye anakubali kuvumilia maisha yenye mateso ili kuwaongoza wanadamu kwenye ukweli na kufanya Mapenzi na Kusudi la Mungu lijulikane kwa muumbo Wake; na kwamba hakuna nguvu duniani hata iwe na uwezo jinsi gani, inayoweza kudhoofisha ushawishi Wake au kumzuia Yeye kukamilisha Ujumbe Wake ambao kwao Yeye amekabidhiwa. Kuhusiana na hili, dhana moja muhimu inayoongelewa katika kitengo cha tatu ni ile ya hali ya hatari na ushindi. Uelewa wa dhana hii—kwamba kila hali ya hatari katika Hoja ya Mungu hutumika kuachilia kipimo kipya cha nguvu yake ya kiasili—ni muhimu kwa wale wote wanaotembea njia ya huduma, siyo tu kwamba waweze kutambua historia ya Imani, bali pia waweze kuchangia kwenye ukunjukaji wake thabiti katika ujirani na vijiji vyao, mchakato ambao hauepuki kupita kwenye mifuatano kadhaa ya hali za hatari na ushindi.

Tafakari juu ya dhima kama hizi itawasaidia washiriki kuona katika matukio yanayohusu maisha ya Báb na Bahá'u'lláh joto la upendo Wao kwa wanadamu na tabia iliyotukuka ya Jumbe Zao zinazofuatana. Itasaidia kuvutia mioyo yao karibu zaidi na Mdhihirishaji wa Mungu na kuweka imara hatua zao katika njia ya huduma kwa Hoja Yake. Pia itaendeleza uwezo wao wa kufanya mazungumzo na wengine kuhusu utu wa Bahá'u'lláh na Ufunuo Wake, uwezo ambao wamekuwa wakiukuza tangu waliposoma hadithi ya maisha Yake katika Kitabu cha 2. Kwa kuwa, uwezo wa kusimulia historia ya maisha Yake na maisha ya Mtangulizi Wake kwa namna ambayo hugusa moyo wa msikilizaji, zaidi ya yote, hutegemea uelewa wa umuhimu wa kiroho wa matukio yanayosimuliwa. Bila shaka, mazoezi mengi pia yanahitajika, na mkufunzi lazima ahakikishe kuwa washiriki wanapewa fursa ya kutosha ya kuhusisha visa katika mfululizo wa matukio moja kwa lingine kutoka maisha ya Wadhihirishaji Pacha. Baadhi ya washiriki wangeweza hata kuona inawezekana kutambulisha kile wanachojifunza katika mazungumzo yanayofanyika pamoja na marafiki na majirani kama sehemu ya mfuatano wa matembezi kwa kaya zao. Ili kuwasaidia katika haya na matukio mengineyo, kijitabu chenye michoro na maelezo mafupi kimeambatanishwa kwa kila kitengo cha historia. Kijitabu hiki kinaweza kurudufiwa kulingana na mahitaji au kinaweza kupakuliwa kutoka kwenye tovuti ya umma ya Taasisi ya Ruhi.

Ni muhimu kutaja hapa kwamba matukio yanayohusiana na maisha ya Wadhihirishaji Pacha yanaandikwa katika vitengo kulingana na tarehe za Kigregori ambapo yalitukia. Leo hii, kumbukizi za matukio muhimu kabisa huadhimishwa kwenye tarehe zake za Kibahá'í,

kulingana na maelezo ya kalenda ya Badí‘, na uwiano wake wa tarehe za Kigregori zinaweza kutofautiana mwaka hadi mwaka. Mkufunzi hahitaji kuingia katika mjadala kuhusu suala hili pamoja na washiriki wa kikundi; pole pole itakuwa dhahiri kwao kadiri wanavyoshiriki katika maadhimisho ya Siku Takatifu katika jumuiya yao. Kwa hakika, wakati wa shughuli hizi na zingine za pamoja, visa vya mfululizo wa matukio ya maisha ya Wadhihirishaji na ya siku za mwanzoni za Imani aghalabu husimuliwa, na hii itawapa washiriki umaizi zaidi katika mazingira ya kihistoria yaliyotoa msukumo wa awali kwa michakato wanayoiendeleza katika kijiji au ujirani wao leo.



# Ukuu wa Siku Hii

## Kusudi

Kupata umaizi juu ya umuhimu wa Siku hii na ahadi ilizonazo kwa wanadamu

## SEHEMU YA 1

Tumebarikiwa kuishi katika kipindi hiki maalum cha historia ya mwanadamu—kipindi kilichozinduliwa na Wadhihirishaji wawili wa Mungu, Bahá'u'lláh na Mtangulizi Wake Báb, waliokuja kuhuisha vitu vyote vilivyoumbwa. Tunaweza kutazama kwa macho yetu wenyewe, jinsi nguvu Walizoziachilia zinavyobadilisha jamii, jinsi ulimwengu wa zamani unavyotoweka na ule mpya unavyoanzishwa badala yake. Ni kweli, bila shaka, kwamba kufa kwa utaratibu wa zamani kunaambatana na mateso yasiyoelezeka. Hatuna budi ila kuathiriwa na kuhuzunishwa sana na uharibifu na mateso kwa kiwango kama hicho. Walakini hatuelemewi, kwa kuwa tunatambua kwamba ulimwengu unasonga mbele kwa uthabiti kuelekea kwenye ustaarabu mtukufu ambao Bahá'u'lláh ameutazamia.

Hii ni Siku ya Mungu. Kuishi katika Siku ya Mungu ni fadhili isiyopimika; humaanisha pia majukumu mazito. Kutambua ukubwa wa fadhili hii na kutimiza wajibu wetu ipasavyo, lazima tutafakari mara kwa mara juu ya umuhimu na ukuu wa Siku hii, na kuongeza zaidi uelewa wa kusudi la Mungu kwa wanadamu. Kusudi la kitengo hiki, ambacho ni kifupi kiasi, ni kuwafahamisha baadhi ya vifungu kutoka katika Maandiko ya Kibahá'í vinavyoongelea umuhimu wa zama tunamoishi. Kabla ya kujifunza vifungu hivi na kutafakari juu ya maana zake, unaweza kuona kuwa inafaa kwako na wenzako katika kikundi chenu kubaini baadhi ya malengo ambayo Mungu amekusudia kwa ajili ya jamii ya wanadamu leo. Tunajua kwamba muungamo wa watu wote wa ulimwengu katika familia moja ya wote ni miongoni mwa malengo yanayotakiwa kufikiwa katika zama hizi. Ni yapi mengine machache?

________________________________________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

________________________________________________________

## SEHEMU YA 2

Bahá'u'lláh husema:

> **"Kwa kweli Mimi nasema, hii ndiyo ile siku ambamo binadamu wanaweza kuutazama Uso, na kusikia Sauti ya Yule Mwahidiwa. Mwito wa Mungu umepaazwa, na nuru ya wajihi Wake imeinuliwa juu ya watu. Inambidi kila mtu kufutilia mbali dalili ya kila neno la upuuzi kutoka ubao wa moyo wake, na kutazama, kwa akili iliyo wazi na isiyo na upendeleo, juu ya ishara za Ufunuo Wake, mathibitisho ya Ujumbe Wake, na alama za utukufu Wake"**[1]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Katika Siku hii, tunaweza kuuona _______________ , na kusikia ____________ ya Yule Mwahidiwa.

b. __________________________ umepaazwa, na ___________________ wa ________________ Wake umeinuliwa juu yetu.

c. Ni wajibu wetu kufuta __________________ ya kila _________________ , na kuutazama, kwa akili na _______________ , juu ya _____________ za Ufunuo Wake, ________________ ya Ujumbe Wake, na ____________ za Utukufu Wake.

2. Ni yapi kati ya yafuatayo ni mawazo ambayo huwazuia watu kuutambua ukweli wa Ufunuo wa Bahá'u'lláh?

_____ "Dini ya wazazi wangu inanitosha."

_____ "Jamii ya wanadamu ipo katika uhitaji wa majira ya machipuko ya kiroho."

_____ "Dini ni nzuri kwa wale wanaoihitaji."

_____ "Dini ni chanzo tu cha ugomvi, hivyo tuachane nayo."

_____ "Kadiri nionavyo mimi, dini zote takriban ni sawa; hakuna tofauti yoyote ipi unaifuata."

_____ "Mungu ameitelekeza jamii ya wanadamu."

_____ "Mambo yote sharti yafanywe upya, ikiwemo dini."

_____ "Sayansi huthibitisha kwamba hakuna Mungu. Matatizo yetu yote yanaweza kutatulika ikiwa tutatumia uwezo wa akili"

_____ "Sitaki kujifungamanisha mwenyewe na dini yoyote."

_____ "Sihitaji dini ili miwe wa kiroho."

_____ "Kila mtu binafsi anapaswa aruhusiwe kumjua Mungu kwa namna yake mwenyewe. Kwa nini tumhitaji Mdhihirishaji?"

_____ "Tuna Maandiko Matakatifu ya dini yetu wenyewe. Hakuna haja ya Mdhihirishaji mpya."

3. Ni zipi kati ya zifuatazo ni miongoni mwa alama za Utukufu wa Bahá'u'lláh?

_____ Ufasaha wa matamshi Yake

_____ Uwezo upenyezao wa Maneno Yake

_____ Mabadiliko yanayotokea ndani ya mioyo ya wale wanaokutana na Maandiko Yake

_____ Athari ambayo Mafundisho Yake yanayo juu ya mawazo na vitendo vya watu

_____ Athari ambayo Mafundisho Yake yanayo juu ya mwelekeo wa historia

_____ Ubora wa muono Wake kwa ajili ya mustakabali wa jamii ya wanadamu

_____ Mateso na taabu ambazo Yeye alivumilia kwa ajili ya wanadamu

_____ Mamlaka Yake licha ya kuwa chombo cha kuteswa na nguvu za kidunia

_____ Nguvu ya mafundisho Yake ya kuunganisha watu wa kila dini na usuli

_____ Ukuaji thabiti wa jumuiya ya wafuasi Wake

_____ Nguvu ya Agano Lake kushinda kila kizuizi na kudumisha umoja wa Hoja Yake

_____ Utukufu wa Utaratibu Wake wa Kiutawala

_____ Jinsi ulimwengu unavyosonga mbele kuelekea kile Alichokitazamia

## SEHEMU YA 3

Bahá'u'lláh husema:

**"Ni kuu kwa hakika Siku hii! Vidokezo vilivyotajwa juu yake katika Maandiko yote Matakatifu kama Siku ya Mungu huthibitisha ukuu wake. Roho ya kila Mtume wa Mungu, ya kila Mjumbe Mtakatifu, imeitamani sana Siku hii ya ajabu. Koo zote mbalimbali za dunia, kadhalika, zimetamani sana kuifikia. Walakini, punde tu Nyota ya Mchana ya Ufunuo Wake ilipojidhihirisha katika mbingu ya Mapenzi ya Mungu, ndipo wote isipokuwa wale ambao Mwenyezi alipendezwa kuwaongoza, walipokutwa wamepigwa na bumbuwazi na wasiojali."**[2]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. ____________ kwa hakika Siku hii! Vidokezo ambavyo vimetajwa juu yake katika _____________ yote ____________ kama ____________________ vinashuhudia _____________ wake.

   b. Roho ya kila _______________ wa Mungu, ya kila _________________ _______________ , ime ________________ Siku hii ya _______________ .

   c. ___________________________ za dunia, kadhalika, ______________________ ______________________ .

   d. Punde tu Nyota ya Mchana ya Ufunuo Wake _________________ , ndipo wote isipokuwa wale ambao ______________________________________________ , walikutwa ______________________ na _________________ .

2. Kutokana na kifungu cha hapo juu, ni dhahiri kwamba Siku hii ni siku ya utimilizo. Mitume na Wajumbe wote wa Mungu wametabiri kuja kwa Siku ambapo amani na upatano vitasimikwa duniani. Bahá'u'lláh anarejelea katika kifungu kwa wale ambao, ingawa walisubiri kwa shauku Siku iliyoahidiwa, hawakumkubali Yeye pale Alipotangaza ujio wake. Taswira nyingi huja akilini pale mtu anapofikiri juu ya roho inayomtambua Bahá'u'lláh. Jaza katika kila nafasi za hapo chini kwa maneno yanayofaa: kuamka, yakini, kutambua, kuamini, tumaini.

   a. Kupita kutoka usingizini hadi __________________________________________

   b. Kupita kutoka uzembe hadi ___________________________________________

c. Kupita kutoka ukataji tamaa hadi ____________________

d. Kupita kutoka tuhuma hadi ____________________

e. Kupita kutoka shaka hadi ____________________

3. Unafikiri ni kitu gani kinachoweza kuufungua moyo kwa Ufunuo wa Bahá’u’lláh?

## SEHEMU YA 4

Bahá’u’lláh hueleza:

**“Hii ndiyo Siku ambamo fadhili bora kabisa za Mungu zimemiminwa juu ya watu, Siku ambamo neema Yake yenye nguvu kabisa imeingizwa ndani ya viumbe vyote. Inawapasa watu wote wa ulimwengu kusuluhisha tofauti zao, na, kwa umoja na amani kamili, waishi chini ya kivuli cha Mti wa uangalizi na wema Wake wa upendo. Inawabidi kushikilia chochote kile ambacho, katika Siku hii, kitachangia kwenye utukuzaji wa madaraja yao, na kwenye uendelezaji wa maslahi yao bora kabisa.”**[3]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

a. Katika Siku hii, ____________ bora kabisa za Mungu ____________ juu ya wanadamu.

b. Katika Siku hii, ____________ ya Mungu yenye nguvu kabisa ____________ ndani ya viumbe vyote.

c. Watu wote wa ulimwengu lazima ____________ zao, na, kwa ____________ , na, ____________ waishi chini ya kivuli cha ____________ wa ____________ na ____________ .

d. Watu wa ulimwengu inawabidi kushikilia chochote kile ambacho kitachangia kwenye ____________ wa ____________ yao, na kwenye ____________ wa ____________ .

2. Ni zipi baadhi ya “fadhili bora kabisa” ambazo Mungu amewajalia wanadamu katika Siku hii? ____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________

3. Je, neno “changia kwenye” humaanisha nini? ______________________________
______________________________________________________________________

4. Orodhesha yale mambo unayoweza kufanya ili kuendeleza maslahi bora kabisa ya wanadamu: ______________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 5

Bahá’u’lláh hueleza:

**“Hii ndiyo Siku ambamo Bahari ya rehema ya Mungu imedhihirishwa kwa watu, ile Siku ambamo Nyota ya Mchana ya wema Wake wa upendo imetawanya wangavu wake juu yao, Siku ambamo mawingu ya fadhili Yake ya ukarimu yameifunika jamii nzima ya wanadamu. Sasa ni wakati wa kuwachangamsha na kuwaburudisha wale wenye huzuni kwa upepo mwanana uhuishao wa upendo na urafiki, na maji ya uzima ya urafiki na hisani.”**[4]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Katika Siku hii, Bahari ya ________________ ya Mungu ___________________ kwa wanadamu.

   b. Katika Siku hii, Nyota ya Mchana ya ______________________________ __________________________ Wake juu ya wanadamu.

   c. Katika Siku hii, mawingu ya _________________ Yake _______________ jamii nzima ya binadamu.

   d. ___________ ni wakati wa ________________na _______________ wale wenye huzuni kwa upepo mwanana uhuishao wa _____________ na _____________ , na maji ya uzima ya ____________ na _____________ .

2. Yapi kati ya yafuatayo huwachangamsha na kuwainua watu?

_____ Kuujipatia elimu

_____ Kuongeza uwezo wa kushauriana

_____ Kutazamwa kwa huruma

_____ Kunufaika kutokana na maendeleo ya kisayansi

_____ Kushawishika kuunga mkono chama au kikundi kimoja au kingine cha kisiasa

_____ Kusoma na kushiriki na wengine Neno la Mungu

_____ Kushawishiwa kununua kwa mkopo vitu ambavyo hawavihitaji

_____ Kuwa na utambuzi mkubwa zaidi wa umuhimu wa sala

_____ Kutiwa moyo katika jitihada zao

_____ Kuwezeshwa kuwasilisha malalamiko kwa ufasaha kwa mamlaka kupitia njia za kisheria

_____ Kushiriki katika maandamano

_____ Kunywa pombe ili kusahau matatizo yao

_____ Kupata manufaa ya mfumo wa kiafya

_____ Kuwa na klabu ya usiku katika ujirani kama mahali pa kujiburudisha

_____ Kumtambua Mdhihirishaji wa Mungu wa siku hii

_____ Kutegemea juu ya uwezo wa msaada mtakatifu

## SEHEMU YA 6

Bahá'u'lláh husema:

**"Mizania ya ulimwengu imevurugwa kupitia nguvu itetemeshayo ya Utaratibu huu mpya wa Ulimwengu, huu mkuu kabisa. Maisha yaliyotengamaa ya wanadamu yamevurugwa kupitia utendaji wa Mfumo huu wa kipekee, huu wa ajabu—ambao mfano wake macho ya umauti kamwe hayajapata kushuhudia.**

**"Jizamisheni wenyewe katika bahari ya maneno Yangu, ili muweze kufumbua siri zake, na kugundua lulu zote za hekima zilizofichika katika vina vyake. Jihadharini msiyumbe-yumbe katika dhamira yenu ya kuukumbatia ukweli wa Hoja hii—Hoja ambayo kupitia kwayo uwezo wa nguvu ya Mungu umefunuliwa, na mamlaka Yake kusimikwa."**[5]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

a. _______________ ya ulimwengu ________________ kupitia _______________ itetemeshayo ya _______________ huu mpya wa __________________ , huu mkuu ______________ .

b. ________________________ ya wanadamu _________________ kupitia utendaji wa _________________________ , huu wa ajabu.

c. Sharti __________________ wenyewe katika ___________ ya maneno Yake, ili tuweze _________________ zake, na _____________ lulu zote za ___________ zilizofichika katika vina vyake.

d. ________________ katika _________ yetu kuukumbatia _________ wa Hoja hii.

e. Hii ni Hoja ambayo kupitia kwayo _______________ wa __________ ya Mungu _______________ , na ______________ Yake kusimikwa .

2. Nini maana ya neno "mizania"? __________________________________________

____________________________________________________________________

3. Nini kimeivuruga mizania yu ulimwengu? ___________________________________

____________________________________________________________________

4. Ni zipi baadhi ya ishara zinazoonesha kwamba ulimwengu umepoteza mizania yake?

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

5. Ni zipi baadhi ya ishara zinazoonesha kwamba maisha ya wanadamu yamepinduliwa?

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

6. Ni upi huu "Mfumo wa ajabu" ambao Bahá'u'lláh anauongelea? _______________

____________________________________________________________________

7. Tunajizamishaje wenyewe katika bahari ya maneno ya Bahá'u'lláh? ____________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

8. Jinsi gani fikira zetu huathiriwa tunapojizamishapo wenyewe katika bahari ya maneno Yake? ____________________

9. Jinsi gani vitendo vyetu huathiriwa tunapojizamisha katika bahari ya maneno Yake? ____________________

10. Kutoka wapi tunapokea nguvu zetu za kiroho zinazohitajika kufanya kazi ya kusimika Utaratibu wa Ulimwengu wa Bahá'u'lláh? ____________________

11. Neno "kuyumba-yumba" humaanisha nini? ____________________

12. Jinsi gani nguvu zetu za kiroho huathiriwa kama tukiyumba-yumba katika kuukubali ukweli wa Hoja Yake katika ukamilifu wake? ____________________

## SEHEMU YA 7

'Abdu'l-Bahá hutueleza maneno haya:

**"Enyi wapendwa wa Bwana! Siku hii ni siku ya muungano, siku ya mkusanyiko wa wanadamu wote. 'Kwa kweli Mungu huwapenda wale ambao, mithili ya ukuta imara, hupigania Hoja Yake katika safu zilizojipanga bega kwa bega!' Kumbuka kwamba Yeye husema 'katika safu zilizosimama bega kwa bega'—ikimaanisha kusongamana bila kuacha nafasi, kila mmoja akishikamana kwa anayefuata, kila mmoja akisaidiana na wenzake. Kupigana, kama ilivyoelezwa katika aya hiyo takatifu, katika kipindi hiki kitakatifu na kikuu kuliko vyote, haimaanishi, kujitokeza kwa upanga na mkuki, kwa fumo na mishale ipenyezayo—bali kwa silaha yenye dhamira safi, kwa nia adilifu, kwa nasaha zenye msaada na zinazofaa, kwa sifa za uchaji Mungu, kwa vitendo vimpendezavyo Mwenyezi, kwa sifa za mbinguni. Humaanisha elimu kwa wanadamu wote, uongozi kwa watu**

**wote, uenezaji wa harufu nzuri za roho kwa marefu na mapana, utangazaji wa mathibitisho ya Mungu, uanzishwaji wa hoja zenye kuthibitisha na takatifu, ufanyaji wa vitendo vya hisani.”**[6]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. ‘Abdu’l-Bahá hutuambia kwamba siku hii ni siku ya ______________ , siku ya ______________ , wa _____________ wote.

   b. Yeye hueleza kwamba Mungu _____________ wale ambao, mithili ya _________________ , ____________________ kwa ajili ya Hoja Yake katika ___________________________ .

   c. Kuwa “katika safu zilizojipanga bega kwa bega”, ‘Abdu’l-Bahá hueleza, humaanisha ___________________________ , kila mmoja _____________ kwa anayefuata, kila mmoja __________________ na wenzake.

   d. Kupigana katika huduma kwa Hoja katika _____________ hiki kitakatifu na kikuu kuliko vyote, Yeye hutuambia, haimaanishi kujitokeza kwa ______________ na _________ , kwa __________ na ____________________ bali kwa ___________ yenye _________________________ , kwa ____________________ , kwa ______________________________ , kwa ____________________________ , kwa ___________________________ , kwa __________________________ .

   e. Vivyo hivyo, kupigana katika kipindi hiki kitakatifu humaanisha __________ kwa wanadamu wote, __________ kwa wanadamu wote, _______________________ , wa Mungu, ___________________________________________ , ___________ wa ______________ ya Mungu, _____________ wa ______________________ ____________________ , ___________ wa ___________________ .

2. Hii ndiyo siku ya muungano wa wanadamu. Ili kutambua jinsi gani kazi hizi zilivyo kubwa mbele yetu, fikiria juu ya migawanyiko isiyohesabika ambayo kwayo wanadamu wamegawanyika wenyewe. Orodhesha migawanyiko mingi kadiri uwezavyo.

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

________________________________________________________________
________________________________________________________________
________________________________________________________________
________________________________________________________________
________________________________________________________________
________________________________________________________________
________________________________________________________________
________________________________________________________________

3. Nguvu gani inayoweza kuiondoa migawanyiko yote hii? ______________________
________________________________________________________________

4. Ni ipi asili ya mapigano tunayojihusisha nayo?______________________________
________________________________________________________________

5. Ni zipi miongoni mwa silaha zifuatazo hutumika katika mapigano haya:

_____ Dhamira safi
_____ Sifa za uchaji Mungu
_____ Nia adilifu
_____ Uchu wa madaraka
_____ Ufidhuli na kiburi
_____ Shauku ya haki
_____ Kujiona mwadilifu
_____ Bunduki
_____ Visu
_____ Nguvu ya Neno la Mungu
_____ Kujiridhisha
_____ Kujikweza
_____ Hasira
_____ Ukarimu
_____ Nguvu ya sala
_____ Vitendo vistahilivyo sifa
_____ Upendo wa Mungu
_____ Upendo kwa wanadamu
_____ Kumwamini Mungu
_____ Ushauri wenye msaada na ufaao
_____ Nguvu ya umoja
_____ Fedha
_____ Imani
_____ Unyenyekevu

6. Je, ni sawa kujaribu kuwatawala wengine ili kuleta haki?______________________

7. Ni yapi kati ya yafuatayo huwakilisha mambo tunayofanya wakati tunapojihusisha katika vita vya kiroho ili kuunganisha jamii ya wanadamu?

_____ Kuendeleza elimu
_____ Kuwalazimisha wengine kufanya tunayoyataka
_____ Kufundisha Hoja ya Mungu

______ Kutangaza Hoja ya Mungu

______ Kugawanyika katika makundi kulingana na maslahi yetu wenyewe

______ Kupigania maslahi ya kundi tulilomo

______ Kufanya vitendo vya hisani

______ Kuanzisha hoja zenye kuthibitisho ukweli wa Ufunuo wa Bahá'u'lláh

______ Kujizamisha wenyewe katika bahari ya maneno Yake

______ Kuwakandamiza wanyonge na wadhalili

______ Kusali kwa shauku

______ Kupora mali za watu

______ Kujilimbikizia mali kwa kuwaibia wengine

## SEHEMU YA 8

Utambuzi wa hali ya juu wa ukuu wa Siku hii huumba ndani mwetu sisi sote shauku ya kuinuka kufundisha, kuhudumu, na kufanya vitendo vya dhabihu. Ili kutokupoteza muono wa haraka na muhimu ambao kwao sharti ujihusishe nao katika kufanya vitendo vya huduma kwa Hoja, kariri kifungu kifuatacho kutoka barua iliyoandikwa na Mlinzi:

> **"Hakuna wakati wa kupoteza. Hakuna nafasi iliyoachwa ya kuyumba. Watu wengi mno hutamani sana Mkate wa Uhai. Jukwaa limeandaliwa. Ahadi thabiti na isiyobadilika imetolewa. Mpango wa Mungu umeanzishwa. Unajipatia nguvu kila siku ipitayo. Nguvu zisizoelezeka za mbinguni na duniani husaidia katika utekelezwaji wake. Fursa kama hiyo haina mbadala. Mwache mwenye shaka ainuke, na yeye mwenyewe athibitishe ukweli wa madai hayo. Kujaribu, kustahimili, ni kuhakikisha ushindi wa mwisho na kamili."**[7]

## MAREJELEO


1. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, chapisho la 1983, 2017), VII, aya. 1, uk. 10 (toleo la Kiingereza).

2. Kama hapo juu., VII, aya. 2, ku. 10–11 (toleo la Kiingereza).

3. Kama hapo juu., IV, aya. 1, uk. 5 (toleo la Kiingereza).

4. Kama hapo juu., V, aya. 1, uk. 6 (toleo la Kiingereza).

5. Kama hapo juu., LXX, aya. 1–2, uk. 154 (toleo la Kiingereza).

6. *Mateuzi kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, chapisho la 2010, 2015), na. 207.2, ku. 159–60 (toleo la Kiingereza).

7. Kutoka barua ya 28 Januari 1939, iliyochapishwa katika *Saa Hii ya Mkataa: Jumbe kutoka kwa Shoghi Effendi kwenda kwa Wabahá'í wa Marekani ya Kaskazini, 1932–1946* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2002), uk. 28.

# Maisha ya Báb

## Kusudi

Kupata utambuzi wa nguvu
ya kipindi kifupi cha kuvutia cha Utumishi wa Báb
na kujifunza kusimulia historia ya maisha Yake

# SEHEMU YA 1

Kipindi Kitakatibu cha Báb kilianza mnamo 1844 na kilidumu kwa miaka tisa tu. Kusudi lake la msingi lilikuwa ni kuandaa njia kwa ajili ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh. Ingawa kipindi cha Utumishi wa Báb kilikuwa kifupi, uwezo ulioachiliwa na Ufunuo Wake ulikuwa wenye nguvu mno kiasi kwamba athari yake itagusa mamia ya vizazi vijavyo.

Báb, Ambaye jina lake lilikuwa Siyyid 'Alí-Muhammad, alizaliwa mnamo 20 Oktoba 1819 huko Shíráz, jiji lililoko kusini mwa Iran, pia ilijulikana kama Uajemi. Watu wengi sana huko Uajemi walikuwa wa madhehebu ya Uislam ambao husubiri ujio wa Yule Mwahidiwa wa Mungu aitwaye Qá'im. Jina "Qá'im" maana yake ni "Yule atakayeinuka".

Báb alitokana na familia mashuhuri ambayo ilikuwa ya nasaba ya Muhammad, Mtume wa Uislam. Baba Yake alifariki alipokuwa angali mtoto mdogo, na Yeye alilelewa na mjomba Wake. Báb alijaliwa ujuzi wa kiasili na hakuhitaji kwenda shule, lakini Alifuata mapenzi ya mjomba Wake ambaye alimpeleka shule alipokuwa na umri mdogo. Hata hivyo, mwalimu Wake aliutambua mara moja uwezo mkubwa wa Báb na alielewa kwamba hakuwa na chochote cha kumfundisha mtoto huyo asiye wa kawaida. Yeye alisimulia hadithi ifuatayo kuhusu maisha ya shuleni ya Báb:

> "Siku moja nilimuomba Báb kutongoa maneno ya ufunguzi ya Qur'án . . . Yeye alisita, akaomba kwamba mpaka aambiwe kwanza maana ya maneno hayo la sivyo asingethubutu kuyatamka. Nilijifanya kutojua maana yake. 'Mimi najua maana ya maneno haya,' alisema mwanafunzi wangu; 'kwa ruhusa yako, nitayaelezea.' Alizungumza kwa ujuzi na ufasaha mkubwa mno kiasi kwamba nilishikwa na mshangao. . . . Utamu wa matamshi Yake bado ungali unaishi katika kumbukumbu yangu. Nilihamasika kumrudisha kwa mjomba Wake na kuwasilisha mikononi mwake Dhamana ambayo aliikabidhi katika uangalizi wangu. Nilidhamiria kumwambia jinsi nilivyojisikia kuwa sikustahili kumfundisha mtoto asiye wa kawaida kama huyo. Nilimkuta mjomba Wake peke yake ofisini kwake. 'Nimemrudisha kwako,' nilisema, 'na Ninamkabidhi katika ulinzi wako wenye hadhari. Yeye si wa kutendewa kama mtoto wa kawaida tu, kwani ndani Mwake tayari naweza kuona shuhuda za ule uwezo usioelezeka ambao Ufunuo wa Qá'im peke yake ndio unaweza kuufunua. Imekupasa Kumuweka katika uangalizi wako wa upendo mwingi kabisa. Mhifadhi katika nyumba yako, kwa kuwa Yeye, kwa kweli, hahitaji walimu kama mimi.' Mjomba Wake kwa ukali alimkaripia Báb. 'Umesahau maagizo yangu?' alisema. 'Kwani Sijakuonya kufuata mfano wa wanafunzi Wenzako, kuwa kimya na kusikiliza kwa makini kila neno analolisema mwalimu Wako?' Baada ya kupata ahadi Yake ya kutii kwa uaminifu maagizo yake, mjomba alimtaka Báb arudi shuleni. Hata hivyo, roho ya mtoto yule haikuweza kuzuiliwa na maonyo makali ya mjomba Wake. Hakuna elimu ambayo ingeweza kuzuia mtiririko wa ujuzi Wake wa kiasili. Siku hadi siku Aliendelea kudhihirisha mathibitisho ya ajabu mno ya hekima ipitayo uwezo wa kibinadamu, kiasi kwamba sina uwezo wa kusimulia."[1]

Hatimaye Báb aliruhusiwa kuacha shule. Ndipo alipoanza kufanya kazi na mjomba Wake kama mfanya biashara huko Búshihr, mji ulioko kusini magharibi mwa Shíráz. Katika kipindi hicho, Báb alioa. Yeye na mkewe walibahatika kupata mtoto wa kiume aliyeitwa Aḥmad, ambaye alifariki akiwa bado mchanga mwaka mmoja kabla Báb hajajitangaza Mwenyewe kuwa Qá'im Aliyeahidiwa.

Akiwa kijana, Báb alionesha ishara za uwezo na ukuu ambao hakuna yeyote awezaye kuushinda. Sifa za kipekee ambazo zingeweza kumpambanua Yeye katika kipindi chote cha Utume Wake, cha kasi na chenye huzuni, tayari zilikuwa zimedhihirika. Mlinzi anamrejelea Yeye kama "utu wenye upole, ujana usiokatalika wa Báb, katika unyenyekevu Wake usio na kifani, katika utulivu Wake usiohangaishwa, katika matamshi Yake yenye mvuto". Sehemu zinazofuata zinaweza kuelezea kwa uchache tu matukio ya maisha Yake. Lakini hata maelezo haya mafupi yanapaswa kuwasha katika mioyo yetu cheche za moto wa upendo ambao Yeye aliuwasha katika mioyo ya maelfu na maelfu huko Uajemi na kwingineko.

1. Ni lipi lilikuwa jina la Báb? ______________________________

2. Ni wapi Báb alizaliwa na ilikuwa tarehe ngapi? ______________________________

______________________________

3. Je, jina "Qá'im" lina maana gani? ______________________________

4. Familia ya Báb kiasili ilitokea katika nasaba ya nani? ______________________________

______________________________

5. Ni nani aliyekuwa na wajibu wa kumlea Báb baada ya kufariki Baba yake? ________

______________________________

6. Je, nini maana ya kauli kwamba 'Báb alijaliwa na Mungu ujuzi wa kiasili'? ________

______________________________

7. Je, mwalimu wa Báb alifikiri nini alipoutambua uwezo Wake mkuu? ____________

______________________________

8. Je, kirai "hekima ipitayo uwezo wa binadamu" humaanisha nini? ________________

______________________________

9. Je, Báb alifanya nini baada ya kuacha shule?______________________________

______________________________

10. Ni kwa maneno gani Mlinzi anamrejelea Báb? ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

11. Andika kwa maneno yako mwenyewe hadithi ya maisha ya Báb akiwa shule, kama ilivyoelezwa na mwalimu Wake.

## SEHEMU YA 2

Kabla Báb hajatangaza Ujumbe Wake, watu kadhaa kote ulimwenguni walijua ndani kabisa ya mioyo yao kwamba Siku mpya ilikuwa inakaribia kupambazuka. Miongoni mwao Siyyid Káẓim, mtu mtakatifu ambaye aliishi katika mji wa Karbilá nchini ‘Iráq. Siyyid Káẓim alikuwa na wanafunzi wengi, na aliyatoa maisha yake akiwaandaa kwa ajili ya ujio wa Qá’im aliyekuwa akisubiriwa sana kwa muda mrefu. Yeye aliwaambia mara kwa mara kwamba baada ya kifo chake, ingewabidi kuyaacha makazi yao kwa mioyo iliyojitenga na tamaa zote za kidunia, waende kumtafuta yule mwahidiwa Mpendwa.

Baada ya Siyyid Káẓim kufariki, mwanafunzi wake mwenye kuheshimika, Mullá Ḥusayn, alisali na kutaamali kwa kipindi cha siku arobaini, wakati ambapo aliufungua moyo wake wote ili kupata uvuvio wa Mungu. Kisha aliondoka ‘Iráq pamoja na wenzi wake wawili kwa ajili ya kumtafuta Yule Mwahidiwa. Kwanza alikwenda Búshihr. Hata hivyo hakukaa huko kwa muda mrefu, kwani alihisi kuvutwa bila kuzuilika kuelekea kaskazini katika mji wa Shíráz. Alipoluwa akiukaribia mji huo, yeye aliwaambia wenzi wake watangulie kwenda msikitini na wamsubiri angewakuta huko.

Saa chache kabla ya machweo, nje kidogo ya lango la mji wa Shíráz, alikutana na kijana mashuhuri Ambaye alimkaribisha na kumwalika nyumbani Kwake ili kujipumzisha baada ya safari ndefu na ngumu. Mullá Ḥusayn alivutiwa sana kwa namna ya upole lakini thabiti ambayo Kijana huyu asiye wa kawaida alizungumza. Aliambatana naye na punde walifika kwenye mlango wa nyumba moja ya kawaida. Waliingia ndani na kwenda moja kwa moja kukaa

kwenye chumba cha juu. Mwenyeji wake mkarimu aliagiza liletwe gudulia la maji ili mgeni Wake aweze kunawa mavumbi ya safari zake. Kisha Yeye Mwenyewe aliandaa chai na kumkaribisha Mullá Ḥusayn. Baada ya vitendo hivi vya ukarimu, Yeye alianza kuzungumza. Tondoti za mazungumzo hayo ya kihistoria baadaye yalisimuliwa na Mullá Ḥusayn:

> "Ilikuwa imepita takriban saa moja baada ya machweo, ndipo Mwenyeji wangu kijana alipoanza kuzungumza na mimi. 'Nani, baada ya Siyyid Káẓim', Yeye Aliniuliza, 'unafikiri anaweza kuwa mrithi wake na kiongozi wenu?' 'Wakati wa kifo chake,' nilimjibu, 'mwalimu wetu aliyetutoka kwa msisitizo alitusihi kuacha makazi yetu, kutawanyika kwa mapana na marefu, katika kumtafuta Mpendwa mwahidiwa. Kulingana na maagizo hayo, nimesafiri hadi Uajemi, nimeinuka kukamilisha mapenzi yake, na ningali namtafuta.' 'Je, mwalimu wenu,' Yeye aliendelea kuuliza, ¿'aliwapa maelezo yoyote ya kina kuhusu ishara bainifu za kumtambua Yule Mwahidiwa?' 'Naam,' nilijibu, 'Yeye anatoka katika nasaba safi, wa ukoo maarufu, na wa uzao wa Fátimih. Na kuhusu umri Wake, Yeye ana zaidi ya miaka ishirini na chini ya miaka 30. Yeye amejaliwa ujuzi wa kiasili. Ana kimo cha wastani, havuti tumbaku, na hana dosari mwilini.' Yeye alisita kidogo na kisha kwa sauti yenye mtetemo alitamka: 'Tazama, dalili zote hizi zinadhihirika ndani Mwangu!' Kisha alifikiria kila mojawapo ya dalili zilizotajwa hapo juu, na hatimaye alithibitisha kwamba zote zilihusiana na utu Wake."[2]

Jioni ile, Báb alimthibitishia Mullá Ḥusayn, kwa ushahidi ulio wazi na dhahiri, kwamba Yeye ndiye alikuwa Yule Qá'im Mwahidiwa. Yeye alifunua, kwa wepesi wa kushangaza, sehemu ya kwanza ya fasiri yake juu ya Súra ya Yusufu, sura muhimu ya Qur'an. Kisha Yeye akamwambia Mullá Ḥusayn maneno haya:

> "Ewe ambaye ni wa kwanza kuniamini Mimi! Kwa kweli nasema, Mimi ni Báb, Lango la Mungu, na wewe u Bábu'l-Báb, lango la Lango hilo. Roho kumi na nane lazima, hapo mwanzoni, wao wenyewe na kwa hiari yao wenyewe, wanikubali na watambue ukweli wa Ufunuo Wangu. Bila kuonywa na bila kualikwa, kila mmoja wao lazima atafute kwa uhuru kunifuata Mimi. Na idadi yao itakapokamilika, mmoja wao lazima achaguliwe kufuatana Nami katika hija Yangu huko Makka na Madina. Huko nitawasilisha Ujumbe wa Mungu kwa Sharíf wa Makka. Kisha nitarudi Kúfih, ambako tena ndani ya msikiti wa mji huo mtakatifu, Nitadhihirisha Hoja Yake. Inakubidi usifunue, ama kwa wenzi wako au kwa roho nyingine yoyote ile, kile ambacho umekiona na kukisikia."[3]

Ufunuo huu mtukufu uliijaza roho ya Mullá Ḥusayn msisimko na shangwe, kicho na mshangao. "Jinsi gani nilivyojihisi dhaifu na asiye na nguvu, aliyekata tamaa na mwoga, kama nilivyojihisi hapo mwanzoni!" baadaye alisema. "Wakati huo sikuweza kuandika wala kutembea, kwa jinsi mikono na miguu yangu ilivyotetemeka. Sasa, walakini, utambuzi wa Ufunuo Wake umeamsha nafsi yangu. Nilijisikia mwenye ujasiri na nguvu mno kiasi kwamba laiti ulimwengu, watu wake na watawala wake wote, wangeinuka dhidi yangu, mimi, pekee na pasipo hofu, ningehimili mashambulizi yao. Ulimwengu ulionekana kama konzi ya vumbi tu mkononi mwangu. Nilikuwa kama Sauti ya nafsi ya Gabriel, nikiwaita wanadamu wote: 'Amkeni, kwani, tazama! Mwanga wa asubuhi umechomoza. Inukeni, kwani Hoja Yake imedhihirishwa. Mlango wa neema Yake u wazi kabisa; ingieni humo, Enyi watu wa ulimwengu! Kwani Yule Ambaye ni Mwahidiwa wenu Amekuja!'"[4]

Tangazo la Báb lilifanyika 23 Mei 1844. Alikuwa na miaka ishirini na mitano. Miongo kadhaa baadaye katika tukio la siku ya kumbukizi ya Tangazo la Báb, ‘Abdu’l-Bahá aliwahutubia wale waliokusanyika kwa maneno yafuatayo:

> **“Hii ni tarehe 23 Mei, siku ya kuadhimisha kumbukizi ya ujumbe na Tangazo la Báb. Ni siku iliyobarikiwa na alfajiri ya udhihirisho, kwani kutokea kwa Báb kulikuwa mwanga wa awali wa asubuhi ya kweli, . . . ni siku iliyobarikiwa, chanzo cha fadhili za mbinguni, mwanzo wa mng’ao mtakatifu. Siku kama hii mwaka 1844 Báb alitumwa kupiga mbiu na kutangaza Ufalme wa Mungu, akitangaza habari za furaha za ujio wa Bahá’u’lláh na kuhimili upinzani wa taifa zima la Uajemi.”**[5]

1. Siyyid Káẓim aliwaambia wanafunzi wake wafanye nini pale yeye atakapofariki? __

______________________________________________

______________________________________________

2. Mullá Ḥusayn alifanya nini baada ya kufariki kwa Siyyid Káẓim? ________________

______________________________________________

______________________________________________

3. Jinsi gani Báb alijua kwamba Mullá Ḥusayn alikuwa amewasili Shíráz? ___________

______________________________________________

4. Ni maswali gani Báb alimuuliza Mullá Ḥusayn baada ya kufika nyumbani Kwake?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

5. Ni ishara gani Siyyid Káẓim aliwapa wanafunzi wake zinazohusiana na utu wa yule Qá’im?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

6. Fátimih ni binti wa nani, na ina maana gani “kuwa wa nasaba yake”? ____________

7. Je, Báb alikuwa na zile sifa ambazo Mullá Ḥusayn alikuwa akizitafuta? __________

8. Je, jina “Báb” lina maana gani? ______________________________________

9. Je, ni jina gani Báb alimpa Mullá Ḥusayn? _______________________________

10. Je, jina hili lina maana gani? ______________________________________

11. Ni nini ilibidi kitokee kwanza kabla Báb kutangaza wazi Hoja Yake? ____________

12. Eleza kwa maneno yako mwenyewe kile alichokisema Mullá Ḥusayn kuhusu usiku ule wa kukumbukwa wakati alipomtambua Qá’im mwahidiwa.

13. Tangazo la Báb lilifanyika lini? ______________________________________

14. Báb alikuwa na umri gani wakati wa Tangazo Lake? _________________________

# SEHEMU YA 3

Baada ya Mullá Ḥusayn, watu wengine kumi na saba walimtafuta na kila mmoja wao alimpata Báb, Haja ya moyo wao. Kila mmoja aliongozwa na Mungu kuutambua ukweli wa Ufunuo mpya, baadhi kupitia maono au ndoto, baadhi kupitia sala na wengine kupitia nyakati za taamali. Wote isipokuwa mmoja miongoni mwa roho hizi zilizobarikiwa zilifikia kwenye uwepo wa Báb huko Shíráz. Yule ambaye hakukutana Naye alikuwa ni mshairi wa kike, mahiri na aliyejaliwa aliyeitwa Ṭáhirih. Yeye alimjua Báb kupitia ndoto, alimtambua kama Qa'im Mwahidiwa na akawa mwendelezaji hodari wa Hoja Yake. Mtu wa kumi na nane aliyejiunga na safu ya wafuasi Wake, alikuwa kijana mwenye umri wa miaka ishirini na miwili aliyejulikana kama Quddús. Ingawa alikuwa kijana, Quddús alikuwa na tabia nzuri ya kuigwa, ambazo ni wachache ambao wangeweza kulinganishwa naye kwa ujasiri na Imani yake. Waumini hawa wa kwanza, pamoja na Mullá Ḥusayn, Báb aliwaita "Herufi kumi na nane za Walio Hai".

Punde baada ya idadi ya Herufi za Walio Hai kukamilika, Báb alimuita Mullá Ḥusayn kuja mbele Yake na kumpa maagizo yafuatayo: "Siku zetu za kuwa pamoja zinakaribia mwisho wake. Agano Langu na wewe sasa limetimizwa. Jifunge kibwebwe cha jitihada, na inuka kueneza Hoja Yangu. Usifadhaike kwa kuona uharibifu na upotofu wa kizazi hiki, kwa kuwa Bwana wa Agano kwa hakika atakusaidia. Kwa kweli, atakuzingira kwa ulinzi Wake wa upendo, na atakuongoza kutoka ushindi hadi ushindi. Kama vile wingu linavyonyesha baraka zake juu ya ardhi, kupita juu ya nchi hii kutoka upeo hadi upeo, na kumimina juu ya watu wake baraka ambazo Mwenyezi, kwa rehema Yake, ameridhia kujalia juu yako. . . . Katika hija hii ambayo tutaianza hivi punde, tumemchagua Quddús kama mwenzi Wetu. Tumekuacha wewe nyuma ili ukabiliane na mashambulizi ya adui mkali na asiyechoka. Walakini, uwe na hakika kwamba, fadhili tukufu isiyosemeka itajaliwa juu yako. Fuata njia ya safari yako kuelekea kaskazini, na njiani mwako tembelea miji ya Iṣfáhán, Káshán, Qum na Ṭihrán. Msihi Mwenyezi Mjalia ili akuwezeshe kwa neema kufikia, katika mji huo mkuu, kiti cha enzi ya kweli, na kuingia katika jumba la yule Mpendwa. Siri imefichwa ndani ya mji huo. Itakapodhihirishwa, itaigeuza dunia hii kuwa paradiso. Tumaini Langu ni kwamba utaweza kushiriki katika neema yake na kuutambua utukufu wake." [6]

Baada ya kumpa Mullá Ḥusayn maagizo ya kwenda Ṭihrán, Báb aliwaita Kwake wale Herufi za Walio Hai wengine na kumpa kila mmoja kazi maalum. Katika maneno Yake ya kuagana nao, aliwasihi kuweka kando kila tamaa ya kidunia na kutawanyika kwa marefu na mapana kutangaza Hoja Yake. Yeye aliwaambia maneno haya:

> **"Enyi rafiki zangu wapendwa! Ninyi ni wachukuzi wa jina la Mungu katika Siku hii. Mmechaguliwa kama ghala za siri Yake. Inampasa kila mmoja wenu adhihirishe sifa za Mungu, na kuonesha kwa mfano wa matedo na maneno yenu ishara za unyofu Wake, nguvu na utukufu Wake. Viungo vyenyewe vya miili yenu lazima vishuhudie ubora wa kusudi lenu, uadilifu wa maisha yenu, uhalisia wa imani yenu, na tabia iliyotukuka ya ibada yenu. Kwani kwa kweli Mimi nasema, hii ni Siku iliyozungumziwa na Mungu katika Kitabu Chake: 'Siku hiyo ndipo Tutawafunga midomo yao; walakini mikono yao itazungumza Nasi, na miguu yao itashuhudia kile ambacho watakuwa wamekitenda.' Tafakarini juu ya maneno ya Yesu aliyowaambia wanafunzi Wake, alipokuwa anawatuma kwenda kueneza Hoja ya Mungu. Kwa maneno kama haya, Yeye aliwaambia kuinuka na kutimiza kazi yao: 'Ninyi ni kama moto ambao katika giza la usiku umewashwa juu ya kilele cha mlima. Acha mwangaza wenu ung'ae mbele ya macho ya watu. Hivyo**

**ndivyo unavyopaswa kuwa usafi wa tabia yenu na kiwango cha kujikana kwenu ili watu wa dunia kupitia kwenu waweze kutambua na kusogezwa karibu zaidi na Baba wa mbinguni ambaye ni Chanzo cha utakaso na neema. Kwa kuwa hakuna aliyemuona Baba aliye mbinguni. Ninyi ambao ni watoto Wake wa kiroho, kupitia matendo yenu lazima muoneshe mfano wa njema Zake, na mshuhudie utukufu Wake. Ninyi ni chumvi ya dunia, lakini kama chumvi imepoteza ladha yake, ni wapi itafaa? Hicho ndicho sharti kiwe kiwango cha kujitenga kwenu, ili katika mji wowote mtakaoingia kwa ajili ya kutangaza na kufundisha Hoja ya Mungu, kwa vyovyote msitarajie kupata nyama au zawadi kutoka kwa watu wake. La, mtakapoondoka kutoka mji huo, kung'uteni vumbi miguuni mwenu. Kama mlivyoingia mkiwa wasafi na bila najisi, ndivyo mnavyopaswa kuondoka kutoka mji huo. Kwani kwa kweli nasema, Baba wa mbinguni yu nanyi na anaendelea kuwalinda daima. Mkiwa waaminifu Kwake, Yeye kwa hakika atawakabidhi mikononi mwenu hazina zote za duniani, na atawainua juu ya watawala na wafalme wa ulimwengu.' Enyi Herufi Zangu! Kwa kweli nasema, imetukuka mno Siku hii kuliko siku za Mitume wa kale. La, tofauti yenyewe haipimiki! Ninyi ni mashahidi wa Mapambazuko ya Siku iliyoahidiwa ya Mungu. Ninyi ni washiriki wa kalisi isiyoelezeka ya Ufunuo Wake. Fungeni vibwebwe vya jitihada, na zingatieni maneno ya Mungu kama yalivyofunuliwa katika Kitabu Chake: 'Tazama, Bwana Mungu wenu amekuja, na pamoja Naye kuna umati wa malaika Wake wakiwa wamejipanga mbele Yake!' Safisheni mioyo yenu dhidi ya tamaa za kidunia, na acheni sifa za kimalaika ziwe pambo lenu. Jitahidini ili kwa matendo yenu muweze kuwa mashahidi kwa ukweli wa maneno haya ya Mungu, na mtambue kwamba kwa 'kurudi nyuma', Yeye ataweza 'kuwaleta watu wengine badala yenu,' ambao 'hawatakuwa mfano wenu,' na ambao watachukua kutoka kwenu Ufalme wa Mungu. Siku ambapo ibada ya kipuuzi ilikuwa inaonekana kuwa inatosha, sasa zimekwisha. Muda umefika ambapo hakuna chochote ila nia safi kabisa, ikisaidiwa na matendo ya usafi usio na mawaa, inaweza kupanda hadi kwenye kiti cha enzi cha Yule Aliye Juu kabisa na kukubalika Kwake. 'Neno jema hupaa Kwake, na kitendo adilifu kitalifanya kutukuzwa mbele Yake.' Ninyi ni dhalili, ambao Mungu amewazungumzia katika Kitabu Chake: 'Nasi tunatamani kuwaonesha fadhili wale ambao walidhalilishwa duniani, na kuwafanya kuwa viongozi wa kiroho miongoni mwa watu, na kuwafanya warithi Wetu.' Ninyi mmeitwa kwenye daraja hili; ninyi mtalifikia, ikiwa tu mtainuka kukanyaga chini ya miguu yenu kila tamaa ya kidunia, na kujitahidi kuwa wale 'watumishi Wake wenye kuheshimiwa ambao hawazungumzi mpaka Yeye amezungumza kwanza, na wanaotii amri Yake.' Ninyi ni Herufi za kwanza zilizotokana na Nukta ya Awali, Chemchemi za kwanza zilizobubujika kutoka Chanzo cha Ufunuo huu. Msihini Bwana Mungu wenu ajalie kwamba isiwepo misukosuko ya kidunia, wala huba za kiulimwengu, wala shughuli za mpito, zitakazoweza kutia doa utakaso, au kuutia uchungu utamu, wa ile neema itiririkayo kupitia kwenu. Mimi nawaandaa kwa ajili ya ujio wa Siku yenye nguvu. Fanyeni jitihada zenu za juu kabisa, ili, katika ulimwengu ujao, Mimi, ambaye sasa nawapa maagizo haya, niweze, mbele ya kiti cha rehema cha Mungu, kufurahia matendo na utukufu wenu katika mafanikio yenu. Siri ya Siku ambayo inatarajiwa kuja sasa imefichwa. Haiwezi kufichuliwa wala kukadiriwa. Mtoto atakayezaliwa Siku hiyo atawapita watu wenye hekima na wanaoheshimika kabisa wa wakati huu, na watu dhalili kabisa na ambao hawana elimu kabisa wa wakati huo watawapita katika uelewa makasisi wenye elimu sana na hodari wa zama hizi. Tawanyeni kwa marefu na mapana katika nchi hii, na,**

**kwa miguu thabiti na mioyo iliyotakasika, andaeni njia ya ujio Wake. Msiangalie unyonge na udhaifu wenu; kazieni macho yenu juu ya nguvu isiyoshindika ya Bwana, Mungu wenu, Mwenyezi. Je, Asingemfanya Abraham siku zilizopita, licha ya kuonekana asiyejiweza, kuyashinda majeshi ya Nimrodi? Je, Hakumwezesha Musa, ambaye fimbo Yake ndiyo ilikuwa mwenzi Wake pekee, kumtiisha Farao na majeshi yake? Je, Hakumfanya Yesu, ambaye alikuwa masikini na dhalili kama Alivyoonekana mbele ya macho ya watu, dhidi ya muungano wa majeshi ya Wayahudi? Je, Hakuyafanya makabila ya kishenzi na yenye shari ya Uarabuni yakubali elimu takatifu na ibadilishayo ya Muḥammad, Mtume Wake? Inukeni kwa jina Lake, wekeni matumaini yenu yote Kwake, na muwe na hakika juu ya ushindi wa mwisho."[7]**

1. Ni jina gani Báb aliwapa waumini wa kwanza ambao walimtambua Yeye kama Qá'im mwahidiwa? ____________________________________________

____________________________________________

2. Je, Herufi za Walio Hai walikuwa wangapi? ______________________

____________________________________________

3. Nani alikuwa wa kwanza kumtambua Báb?______________________

____________________________________________

4. Nani alikuwa Herufi ya mwisho ya Walio Hai?____________________

____________________________________________

5. Jinsi gani Herufi za Walio Hai waliongozwa kuutambua ukweli wa Ufunuo wa Báb?

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

6. Ni yupi miongoni mwa Herufi za Walio Hai hakuweza kufika mbele ya uwepo wa Báb?

____________________________________________

____________________________________________

7. Punde baada ya idadi ya Herufi za Walio Hai kukamilika, Báb alimwita Mullá Ḥusayn kuja mbele yake na akampa maagizo yafuatayo: "Siku zetu za ______________ zinakaribia __________ wake. ___________ Langu na nawe sasa _____________ . _____________ kibwebwe cha ___________ , na __________ kueneza __________ Yangu. ________________ kwa __________________________ na ____________ wa ____________ hiki, kwa kuwa _____________ wa ________________________ ________________________ . Kwa kweli, _________________ kwa _________ Wake wa upendo, na atakuongoza kutoka ______________ hadi ______________ .

Kama vile ______________ linavyonyesha baraka zake juu ya ardhi, _____________ juu ya nchi hii kutoka upeo hadi upeo, na _________________ juu ya watu wake ________________ ambazo _______________ , kwa rehema Yake, ameridhia kujalia juu yako."

8. Báb alimchagua nani wa kuambatana Naye kwenda hija?______________________

_______________________________________________________________________

9. Ni wapi Yeye alimuagiza Mullá Ḥusayn aende? ______________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

10. Ni matumaini gani alimpa Mullá Ḥusayn?___________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

11. Pengine mgependa kukariri angalau sehemu ya hotuba ya Báb kwa Herufi za Walio Hai.

## SEHEMU YA 4

Mnamo Oktoba 1844 Báb, akiambatana na Quddús, alianza safari ya hija Yake kwenda Makka na Madina. Miji hii miwili, iliyoko nchini Saudi Arabia, inachukuliwa kuwa mitakatifu na wafuasi wa Kiislamu. Báb na mwenzi Wake waliingia chomboni hapo Búshihr, ambacho kiliwapeleka kuzunguka Rasi ya Uarabuni, na kuwasili karibu na Makka baada ya takriban miezi miwili. Wakiwa huko Makka, Báb aliandika barua kwa Sharíf, mkuu wa mji na mlinzi wa kaburi lake takatifu. Katika barua hiyo, Yeye Alieleza kwa wazi Ujumbe Wake na kumsihi Sharíf kuikubali Hoja Yake. Lakini Sharíf, ambaye alikuwa ametingwa na mambo yake binafsi, alishindwa kuujibu Ujumbe mtakatifu. Kisha Bab alisafiri pamoja na Quddús kutoka Makka hadi Madina, ambako mabaki ya kimwili ya Mtume Muḥammad yamezikwa. Baada ya kuutembelea mji huo mtakatifu, walirejea Uajemi kwa mashua. Walifika Búshihr, na Báb alimwagiza Quddús aendelee moja kwa moja hadi Shíráz:

> "Siku zetu za kuwa pamoja zinakaribia mwisho. Saa ya utengano imewadia, utengano ambao hakuna muungano tena utakaofuata isipokuwa katika Ufalme wa Mungu . . . Katika mitaa ya Shíráz, ufidhuli utalundikiwa juu yako, na majeraha makali kabisa yatautesa mwili wako. Utaendelea kuishi baada ya vitendo vya kufedhehesha vya maadui zako, na utafikia uwepo wa Yule ambaye ndiye kusudi pekee la ibada na upendo wetu. Mbele Yake utasahau madhara na fedheha zote ambazo zitakuwa zimekupata. Majeshi ya Asiyeonekana yataharakia mbele kukusaidia, na yatautangazia ulimwengu mzima ushujaa na utukufu wako. Yako itakuwa ni furaha isiyo na kifani ya kugugumiza kikombe cha kifo cha kishahidi kwa ajili Yake. Mimi, pia, nitakanyaga njia ya kujitoa dhabihu, na nitaungana nawe katika milki ya milele."[8]

1. Ni lini Báb alianza hija Yake? ______________________________

______________________________

2. Je, Báb alitembelea miji ipi wakati wa hija Yake?______________________________

______________________________

3. Alimwandikia nani huko Makka? ______________________________

______________________________

4. Kwa nini Madina ni mji mtakatifu kwa Waislamu?______________________________

______________________________

5. Katika nafasi ya hapo chini kwa maneno yako mwenyewe, andika maneno ambayo Báb alimwambia Quddús walipofika Búshihr.

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

6. Ni nani ambaye Báb alimwahidi Quddús kuwa angekutana naye? ______________

______________________________

## SEHEMU YA 5

Huko Shíráz Quddús alianza kufundisha Ujumbe wa Báb kwa bidii kubwa. Lakini punde alikabiliwa na upinzani kutoka kwa makasisi wa Kiislamu na gavana wa jimbo, ambaye aliamuru Quddús pamoja na wenzake wawili wakamatwe. Gavana huyo ambaye alikuwa katili

na muovu, aliamuru waadhibiwe hadharani. Ndevu zao zilichomwa, na pua zao zilitobolewa na kamba ilipitishwa humo, na kisha katika hali hii ya aibu, walivutwa kwa kamba hiyo na kutembezwa mitaani. “Litakuwa funzo kubwa kwa watu wa Shíráz,” hiyo ilikuwa amri ya gavana, “ambao watajua ipi itakuwa adhabu ya uasi wa kidini.”[9] Baada ya kupitia fedheha kama hii, Quddús na wenzi wake walifukuzwa kutoka katika mji huo, huku wakionywa kwamba wangeuawa kama wangejaribu kurejea. Hivyo ndivyo roho hizi shujaa zilivyojipatia heshima ya kuwa wa kwanza kuteswa huko Uajemi kwa ajili ya Imani yao mpya. ‘Abdu’l-Bahá amewazungumzia maelfu ambao baadaye waliteswa katika njia ya Mpendwa wao, Báb, kwa maneno haya:

> **“. . . walipata shida za kuhuzunisha na mateso makali kabisa. Walistahimili majaribu kwa uwezo wa ajabu na kwa ushujaa mkuu. Maelfu walitupwa gerezani, kuadhibiwa, kuteswa na kuuawa kishahidi. Makazi yao yalitekwa na kuharibiwa, mali zao zilitaifishwa. Waliyatoa dhabihu maisha yao kwa hiari na kubakia bila kutetereka katika imani yao hadi mwisho kabisa. Roho hizo za ajabu ni taa za Mungu, Nyota za utakatifu zing’aazo kwa utukufu kutoka upeo wa milele wa mapenzi ya Mungu.”[10]**

Baada ya kuamuru adhabu ya kidhalimu kama hiyo kutolewa kwa Quddús na wenzi wake, gavana huyo aligeuzia hasira zake kumuelekea Báb. Aliwatuma askari wake wa farasi kwenda hadi Búshihr kwa maagizo ya kumkamata na kumleta Shíráz akiwa amefungwa minyororo. Wakati huo huo, Báb alikuwa amekwishaondoka Búshihr kwa farasi kuelekea Shíráz. Kikundi hiki cha walinzi wapanda farasi kilikutana Naye katika pori lililokuwa kati ya miji hii miwili. Baadaye kabisa, kiongozi wa kikundi hicho alisimulia hadithi ya kukutana kwao:

> “Tulipomkaribia, alitusalimu na akatuuliza tulikuwa tunaenda wapi. Nilifikiri ni bora kabisa kumficha ukweli, na nilijibu kwamba katika ujirani huu tumeamriwa na gavana kufanya uchunguzi fulani. Yeye alisema huku akitabasamu: ‘Gavana amewatuma kunikamata Mimi. Nipo hapa; nitendeeni kama mtakavyo. Kwa kuja kukutana nanyi, nimeifupisha safari yenu, na kufanya iwe rahisi kunipata Mimi.’ Nilishtushwa kwa maneno yake na kushangazwa kwa unyofu na uwazi wake. Hata hivyo, sikuweza kuelezea utayari wake wa kujisalimisha mwenyewe, kwa hiari yake mwenyewe kwenye adhabu kali za maafisa wa serikali, na hivyo kuhatarisha maisha na usalama wake. Nilijaribu kumpuuza, na nilikuwa najiandaa kuondoka, ndipo aliponisogelea na kusema: ‘Naapa kwa haki ya Yule ambaye alimuumba mwanadamu, akamtofautisha kutoka miongoni mwa viumbe Vyake vingine, na kuufanya moyo wake kuwa kiti cha mamlaka na ujuzi Wake, kwamba maisha Yangu yote sijawahi kutamka neno lolote isipokuwa ukweli, na sikutamani kingine isipokuwa ustawi na maendeleo ya wanadamu Wenzangu. Nimepuuzia raha Zangu mwenyewe na nimeepuka kuwa chanzo cha maumivu au huzuni kwa mtu yeyote. Nafahamu kwamba mnanitafuta Mimi. Napendelea kujisalimisha Mwenyewe mikononi mwenu, kuliko kukupa wewe na wenzi wako usumbufu usio wa lazima kwa ajili Yangu.’ Maneno haya yalinigusa sana. Bila kufikiri nilishuka kutoka kwenye farasi wangu, na, nikibusu vikuku vyake, nikamwambia maneno haya: ‘Ewe mwanga wa macho ya Mtume wa Mungu! Nakusihi, kwa Yule ambaye amekuumba na kukujalia ukuu na uwezo kama huo, ukubali ombi langu na ujibu sala yangu. Nakusihi utoroke kutoka mahali hapa na ukimbia kutoka kwa gavana huyu katili na duni wa jimbo hili. Naogopa njama zake dhidi yako; nakataa wazo la kufanywa chombo cha mipango yake miovu dhidi ya uzao bora na usio na hatia wa Mtume wa Mungu . . . ’ Kwa maombi yangu ya dhati yeye alitoa jibu hili: ‘Acha

Bwana Mungu wako akulipe kwa ukarimu na dhamira yako njema. Hakuna ajuaye fumbo la Hoja Yangu, hakuna awezaye kuelewa siri zake. Kamwe sitaweza kugeuzia mbali uso Wangu kutoka amri ya Mungu. Yeye peke ndiye Ngome Yangu ya uhakika, Mhimili Wangu, Kimbilio Langu. Hadi saa Yangu ya mwisho itakapowadia, hakuna awezaye kunishambulia Mimi, hakuna awezaye kuvuruga mipango ya Mwenyezi. Na saa Yangu itakapowadia, furaha yangu itakuwa kubwa jinsi gani kugugumiza kikombe cha kifo cha kishahidi kwa jina Lake! Nipo hapa; nifikishe katika mikono ya bwana wako. Usiogope, kwani hakuna atakayekulaumu.' Nilikubali na kutekeleza haja yake."[11]

Papo hapo Báb aliendelea na safari Yake kuelekea Shíráz. Akiwa huru bila minyororo, Yeye alitangulia huku walinzi Wake wakimfuata kwa heshima. Alipowasili Shíráz, Báb aliletwa mbele ya gavana, ambaye alimtendea ukatili wa kuaibisha. Alimkemea na kumpinga Báb hadharani. Kisha alimuacha chini ya uangalizi wa mjomba Wake. Ingawa Báb aliruhusiwa kurudi nyumbani Kwake, uhuru Wake uliwekewa mipaka. Watu wa familia Yake na wengine wachache tu waliruhusiwa kumuona. Licha ya majaribio ya yule gavana na makasisi kukomesha ushawishi Wake, bado idadi ya wafuasi Wake iliongezeka kwa haraka.

Habari za Tangazo muhimu la Báb zikawa zimeenea sana kiasi kwamba mfalme wa Uajemi aliamua kumtuma mmoja wa wanazuoni wake mwenye ujuzi na aliyeaminika kwenda Shíráz kuchunguza hali. Akiwa kama mgeni nyumbani kwa gavana mwenyewe, msomi huyu alikutana na Báb mara tatu. Alidhamiria kukanusha madai ya Báb, lakini katika kila mkutano aliendelea kuvutiwa zaidi kwa ujuzi, ufasaha na hekima Yake. Hadi kufikia mkutano wa tatu, Vaḥíd—jina ambalo kwalo mwanazuoni huyu baadaye alikuja kujulikana—alikuwa ameshawishika kabisa juu ya Daraja Takatifu la Kijana huyo. Vaḥíd baadaye alieleza kuwa, wakati wa kukutana na Báb, yeye alijihisi "dhalili kama vumbi chini ya miguu Yake". Yeye mara moja alituma taarifa kwa maandishi kwa baraza la mfalme na aliondoka Shíráz kwa maagizo ya Báb. Tangu siku hiyo na kuendelea, yeye aliziweka wakfu nguvu zake kwa ajili ya uendelezaji wa Hoja Yake na hatimaye aliyatoa maisha yake dhabihu katika njia ya Mpendwa wake.

Kutokana na kuongezeka kwa upendo na umashuhuri wa Báb, hasira ya gavana iliongezeka. Yeye kwa mara nyingine tena aliamuru kukamatwa Kwake. Wakati huu gavana alikusudia kumuua Báb, na alimtuma askari polisi mmoja kwenda kumkamata nyumbani kwa mjomba Wake usiku wa manane. Usiku ule ule, hata hivyo, janga la tauni lilitokea katika mji wa Shíráz na mji mzima ukawa katika hali ya taharuki. Ndani ya saa chache, zaidi ya watu mia moja walikuwa wamefa kutokana na ugonjwa huu wa kutisha. Kelele za maumivu na huzuni ziliweza kusikika mitaani, na wakazi wa mji huo walikuwa wakiukimbia kwa kiwewe. Bila kuwa na uhakika wa nini cha kufanya, afisa huyo alimpeleka Báb nyumbani kwake mwenyewe. Alipofika nyumbani na kumkuta mwanaye akiwa mahututi kutokana na ugonjwa huo alifadhaika sana. Alihamaki kwa mshtuko mkubwa, akajitupa miguuni kwa Báb na kumuomba msamaha. Wakati mtoto wake alipoponywa kimuujiza, yule afisa aliutambua Mkono wa Mungu katika kuzuka kwa tauni hiyo na akamsihi gavana amuachilie Báb. Gavana, akihofia maisha ya familia yake na wengine, alimwachilia Báb, kwa sharti kwamba Báb aondoke Shíráz.

Wakati wa kipupwe cha 1846 Báb aliondoka kuelekea Iṣfáhán, mji uliopo kaskazini mwa Shíráz. Wakati akimuaga mjomba Wake, Alimwambia: "Nitakutana nawe tena katikati ya milima ya Ádhirbáyján, ambapo kutokea hapo nitakutuma kwenda kupata taji la kifo cha kishahidi. Mimi mwenyewe nitakufuata pamoja na mmoja wa wanafunzi wangu waaminifu, na tutaungana nawe katika milki ya milele."[12]

1. Quddús alifanya nini alipowasili huko Shíráz? ____________________

____________________________________________

2. Nani alimpinga Quddús alipoanza kufundisha Ujumbe wa Báb huko Shíráz? ______

____________________________________________

3. Neno “kasisi” lina maana gani? ____________________

____________________________________________

4. Ni maneno gani huelezea tabia ya gavana wa Shíráz? ____________________

____________________________________________

5. Gavana aliamuru adhabu gani kwa Quddús na wenzi wake wawili? ______________

____________________________________________

____________________________________________

6. Neno hili “uasi wa kidini” lina maana gani? ____________________

____________________________________________

7. Baada ya kumfukuza Quddús na wenzi wake wawili kutoka Shíráz, gavana aliwaagiza walinzi wake wafanye nini? ____________________

____________________________________________

8. Báb alikuwa anafanya nini pale walinzi walipokutana Naye? ____________________

____________________________________________

9. Báb alimwambia kiongozi wa askari waliotumwa kumkamata Yeye, “____________ ______________________________ Mimi. _____________ hapa; ________________ kama _________________ . Kwa kuja _____________ nanyi, _______________ __________ yenu, na kufanya iwe ___________ kunipata Mimi.” Kiongozi alijaribu kumpuuza Báb na alikuwa anajiandaa kuondoka, ndipo Báb aliposema: “. . . ___________________ Zangu mwenyewe na ______________ kuwa _________ cha ______________ au _____________ kwa mtu yeyote. __________________ kwamba ___________________ Mimi. Napendelea ____________________________ __________________ mwenu, kuliko _______________ wewe na _______________ wako ___________________________________ kwa ajili Yangu.”

10. Jinsi gani Báb alivunja uadui wa walinzi Wake? ____________________

____________________________________________

11. Ni kwa namna gani Báb alifika Shíráz?

12. Gavana alichukua hatua gani dhidi ya Báb?

13. Majaribio ya gavana na makasisi kukomesha ushawishi Wake yalikuwa na matokeo gani miezi michache baadaye?

14. Vaḥíd ni nani?

15. Gavana alifanya nini alipoona umashuhuri wa Báb unazidi kuongezeka?

16. Nini kilimfanya gavana hatimaye amuachilie Báb na kumruhusu kuondoka Shíráz?

17. Báb alikwenda wapi alipoondoka Shíráz?

18. Lini alianza safari hii?

19. Báb alimwambia nini mjomba Wake alipokuwa akimuaga?

20. Unda jozi pamoja na mshiriki mwingine wa kikundi chako na kwa zamu wewe na mwezako simulieni hadithi ya wakati wa kukutana kwa maaskari wapanda farasi na Báb katika pori lililokuwa kati ya Búshihr na Shíráz.

## SEHEMU YA 6

Wakati Báb alipokuwa akiukaribia mji wa Iṣfáhán, alimuandikia barua gavana wa jimbo hilo akimuomba kupanga mahali ambapo Yeye angeishi. Gavana huyu, ambaye alikuwa mwenye roho nzuri na mwenye haki, aliguswa mno na adabu na mtindo wa barua ya Báb kiasi kwamba alimuagiza afisa mkuu kabisa wa kidini wa jimbo hilo kumpokea Báb nyumbani kwake na kumpa mapokezi yenye upendo na ukarimu.

Katika kipindi cha kukaa kwa Báb huko Iṣfáhán, makundi ya watu yalikuja kumuona kila siku na kusikiliza maneno Yake. Umaarufu Wake uliokuwa ukiongezeka, hata hivyo, punde uliamsha wivu wa makasisi wa mji huo, ambao waliogopa kupoteza nafasi za kazi na mamlaka waliyokuwa nayo kwa muda mrefu. Walianza kueneza uvumi kumhusu Báb, wakitumaini kuamsha tuhuma dhidi yake. Jambo hili liliposhindwa, walipanga njama za kumuua. Yule gavana, alipotambua njama za makasisi hao, akamkaribisha Báb akae nyumbani kwake. Hapo, wakati wa mazungumzo na Báb, yule gavana pole pole alikuja kuutambua ukuu wa Ufunuo Wake. Siku moja, alipokuwa ameketi na Báb bustanini nyumbani kwake, yule gavana alimwambia maneno haya:

> "Mpaji Mwenyezi amenijalia mali nyingi. Mimi sijui namna bora ya kutumia mali hizi. Sasa kwa kuwa, kwa msaada wa Mungu, nimeongozwa kuutambua Ufunuo huu, ni shauku yangu ya dhati kutoa wakfu mali zangu zote kwa ajili ya kuendeleza maslahi na kueneza umaarufu wake. Ni dhamira yangu kwenda Ṭihrán, kwa idhini Yako, na kufanya kila niwezalo kumvutia mfalme kwenye Hoja hii, ambaye imani yake kwangu ni thabiti na isiyoyumba."[13]

Kwa mmiminiko huu wa upendo na kujitoa, Báb alijibu:

> "Mungu akulipe kwa dhamira yako bora. Kusudi bora kama hilo kwangu Mimi lina thamani zaidi kuliko kitendo chenyewe. Siku zako na Zangu zinahesabika, hata hivyo ni fupi mno kuniwezesha Mimi kushuhudia, na kukuruhusu kufikia na kufanikisha matumaini yako. Siyo kwa njia ambazo wewe unapenda kuzifikiria, Mjalia Mwenyezi atatimiza ushindi wa Imani Yake. Kwa kupitia watu masikini na dhalili wa nchi hii, kwa damu ambayo hawa watakuwa wameimwaga katika njia Yake, Mwenyezi Mwenye mamlaka atahakikisha hifadhi na kuimarisha msingi wa Hoja Yake. Mungu huyo huyo, katika ulimwengu ujao, Ataweka juu ya kichwa chako taji la utukufu wa milele, na kukumiminia baraka Zake zisizokadirika. Kuhusu muda wako wa maisha ya duniani, imebaki miezi mitatu na siku tisa, baada ya hapo, kwa imani na yakini, utaharakia kwenye makao yako ya milele."[14]

Miezi mitatu na siku tisa baadye, yule gavana wa Isfahan alifariki, sawa kabisa kama Báb alivyotabiri. Siku chache baada ya kifo chake, mrithi wake alituma ujumbe kwa mfalme huko Ṭihrán akimuuliza amfanyeje Báb. Mfalme aliamuru kwamba Báb apelekwe kwa kificho hadi mji huo mkuu, ambapo mfalme huyo alikusudia kukutana Naye. Hivyo, akiambatana na kikundi cha askari wapanda farasi, Báb alianza safari Yake kuelekea Ṭihrán.

1. Báb alimuandikia nani barua alipokuwa anakaribia mji wa Iṣfáhán? _____________

_____________________________________________________________

2. Ni maneno gani huelezea tabia za gavana wa Iṣfáhán? ________________________

_____________________________________________________________________

3. Gavana alimpa maagizo gani afisa mkuu kabisa wa kidini wa jimbo hilo?_________

_____________________________________________________________________

4. Kitu gani kiliwafanya makasisi wa Iṣfáhán wawe na wivu? _____________________

_____________________________________________________________________

5. Je, makasisi waliogopa kupoteza nini kama Báb angeruhusiwa kuendelea kutangaza Ujumbe Wake? _______________________________________________________

_____________________________________________________________________

6. Je, yule gavana wa Isfahan alifanya nini kumlinda Báb dhidi ya njama za makasisi?

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

7. Gavana alitaka kufanya nini kwa ajili Hoja ya Báb? ___________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

8. Báb alijibuje ombi la gavana? ____________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

9. Báb alieleza ukweli gani wa kina kuhusu maendeleo ya Hoja ya Mungu katika kumjibu gavana?________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

10. Mfalme alimpa amri gani mrithi wa gavana?_________________________________

_____________________________________________________________________

_____________________________________________________________________

# SEHEMU YA 7

Waziri mkuu wa Uajemi wa wakati huo alikuwa mtu mwenye ubinafsi na asiyejimudu. Alihofia kwamba, kama Báb angekuja Ṭihrán na kukutana na mfalme, angepoteza cheo na madaraka yake. Kwa hiyo, alimshawishi mfalme abadilishe maagizo yake na kumpeleka Báb kwenye jimbo la Á<u>dh</u>irbáyján kaskazini magharibi wa nchi hiyo.

Akiwasili chini ya ulinzi huko Tabríz, mji mkuu wa jimbo hilo, mnamo Juni 1847, Báb alipelekwa kwenye nyumba iliyokuwa imechaguliwa kama mahali Pake pa kifungo. Kikosi maalum cha askari kililinda mlango wa nyumba hiyo. Hakuna aliyeruhusiwa kuonana Naye, isipokuwa wafuasi Wake wawili. Watu wa mji huo walionywa kwamba yeyote ambaye angejaribu kuonana na Báb, angekamatwa na kufungwa gerezani, na mali zake zote zingetaifishwa.

Báb aliishi huko Tabríz kwa muda mfupi na kisha alihamishiwa kwenye ngome ya Máh-Kú, ambayo ilikuwa katika milima ya Á<u>dh</u>irbáyján mbali kabisa na miji mikubwa na midogo. Waziri mkuu alifikiria kuwa, kwa kumhamishia Báb katika kona hiyo ya mbali na isiyokalika ya nchi, ushawishi Wake ungepungua, na Imani Yake pole pole ingesahaulika. Lakini hakutambua kwamba pindi taa ya dini ya Mungu ikishawashwa, hakuna mkono wa mwanadamu uwezao kuzima mwale wake. Kupitia utukufu na wema Wake wa upendo, punde Báb alipata heshima na mvuto kwa wote wawili, ofisa mhusika wa ngome na watu wa eneo hilo.

Hivyo, vizuizi vikali alivyowekewa Báb pole pole vililegezwa na milango ya ngome ilifunguliwa kwa ajili ya wafuasi Wake, ambao walifika kwa wingi kutoka sehemu mbalimbali za Uajemi kuja kumuona. Katika kipindi cha kifungo Chake huko Máh-Kú, Báb alifunua Bayán ya Kiajemi, Kitabu muhimu kabisa miongoni mwa vitabu Vyake. Katika Kitabu hicho, Yeye alianzisha sheria za Kipindi Chake Kitakatifu, alitangaza kwa uwazi na mara moja ujio wa Ufunuo mwingine mkuu zaidi kuliko Wake Mwenyewe, na aliwahimiza wafuasi Wake kumtafuta na kumtambua "Yule Ambaye Mungu angemdhihirisha". Mmoja wa waumini Wake wa kwanza ambaye aliishi huko Máh-Kú wakati huo, aliuelezea ufunuo wa Bayán ya Kiajemi kwa maneno haya:

> "Sauti ya Báb, wakati akisoma mafundisho na kanuni za Imani Yake, iliweza kusikika wazi wazi na wale ambao walikuwa wakiishi chini ya mlima. Lahani za kughani Kwake, mtiririko wa mapigo ya aya ambazo zilimiminika kutoka midomoni Mwake, zilivutia masikio yetu na kupenya ndani kabisa ya roho zetu. Mlima na bonde vilirudisha mwangwi wa utukufu wa sauti Yake. Vina vya mioyo yetu vilitetema kwa kwa mvuto wa matamshi Yake."[15]

Waziri mkuu alipojua kwamba Báb alikuwa amejipatia upendo na uungwaji mkono wa watu wa Máh-Kú na kwamba Imani Yake ilikuwa ikiendelea kuenea kote nchini, alitoa amri kwamba Báb ahamishiwe katika ngome ya <u>Ch</u>ihríq. Walakini, huko pia, watu wa miji ya jirani na maafisa wa ngome hiyo walivutiwa na haiba yenye nguvu ya Báb. Hata baadhi ya makasisi mashuhuri kabisa wa eneo hilo waliikubali Imani mpya na waliacha vyeo vyao vya heshima ili kuungana na safu za wafuasi Wake.

Mara tu waziri mkuu aliposikia matukio yaliyotokea huko <u>Ch</u>ihríq, alitoa amri mara moja Báb ahamishiwe Tabríz. Mkutano wa mamlaka za kidini uliitishwa ili kumchunguza Báb na kupata njia ifaayo kabisa kukomesha ushawishi Wake. Wakati huu karibu na Julai 1848.

Katika mkutano huo makasisi na maafisa wa serikali walijaribu kumdhalilisha Báb, lakini walishindwa na utukufu Wake. Alipoulizwa, “Wewe unadai kuwa ni nani, na umeleta ujumbe gani?” Yeye alitangaza:

> **“Mimi ndiye, Mimi ndiye, Mimi ndiye, Yule Mwahidiwa! Mimi ndiye Yule Ambaye jina Lake kwa miaka elfu moja mmeliita, Ambaye kwa kutajwa Kwake mmeinuka, Ambaye ujio Wake mmetamani sana kuushuhudia, na Ambaye saa ya Ufunuo Wake mmemuomba Mungu kuiharakisha. Kwa kweli Nasema, imewapasa watu wa Mashariki na Magharibi kutii neno Langu na kuahidi utiifu kwa utu Wangu.”**[16]

Siku chache baada ya mkutano ule, Báb alirudishwa Chihríq. Maadui zake walitumaini kwamba huko Tabríz, wangemshurutisha aache Ujumbe Wake. Lakini mwishowe waliamua kwamba, kama Báb angeendelea kuwa hai, isingewezekana kuzuia wimbi la ushawishi Wake uliokuwa unaendelea kuongezeka miongoni mwa watu wa Uajemi.

1. Ni maneno gani huelezea tabia ya waziri mkuu wa Uajemi wa wakati huo?________

   ____________________________________________________________

2. Kwa nini waziri mkuu alihofia kukutana kwa mfalme na Báb?__________________

   ____________________________________________________________

3. Je, waziri mkuu alifanya nini ili kumzuia mfalme asikutane na Báb? _____________

   ____________________________________________________________

4. Kwa nini askari walilinda mlango wa nyumba ambamo Báb alikaa huko Tabríz?

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

5. Watu wa mji huo walipewa onyo gani? ____________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

6. Báb alihamishiwa wapi baada ya kukaa kwa muda mfupi huko Tabríz?___________

   ____________________________________________________________

7. Waziri mkuu alifikiri nini kingetokea kwa Hoja ya Báb kama angefungwa huko Máh-Kú?

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

8. Jinsi gani fikira za waziri mkuu hazikuwa sahihi?____________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

9. Jinsi gani Milango ya gereza la Báb huko Máh-Kú ilikuja kufunguka kwa wafuasi Wake?

10. Ni kitabu gani muhimu ambacho Báb alikifunua katika kipindi cha kufungwa Kwake huko katika ngome ya Máh-Kú?

11. Ni zipi baadhi ya dhima za Bayán ya Kiajemi?

12. Katika Bayán, Báb aliwahimiza wafuasi Wake wamtafute na kumpata nani?

13. Je, waziri mkuu alifanya nini aliposikia kwamba Imani ya Báb ilikuwa inaendelea kuenea?

14. Jinsi gani Hoja ya Báb iliathiriwa kwa kuhamishiwa Kwake huko Chihríq?

15. Je, maadui wa Báb walifikiria wangetimiza kitu gani kwa kumhamisha Báb kutoka Chihríq kwenda Tabríz?

16. Ni maswali gani watu wenye mamlaka walimuuliza Báb wakati wa kuhojiwa Kwake?

17. Je, Báb ilitangaza nini katika kuyajibu maswali yao?

## SEHEMU YA 8

Akimzungumzia Báb, 'Abdu'l-Bahá husema:

**"Na kuhusiana na Báb—roho yangu iwe dhabihu Yake!—ilikuwa katika umri wa ujana, yaani pale Yeye alipofikia umri wa miaka ishirini na mitano wa maisha Yake yaliyobarikiwa, ndipo Alipoinuka kutangaza Hoja Yake. . . . Pekee, katika namna ambayo haiwezi kufikirika, Yeye aliifanya kazi ambayo ni nadra kuifikiria. Kwa kuwa Waajemi wanafahamika kote ulimwenguni kwa misimamo yao mikali ya kidini. Kiumbe huyu mwangavu aliinuka kwa ule uwezo kiasi cha kuitikisa misingi ya sheria za kidini, mila na desturi, mienendo, maadili na mazoea ya Uajemi, na alianzisha sheria, imani na dini mpya. Ingawa watu mashuhuri wa nchi, idadi kubwa ya watu na viongozi wa dini wote waliinuka kumwangamiza na kumteketeza, peke, Yeye alikabiliana nao na aliitikisa Uajemi nzima. Jinsi gani maulamaa, viongozi na wakazi wengi wa nchi hiyo, ambao kwa shangwe na furaha waliyatoa dhabihu maisha yao katika njia Yake, na waliharakia kwenye uwanja wa kifo cha kishahidi!**

**"Serikali, taifa, makasisi na viongozi mashuhuri walitamani kuuzima mwanga Wake, lakini hawakuweza kufanya hivyo. Hatimaye mwezi Wake ulichomoza, nyota Yake iling'aa zaidi, msingi Yake ukasimamishwa kwa uthabiti, na upeo Wake ulifurikwa kwa mwangaza. Yeye aliufundisha watu wengi kupitia elimu takatifu na alisababisha matokeo ya ajabu juu ya fikra, maadili, desturi na mienendo ya Waajemi. Yeye alitangaza habari njema za udhihirisho wa Jua la Bahá kwa wafuasi Wake na aliwaandaa kwa imani na yakini.**

**"Udhihirisho wa dalili za ajabu na shughuli zenye nguvu kama hizo; athari zilizoletwa juu ya fikra na akili za watu, uwekaji wa misingi ya maendeleo; na uanzishwaji wa kanuni za lazima za mafanikio na ustawi vilivyofanywa na mfanyabiashara huyu kijana, hufanyiza uthibitisho mkubwa kabisa kwamba Yeye alikuwa Mwelimishaji wa Ulimwengu—ukweli ambao hakuna mtu yeyote mwenye haki daima angesita kuulikubali."[17]**

Unahamasishwa kuandaa na kutoa mazungumzo mafupi juu ya maisha ya Báb kulingana na maneno ya 'Abdu'l-Bahá hapo juu na kutokana na historia uliyokwishaisoma hadi sasa.

## SEHEMU YA 9

Mnamo mwaka 1850, waziri mkuu mpya wa Uajemi, mwenye kiu ya kumwaga damu kama yule aliyetangulia, aliamuru adhabu ya kifo kwa Báb. Tena, Báb aliletwa kutoka Chihríq hadi Tabríz, ambako alifungiwa kwenye chumba kidogo kando ya uwanja, ambao ndio ungekuwa mahali pa kifo Chake cha kishahidi.

Wakati Báb alipokuwa akipelekwa kwenye chumba hicho, kijana mmoja alilazimisha kujipenyeza katikati ya umati wa watu na kujitupa kwenye miguu ya Báb. “Usiniondoe kutoka Kwako, Ee Bwana,” alisihi kijana huyo. Alimuomba Báb amruhusu kumfuata kokote ambako Yeye angekwenda. “Inuka,” Báb alijibu, “na uwe na hakika kwamba utakuwa pamoja Nami. Kesho utashuhudia kile ambacho Mungu amekiamuru.”[18] Yule kijana alikamatwa mara moja pamoja na wenzi wake wawili, na aliwekwa katika chumba kile kile ambamo Báb na mwandishi Wake walifungiwa. Kijana huyu alikuja kujulikana kama Anís.

Anís alikuwa amesikia juu ya Ujumbe mpya kutoka kwa Báb Mwenyewe alipokuwa akikaa kwa muda mfupi huko Tabríz—licha ya vizuizi hivi vikali ambavyo vilikuwa vimewekwa kwa muda baina Yake na wakazi wa mji ule aliokuwa anakutana nao. Moto wa upendo wa Mungu uliwaka kwa nguvu mno ndani ya moyo wa Anís kiasi kwamba shauku yake pekee ilikuwa ni kujitoa dhabihu kwa ajili ya Imani yake mpya. Lakini baba yake wa kambo, akishitushwa kwa tabia ya kijana wake, alimzuia Anís kutembea tembea na alimwekea ulinzi mkali nyumbani kwake. Humo Anís alitumia majuma kadhaa katika sala na tafakari, akimsihi Mungu amruhusu kufika, kwa mara nyingine tena, mbele ya Mpendwa wake. Siku moja, alipokuwa amezama katika sala, alipata maono yasiyo ya kawaida. Yeye alimuona Báb amesimama mbele yake na akimuita. Anís alijitupa miguuni Pake. “Shangilia,” Báb alimwambia, “saa inakaribia, ambapo, katika mji huu huu, nitatundikwa mbele ya macho ya umati wa watu na nitakuwa mhanga kwenye moto wa adui. Sitamchagua yeyote isipokuwa wewe kushiriki Nami kikombe cha kifo cha kishahidi. Uwe na hakika kwamba ahadi hii Ninayokupa itatimizwa.”[19] Na hivyo Anís alianza kungojea kwa subira, akijua kwamba punde siku ingewadia ambapo yeye angeungana tena na Mpendwa wake. Sasa, hatimaye, yeye aliiifikia haja ya moyo wake.

Jioni ile Báb aling’aa kwa furaha. Alizungumza kwa uchangamfu na Anís na wale wafuasi wengine watatu waaminifu waliofungwa pamoja Naye ndani ya kile chumba cha gereza. “Kesho,” Yeye aliwaambia, “itakuwa siku ya kuuawa Kwangu kishahidi. Natamani mmoja wenu hivi sasa angeinuka na, kwa mikono yake mwenyewe, aondoe uhai Wangu. Napendelea zaidi kuuawa kwa mkono wa rafiki kuliko ule wa adui.” Hakuna hata mmoja wao angefikiria kutoa uhai wa thamani kama huo, na walikaa kimya, machozi yakiwatiririka machoni mwao. Kisha ghafla, Anís alisimama na akasema kwamba yeye alikuwa tayari kutii chochote kile ambacho Báb angeamuru. “Kijana huyu huyu ambaye ameinuka kukubaliana na matakwa Yangu,” Báb alitangaza, “atauawa kifo cha kishahidi pamoja Nami. Yeye ndiye nitakayemchagua kushiriki Nami taji lake.”[20]

Mapema asubuhi iliyofuata, tarehe 9 Julai 1850, Báb alikuwa anazungumza na mwandishi Wake ndipo ghafla afisa mmoja alipoingilia mazungumzo yao. “Hadi pale nitakapokuwa nimemaliza yale yote Ninayotaka kumwambia,” Báb alimwambia yule afisa, “ndipo nguvu yoyote ya kidunia itakapoweza kuninyamazisha. Hata kama ulimwengu mzima ungetwaa silaha dhidi Yangu, bado wasingekuwa na uwezo wa kunizuia kutimiza kusudi Langu hadi neno la mwisho.”[21] Lakini yule afisa hakuelewa maana ya maneno ya Báb. Yeye hakujibu lolote na akamuamuru yule mwandishi amfuate. Báb kisha alichukuliwa kutoka chumbani Kwake hadi kwenye makazi ya makasisi watatu wenye vyeo vya juu kabisa wa mji huo, ambao bila kusita, walitia sahihi amri ya kuuawa Kwake.

Baadaye asubuhi ile Báb alipelekwa kwenye uwanja ambako umati wa watu wanaokaribia elfu kumi walikuwa wamekusanyika juu ya mapaa ya nyumba ili kushuhudia mauaji Yake. Alikabidhiwa kwenye mikono ya Sám Khán, kamanda wa kikosi cha wanajeshi kilichoamriwa kumuua. Lakini Sám Khán alitahayari mno, akijikuta ameshikwa na hofu

kwamba kitendo chake kingeleta ghadhabu ya Mungu juu yake. "Ninakiri Imani ya Kikristo," yeye alimueleza Báb, "na sina dhamira yoyote mbaya dhidi Yako. Kama Hoja Yako ni Hoja ya Ukweli, uniwezeshe kuepukana na sharti la kumwaga damu Yako." "Fuata maagizo yako," Báb alijibu, "na kama dhamira yako ni ya kweli, Mwenyezi kwa hakika atakuondolea mfadhaiko wako."[22]

Sám Khán aliwaamuru watu wake kupigilia msumari wa chuma kwenye ukuta na kufunga kamba mbili juu yake. Kwenye kamba hizo, Báb na Anís walining'inizwa. Ndipo kikosi hicho kikajipanga katika safu tatu, kila moja ikiwa na watu mia mbili na hamsini. Moja baada ya nyingine, kila safu ilipiga risasi. Wakati moshi kutoka kwenye zile bunduki mia saba na hamsini ulipotawanyika, umati ule uliokuwa umeduwaa uliona mandhari ambayo ilikuwa vigumu kuamini. Anís alikuwa amesimama mbele yao mzima na bila kudhurika, na Báb alikuwa ametoweka machoni pao. Zile risasi zilikuwa zimekata tu kamba walizokuwa wametundikwa nazo. Msako wa hasira wa kumtafuta Báb ukaanza. Hatimaye alikutwa amekaa ndani ya chumba Chake cha gereza, akiwa anamalizia mazungumzo na mwandishi Wake yaliyokuwa yamekatizwa. "Nimemaliza mazungumzo yangu," Báb alisema. "Sasa mnaweza kuendelea kutimiza azma yenu."[23]

Akiwa amepigwa na butwaa kwa kile kilichotokea, Sám Khán alikataa kuwaruhusu watu wake kumdhuru Báb na aliwaamuru waondoke pale uwanjani. Kikosi kingine kiliitwa mara moja kutekeleza mauaji. Kwa mara nyingine tena Báb na Anís walitundikwa katika uwanja ule, na wanajeshi wakapiga risasi. Safari hii risasi ziliwapata. Miili ya Báb na Anís iliharibika kabisa; lakini nyuso zao takriban hazikuguswa. Wakati kile kikosi kilipokuwa kinajiandaa kupiga risasi, Báb aliuambia ule umati uliokuwa ukikodoa macho maneno haya ya mwisho:

> **"Enyi kizazi kipotofu! Laiti mngeniamini Mimi, kila mmoja wenu angefuata mfano wa kijana huyu, ambaye kwa daraja yu juu zaidi ya wengi wenu, na kwa hiari angejitoa dhabihu katika njia Yangu. Siku itakuja ambapo mtakuwa mmenitambua Mimi; siku hiyo sitakuwa tena nanyi."**[24]

1. Báb aliuawa kishahidi katika mji gani? ______________________________

2. Nani aliamuru kuuawa kwa Báb?______________________________

   ______________________________

3. Kwa maneno yako mwenyewe, simulia jinsi yule kijana, Anís, alivyouawa kishahidi pamoja na Báb.

   ______________________________
   ______________________________
   ______________________________
   ______________________________
   ______________________________
   ______________________________
   ______________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

4. Kwa nini Anís alichaguliwa na Báb kushiriki naye taji la kifo cha kishahidi? ______

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

5. Wakati yule afisa alipomkatisha Báb na mwandishi Wake ile asubuhi ya Mauaji Yake, Báb alimwambia: "Hadi pale nitakapokuwa nimemaliza __________________ ________________ kumwambia, ndipo nguvu __________________________________ ____________________________________________ ."

6. Kamanda wa jeshi wa kile kikosi kilichoamrishwa kutekeleza mauaji ya Báb alikuwa anaitwa nani? ___________________________________________________________

______________________________________________________________________

7. Je, Sám <u>Kh</u>án alimuomba nini Báb? __________________________________________

______________________________________________________________________

8. Je, Báb alimwambia Sám <u>Kh</u>án afanye nini? __________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

9. Ni askari wangapi walimpiga risasi Báb na mwenzi Wake, Anís? ________________

10. Umati ulioduwaa uliona nini pale moshi wa risasi za bunduki ulipokwisha? _______

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

11. Je, Báb alikuwa anafanya nini pale walipompata? ____________________________

____________________________________________________________________

12. Báb alisema nini pale hatimaye walipompata? ______________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

13. Kifo cha kishahidi cha Báb kilitokea tarehe ngapi? ___________________________

____________________________________________________________________

14. Báb alikuwa wa umri gani wakati wa kuuawa Kwake kishahidi? ________________

____________________________________________________________________

15. Katika nafasi ya hapo chini, andika maneno ya mwisho yaliyosemwa na Báb kwa ule umati uliokuwa umekusanyika kushuhudia mauaji Yake.

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

____________________________________________________________________

## SEHEMU YA 10

Inapendekezwa kwamba uchore katika ramani hapo chini njia ya safari na uhamisho wa Báb. Wakati unafanya hivyo, jaribu kukumbuka nini kilitokea kila mahali na taamali juu ya umuhimu wake.




## SEHEMU YA 11

Katika kitengo hiki mmejifunza kuhusu maisha ya mmojawapo wa Wadhihirishaji Pacha wa Mungu kwa Siku hii. Wakati wa utumishi Wake mfupi Báb alianzisha mageuzi ya kiroho huko Uajemi. Maelfu kwa maelfu ya roho safi waliupokea Ujumbe Wake na walianza kujiandaa kwa ajili ya ujio wa Mdhihirishaji wa Mungu Ambaye Báb alimtaja kama "Yule Ambaye Mungu atamdhihirisha". Mnajua kwamba wakati wowote Mdhihirishaji wa Mungu atokeapo duniani, wale wenye kiu ya mamlaka na uongozi huinuka dhidi Yake na kujaribu kuuzima mwanga wa Ufunuo Wake. Kwa jinsi hii, si tu kwamba Báb aliuawa na viongozi wajinga wa Uajemi, bali pia maelfu ya wafuasi Wake waliuawa. Maisha ya kishujaa ya Wabábí hawa wa mwanzoni, ambao waliumwagilia mti wa Ufunuo mchanga kwa damu yao, yatakuwa somo la kujifunza kwenu katika miaka ijayo. Watu maarufu kama vile Mullá Ḥusayn, Quddús, Ṭáhirih na Vahíd watakuwa chanzo cha uvuvio na ujasiri kwenu katika maisha yenu yote kadiri muendeleavyo kujifunza juu ya historia isiyo ya kawaida ya miaka ya mwanzoni ya Zama za

Kibahá'í. Kwa sasa, itakuwa vyema kutafakari juu ya suala moja la kimsingi: Jinsi gani katika kipindi cha muda mfupi kama huo, maisha ya maelfu ya watu yangeweza kubadilishwa kabisa na kutoka miongoni mwa umma uliobobea katika ushirikina na ukitawaliwa kabisa na viongozi wapotofu, roho takatifu kama hizo zingeinuka na kufanya vitendo vya kishujaa kama hivyo? Jibu linaweza kupatikana tu katika Nafsi ya 'Alí-Muḥammad, Báb. Hivyo, inashauriwa tujifunze na kutaamalii juu ya baadhi ya vifungu kutoka maandiko ya Bahá'u'lláh, 'Abdu'l-Bahá na Mlinzi juu ya Kiumbe huyo Mtakatifu.

Katika Wasia na Agano Lake, 'Abdu'l-Bahá husema:

**"Huu ndio msingi wa imani ya watu wa Bahá (acha maisha yangu yatolewe kwa ajili yao): 'Mtakatifu, Yule Aliyetukuka (Báb), ni Udhihirisho wa Umoja na Upekee wa Mungu na Mtangulizi wa Uzuri wa Kale. Mtakatifu Uzuri wa Abhá (acha maisha yangu yawe dhabihu kwa ajili ya marafiki Zake thabiti) ni Mdhihirishaji Mkuu Kabisa wa Mungu na Chimbuko la Asili Yake Takatifu Kabisa. Wengine wote ni watumishi Kwake na hutii amri Yake.'"**[25]

Katika *Mungu Yu Nasi*, tunasoma kifungu kifuatacho kilichoandikwa na Mlinzi:

**"Báb, akitangazwa kwa shangwe na Bahá'u'lláh kama 'Asili ya Asili zote,' 'Bahari ya Bahari zote,' 'Nukta Ambayo kwayo Uhalisia wa Mitume na Wajumbe huizungukia,' 'Ambaye kutoka Kwake Mungu amesababisha kutokea elimu ya vyote vile vilivyokuwepo na vitakavyokuwepo,' Ambaye 'daraja Lake hulizidi lile la Mitume Wote,' na Ambaye 'Ufunuo Wake hupita kabisa ufahamu na uelewa wa wateule wao wote,' aliwasilisha Ujumbe Wake na kutimiza dhima Yake. Yule Ambaye alikuwa, kwa maneno ya 'Abdu'l-Bahá, 'Asubuhi ya Ukweli' na 'Ishara ya Mwanga Mkuu Kabisa,' Ambaye ujio Wake huashiria mara moja mwisho wa 'Kipindi cha Utabiri' na mwanzo wa 'Kipindi cha Utimilizo,' kwa wakati huo huo kupitia Ufunuo Wake ameondoa giza lililokuwa limeshuka juu ya nchi Yake, na wakati huo huo kutangaza kuchomoza kulikotarajiwa kwa lile Duara lisilolinganishika ambalo wangavu Wake ungewafunika wanadamu wote."**[26]

Bahá'u'lláh Mwenyewe huelezea:

**"Kipindi kifupi kama hicho ambacho kingepaswa kutenganisha Ufunuo huu wenye nguvu kabisa na wa ajabu na Udhihirisho Wangu uliotangulia, ni siri ambayo hakuna mtu awezaye kuifumbua na fumbo ambalo hakuna akili iwezayo kulielewa."**[27]

'Abdu'l-Bahá husema:

**"Kutokea kwa Báb hufanana na mapambazuko, kwa kuwa mapambazuko hubeba ahadi ya jua. Mapambazuko ya Báb yaliahidi kuchomoza kwa Jua la Ukweli ambalo linapaswa kuufunika ulimwengu mzima."**[28]

## SEHEMU YA 12

Katika kipindi maisha Yake mafupi kama Mdhihirishaji wa Mungu duniani, Báb alifunua idadi kubwa ya vitabu na Nyaraka. Sasa kwa kuwa umemaliza usomaji wako juu ya maisha Yake, inapendekezwa kwamba ukariri sala Zake mbili ziizopo hapa chini.

> **"Kuna Muondoa shida yeyote isipokuwa Mungu? Sema: Mungu asifiwe! Yeye ni Mungu! Wote ni watumishi Wake, na wote hutii amri Yake!"[29]**


> **"Sema: Mungu hutosheleza vitu vyote juu ya vitu vyote, na hakuna chochote mbinguni au duniani bali Mungu hutosheleza. Kwa kweli, Yeye Mwenyewe nafsini Mwake yu Mjuzi, Mruzuku, Mwenye nguvu zote."[30]**

## SEHEMU YA 13

Katika kitengo cha tatu cha Kitabu cha 2, mlikazia jitihada zenu juu ya kujifunza jinsi ya kufanya mazungumzo juu ya mada kadhaa, hususan na wale ambao ni wapya katika Imani, wakati wa mfuatano wa ziara zilizofanyika kwenye kaya zao ndani ya jumuiya yenu. Sasa kwa kuwa mmemaliza kitengo hiki, mnaweza kuongeza kwenye orodha ya mada ambazo mngependa kuzungumzia historia ya maisha ya Báb. Kiasi gani cha maelezo ya kina mchaguayo kuongelea katika tukio lolote, bila shaka kitategemea mambo mengi. Lakini bila kujali hali, mnaweza kutumaini kushiriki maelezo mapana juu ya matukio makuu ya maisha Yake kama Mtangulizi wa Bahá'u'lláh na Mpiga mbiu wa Zama Mpya. Mara nyingi kurasa zifuatazo zinaweza kuwasaidia.

# Báb

## *Mtangulizi wa Siku Mpya*




**Báb alizaliwa 20 Oktoba 1819 huko Shíráz, mji ulioko sehemu ya kusini mwa Iran. Alikuwa bado mtoto mdogo, wakati baba Yake alipofariki. Alilelewa na mjomba Wake, ambaye alimpeleka shule akiwa na umri mdogo.**




**Mwalimu wa Báb kwa haraka alitambua uwezo Wake mkubwa na aliona kwamba hakuwa na uwezo wa kumfundisha mtoto asiye wa kawaida kama huyo. Báb alijaliwa na Mungu elimu ya asili.**



**Wakati ule watu wa Iran walikuwa wakingojea ujio wa Mjumbe mpya wa Mungu.
Walisali ili punde aweze kudhihirishwa, akileta kipindi cha amani na haki duniani.
Wengi waliyaacha makazi yao kwenda kumtafuta Yule Mwahidiwa.**




**Mnamo 23 Mei 1844, kijana mmoja aliwasili huko <u>Sh</u>íráz akimtafuta Yule Mwahidiwa. Báb alimkuta nje ya malango ya mji na akamwalika nyumbani Kwake kujipumzisha baada ya safari yake ndefu. Hapo Báb alitangaza kwamba Yeye Ndiye Yule Ambaye ujio Wake watu walikuwa wakingojea kwa shauku mno.**




**Neno “báb” maana yake lango au mlango. Báb alitangaza kwamba punde Mjumbe mwingine wa Mungu angetokea Ambaye angeunganisha watu wote wa ulimwengu kuwa familia moja. Báb alikuwa kama mlango ukiwaongoza wanadamu kuelekea wakati mpya na mtukufu ujao.**



**Idadi ya wafuasi wa Báb iliongezeka kwa haraka. Iran nzima, walianza kuenezo mafundisho matakatifu Aliyoyafunua.**




**Punde mamlaka za kiserikali na makasisi, ambao walikuwa wakihofia kupoteza madaraka yao, juu ya watu waliinuka dhidi ya Imani hii mpya ya Mungu. Walimfunga Báb katika ngome iliyokuwa sehemu ya mbali iliyojitenga ya nchi, mbali kabisa na wafuasi wake.**



**Wafuasi wa Báb walipata mateso ya kikatili sana. Walishambuliwa, kupigwa na kutupwa gerezani. Maelfu waliuawa, lakini Hoja ya Mungu iliendelea kuenea.**



**Mnamo 1850 Báb aliuawa kifo cha kishahidi. Kwa amri ya serikali, Yeye pamoja na mmoja wa wafuasi Wake walitundikwa uwanjani pamoja na kupigwa risasi na kikosi cha wanajeshi. Báb alikuwa na umri wa miaka 31 tu.**



**Báb aliyatoa maisha Yake ili kuandaa njia kwa ajili ya ujio wa Bahá'u'lláh, "Utukufu wa Mungu", Ambaye bendera ya Imani Yake ya Imani ilikusudiwa kuinuliwa katika kila kona ya sayari.**

# MAREJELEO


1. *Wanamapambazuko: Masimulizi ya Nabil ya Siku za Mwanzoni za Ufunuo wa Kibahá'í* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, chapisho la 1932, 2018), ku. 75–76 (toleo la Kiingereza).

2. Kama hapo juu, uk. 57.

3. Kama hapo juu, uk. 63.

4. Kama hapo juu, uk. 65.

5. Kutoka mazungumzo yaliyotolewa 23 Mei 1912, yaliyochapishwa katika *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu: Mazungumzo Yaliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá wakati wa Ziara Yake huko Marekani na Canada mnamo 1912* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 2012), aya. 2, uk. 196 (toleo la Kiingereza).

6. *Wanamapambazuko,* ku. 85–86 (toleo la Kiingereza).

7. Báb, iliyonukuliwa katika *Wanamapambazuko*, ku. 92–94 (toleo la Kiingereza).

8. *Wanamapambazuko*, ku. 142–43 (toleo la Kiingereza).

9. Kama hapo juu, uk. 146.

10. Kutoka mazungumzo yaliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá 23 Mei 1912, yaliyochapishwa katika *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu*, aya. 2, uk. 196 (toleo la Kiingereza).

11. *Wanamapambazuko*, ku. 148–50 (toleo la Kiingereza).

12. Kama hapo juu, uk. 198.

13. Kama hapo juu, uk. 212.

14. Kama hapo juu, uk. 213.

15. Kama hapo juu, uk. 249.

16. Báb, yailiyonukuliwa na Shoghi Effendi, *Mungu Yu Nasi* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, chapisho la 1974, 2019), uk. 34; pia katika *Wanamapambazuko*, ku. 315–16 (toleo la Kiingereza).

17. 'Abdu'l-Bahá, katika *Baadhi ya Maswali Yaliyojibiwa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, chapisho la 2014, 2016), na. 8.1–3, ku. 38–39 (toleo la Kiingereza).

18. *Wanamapambazuko*, uk. 507 (toleo la Kiingereza).

19. Kama hapo juu, ku. 307–8.

20. Kama hapo juu, uk. 508.

21. Kama hapo juu, uk. 509.

22. Kama hapo juu, uk. 512.

23. Kama hapo juu, uk. 513.

24. Báb, yaliyonukuliwa katika *Mungu Yu Nasi*, uk. 84; pia katika *Wanamapambazuko*, uk. 514 (toleo la Kiingereza).

25. *Wasia na Agano la 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, 1944, chapisho la 2013), uk. 39 (toleo la Kiingereza).

26. *Mungu Yu Nasi*, ku. 90–91 (toleo la Kiingereza).

27. Bahá'u'lláh, yaliyonukuliwa na Shoghi Effendi, *Utaratibu wa Ulimwengu wa Bahá'u'lláh: Barua Zilizoteuliwa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, chapisho la 1991, 2012), uk. 124 (toleo la Kiingereza).

28. *Abdul Baha juu ya Falsafa Takatifu* (Boston: The Tudor Press, 1918), ku. 51–52 (toleo la Kiingereza).

29. Báb, katika *Sala za Kibahá'í: Uteuzi wa Sala Zilizofunuliwa na Bahá'u'lláh, Báb na 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, chapisho la 2002, 2017), uk. 221 (toleo la Kiingereza).

30. Kama hapo juu, uk. 55.



# Maisha ya Bahá’u’lláh

## Kusudi

Kupata utambuzi wa ukuu wa
nguvu za kiroho zilizoachiliwa na Bahá’u’lláh
na kujifunza kusimulia historia ya maisha Yake

## SEHEMU YA 1

Bahá'u'lláh, Ambaye jina Lake lilikuwa Mírzá Ḥusayn-'Alí, alizaliwa 12 Novemba 1817 huko Ṭihrán, mji mkuu wa Uajemi. Baba yake, Mírzá Buzurg, alikuwa mtu mashuhuri ambaye alikuwa na cheo kikubwa katika baraza la mfalme wa Uajemi. Tangu umri mdogo, Bahá'u'lláh alionesha ishara za ukuu na ujuzi na hekima isiyo ya kawaida. Yeye hakuhudhuria shule ya kawaida na alipata mafunzo kiasi tu nyumbani. Kuhusu utoto Wake, 'Abdu'l-Bahá husema:

> **"Uzuri Uliobarikiwa, Bahá'u'lláh, alitokana na nasaba bora ya Uajemi. Tangu utoto wa mwanzoni kabisa Yeye alitofautishwa miongoni mwa ndugu na marafiki Zake. Walisema, 'Mtoto huyu ana uwezo usio wa ajabu.' Kwa hekima, akili na kama chanzo cha elimu mpya, aliuzidi umri Wake na alikuwa bora kuliko mazingira Yake. Wote waliomjua walishangazwa na upevu wa akili Yake. Ilikuwa kawaida kwao kusema, 'Mtoto kama huyu hataishi,' kwa kuwa kwa kawaida huaminika kwamba watoto waliokomaa kiakili mapema hawafiki utu uzima."[1]**

Katika Waraka mmoja, Bahá'u'lláh Mwenyewe husimulia hadithi kutoka utoto Wake kuhusu tukio moja alipohudhuria sherehe ya harusi ya mmoja wa ndugu zake huko Ṭihrán. Kama ilivyokuwa desturi wakati huo, karamu kubwa ilifanywa kwa siku saba mchana na usiku. Siku ya mwisho, yalifanyika maonesho ya vikaragosi kuhusu mfalme mmoja maarufu kama burudani kwa wageni. Bahá'u'lláh aliketi katika chumba cha juu kilichokuwa kinatazamana na uwanja ambako hema lilikuwa limesimikwa kwa ajili ya maonesho hayo.

Yeye hutuambia kwamba mchezo huo ulianza kwa kuingia kwa visanamu vidogo vidogo vichache vikiwa katika umbo la kibinadamu, vikitangaza mfalme alikuwa anakaribia kuja. Visanamu vingine zaidi punde vikatokea. Baadhi vilikuwa vinafagia na vingine vilikuwa vinanyunyizia maji katika kuandaa ujio wa mfalme. Kisha, mpiga mbiu wa mji aliingia kwenye eneo la tukio na kuwaambia watu kukusanyika kwa ajili ya kusikiliza mazungumzo ya mfalme. Makundi kadhaa ya waheshimiwa yalitokea na kuketi katika sehemu zao maalum. Hatimaye, mfalme aliingia kwa ufahari. Akiwa amevaa taji kichwani mwake, alitembea taratibu na kwa madaha na akaketi katika kiti cha enzi. Risasi zilifyatuliwa, matarumbeta yalipigwa, na hema lilijaa moshi.

Wakati moshi ulipokwisha, mfalme alikuwa bado ameketi kwenye kiti chake cha enzi, akiwa amezungukwa na mawaziri, wana-mfalme na maafisa wa serikali, wote wakiwa wamesimama kwa utulivu mbele yake. Muda huo, mwizi aliletwa mbele ya mfalme, ambaye alitoa amri kwamba akatwe kichwa. Yule muuaji mkuu alitekeleza maagizo yake bila kuchelewa. Baada ya mauaji, mfalme alianza mazungumzo na mawaziri na maafisa wake. Ghafla habari zilifika kwamba uasi ulikuwa umezuka katika mojawapo ya mipaka. Mara moja vikosi vilitumwa kwenda kuzima uasi huo. Dakika chache baadaye, milio ya mizinga ilisikika kwa nyuma, na ilitangazwa kwamba vikosi vya mfalme vilikuwa katika mapambano dhidi ya waasi.

Hivyo, ule mchezo uliendelea. Bahá'u'lláh alitatanishwa sana na asili ya maonesho hayo. Baada ya kumalizika na pazia kuondolewa, alimuona mtu akitokea nyuma ya lile hema amebeba sanduku kwapani mwake. "Sanduku hili ni nini," Bahá'u'lláh alimuuliza, na nini asili ya maonesho hayo?" Yule mtu alijibu, "Mikogo na vikorokoro vyote hivi vilivyorembwa," mfalme, wana-mfalme na mawaziri, fahari na utukufu wao, nguvu na uwezo wao, kila kitu

ulichokiona, sasa vimo ndani ya sanduku hili."[2] Maelezo haya yalimgusa sana Bahá'u'lláh Ambaye baadaye alitamka:

> **"Tangu siku ile, mapambo yote ya ulimwengu yameonekana katika macho ya Kijana huyu sawa na maonesho yale. Kamwe hayajawahi, wala daima hayatakuwa, yenye uzito wowote wala umuhimu wowote, hata kufikia kiasi cha punje ya mbegu ya haradali. . . .**

> **"Hivi punde mapambo haya ya nje, hazina hizi zinazoonekana, majivuno haya ya kidunia, majeshi haya yaliyojipanga, mavazi haya yaliyoapambwa, roho hizi zenye kiburi na majivuno, vyote vitaingizwa ndani ya mipaka ya kaburi, kama vile vilivyoingizwa ndani ya sanduku lile. Katika macho ya wale wenye umaizi, ugomvi, mafarakano na majivuno yote haya yamekuwa, na daima yatakuwa, kama vile mchezo ya kuigiza na burudani za watoto wadogo."[3]**

Hadithi nyingine inayohusishwa na utoto wa Bahá'u'lláh inahusu ndoto ambayo baba Yake aliiota ambamo Bahá'u'lláh alionekana kuwa

> "akiogelea ndani ya bahari kubwa, isiyo na mwisho. Mwili wake uling'aa kwenye maji kwa mng'ao ambao uliiangazia bahari. Kuzungukia kichwa Chake, ambacho kilionekana kwa uwazi juu ya yale maji, nywele Zake ndefu na nyeusi zilisambaa katika pande zote, zikielea kwa wingi mno juu ya mawimbi. . . . Samaki lukuki walimzunguka, kila mmoja aking'ang'ania kwa uthabiti kwenye ncha ya unywele mmoja. Wakivutiwa sana na mng'ao wa uso Wake, walimfuata upande wowote ule alikoelekea. Japokuwa idadi yao ilikuwa kubwa, na japokuwa waling'ang'ania sana nywele zake, hakuna hata unywele mmoja ulioonekana kung'oka kichwani mwake, wala madhara kidogo kabisa kuathiri nafsi Yake. Akikuwa huru na bila kuzuiliwa, Alisonga mbele juu ya yale maji na samaki wote walimfuata."[4]

Akiguswa na ndoto hii, baba Yake Bahá'u'lláh alimuomba mtu anayejulikana kwa umaizi wake amtafsirie ndoto hiyo. Mtu huyu, kana kwamba alivuviwa na kianga cha utukufu siku zijazo wa Bahá'u'lláh, alisema:

> "Ile bahari isiyo na mipaka uliyoiona katika ndoto yako si kingine bali ni ulimwengu wa uhai. Bila msaada na peke Yake, mwanao atajipatia mamlaka ya juu kabisa juu ya ulimwengu. Kokote apendako, ataenda bila kuzuiliwa. Hakuna atakayepinga mwendo Wake, hakuna atakayezuia maendeleo Yake. Samaki lukuki huashiria msukosuko ambao Yeye atauamsha miongoni mwa watu na koo za dunia. Watakusanyika karibu Yake, na Kwake watang'ang'ania. Akihakikishiwa ulinzi usioshindwa wa Mwenyezi, msukosuko huu kamwe hautadhuru nafsi Yake, wala upweke Wake ndani ya bahari ya maisha kutahatarisha usalama Wake."[5]

1. Jina la Bahá'u'lláh lilikuwa lipi? ______________________________

2. Alizaliwa tarehe ngapi? ______________________________

3. Alizaliwa wapi? ______________________________

4. Kwa jina gani lingine Uajemi inajulikana leo? ______________________________

5. Baba Yake Bahá'u'lláh alikuwa anaitwa nani? ______________________________

6. Baba Yake Bahá'u'lláh alikuwa na wadhifa gani? ___________________________

_______________________________________________________________________

7. Ni ishara zipi Bahá'u'lláh alizionesha alipokuwa mtoto? ______________________

_______________________________________________________________________

8. Ni aina gani ya elimu Bahá'u'lláh aliipata? ________________________________

_______________________________________________________________________

9. Elezea maonesho ya vikaragosi ambayo Bahá'u'lláh aliyaona utotoni Mwake.

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

10. Bahá'u'lláh alifikiria nini alipojua kwamba kila kitu alichokiona katika ule mchezo—mfalme, mawaziri, wanajeshi na kiti cha enzi vyote vikiwa vimetupwa ndani ya lile sanduku? __________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

_______________________________________________________________________

11. Bahá'u'lláh alitamka kwamba tangu siku ile alipoona yule mfalme, mawaziri wake, wanajeshi na kiti cha enzi vimetupwa ndani ya sanduku: "______________ yote ya ________________ yameonekana katika __________ ya ___________ huyu sawa na ________________ . Kamwe ___________________ , wala daima hayatakuwa, yenye ______________________________ wowote, hata kufikia kiasi cha ________ ya mbegu ya _______________ . . . . Hivi punde _______________ haya ya nje, _____________ hizi __________________ , _______________ haya ya kidunia,

__________ haya yaliyojipanga, _____________ haya ____________________ , _____________ hizi zenye __________ na ________________ vyote vitaingizwa ndani ya mipaka ya ___________ , kama vile vilivyoingizwa ndani ya _____________ lile. Katika macho ya wale wenye ___________ , ___________ , _______________ na ___________ yote haya yamekuwa, na daima yatakuwa, kama vile _____________ _______________ na _____________ za watoto _____________ .”

12. Simulia kwa maneno yako mwenyewe ndoto ya Mírzá Buzurg.

_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________

13. Bahari katika ile ndoto humaanisha nini? ___________________________________
_____________________________________________________________________

14. Wale samaki wengi waliokusanyika kumzunguka Bahá’u’lláh katika ndoto walimaanisha nini? ______________________________________________________
_____________________________________________________________________

15. Bahá’u’lláh kusonga mbele kwa uhuru na bila kuzuiliwa juu ya yale maji ilimaanisha nini? __________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________

## SEHEMU YA 2

Wadhihirishaji watakatifu wamejaliwa elimu ya kiasili na hawahitaji kupata mafunzo shuleni na vyuo vikuu. Wao ni waelimishaji na siyo waelimishwaji. Bahá’u’lláh husema:

> **“Mdhulumiwa Huyu hakwenda shule wala kuhudhuria migongano ya hoja ya wanazuoni. Kwa uhai Wangu! Siyo kwa hiari Yangu kwamba**

**nimejifunua Mwenyewe, bali Mungu, kwa kupendezwa Kwake Mwenyewe, Amenidhihirisha.”**[6]

Akiongelea juu ya elimu ya kiasili ya Bahá’u’lláh, ‘Abdu’l-Bahá huelezea:

**“Hakuna aliyeingia machoni Pake bila kustaajabishwa na uwezo Wake. Wanazuoni waliomwendea walishangazwa na elimu Yake, walakini Yeye abadan hakwenda shule wala kufunzwa na watu. Marafiki Zake na familia Yake wote huthibitisha hili, walakini Mafundisho Yake ndio roho ya zama hizi.**

**“Jua lenyewe ni chanzo cha mwanga, na halichukui mwanga kutoka vyanzo vingine. Walimu Watakatifu wana mwanga wa kiasili; Wana elimu na uelewa wa vitu vyote ulimwenguni; vingine vyote hupata mwangaza kutoka Kwao na kupitia Kwao sanaa na sayansi zinahuishwa katika kila zama.”**[7]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Jua lenyewe ni ____________________ ; na halichukui _____________ kutoka __________________ .

   b. Walimu Watakatifu wana _____________________________ .

   c. Walimu Watakatifu wana ______________ na ______________ wa vitu vyote ulimwenguni.

   d. Kutoka kwa Walimu Watakatifu, vingine vyote ________________________ .

   e. Kupitia Walimu Watakatifu sanaa na sayansi __________________________ ___________________ .

2. Pamoja na washiriki wengine wa kikundi chako, jadilianeni maana ya kirai “elimu ya kiasili” na jinsi elimu ya kiasili inavyotofautiana na elimu ya kujifunza.

3. Kariri teuzi la hapo juu kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh.

## SEHEMU YA 3

Kadiri Bahá’u’lláh alivyoendelea kukua, ishara za Ukuu Wake zilizidi kudhihirika. Wakati alipokuwa kijana, alikuwa mashuhuri kwa akili Yake makini, tabia Yake bora kabisa, ukarimu na huruma Yake. Alikuwa na uwezo wa kutatua matatizo makubwa mno na wa kujibu maswali ya magumu na ya kina. Lakini licha ya vipaji Vyake vya ajabu, kamwe hakutafuta cheo wala umaarufu. Wakati baba Yake alipofariki, Bahá’u’lláh aliombwa kufuata nyayo zake na kujitwalia cheo cha baba Yake katika baraza la mfalme. Lakini Yeye alikataa. Yeye hakuvutiwa na vyeo na heshima ya ulimwengu huu. Shauku Yake ilikuwa katika kuwatetea masikini na kuwalinda wanyonge. Alipofikisha umri wa miaka kumi na minane Bahá’u’lláh alimuoa Ásíyih Khánum na nyumba yao ikawa kimbilio kwa wote. Hakuna aliyenyimwa ukarimu wao.

Bahá'u'lláh alikuwa na umri wa miaka ishirini na saba, wakati Báb alipotangaza Ujumbe Wake kwa Mullá Ḥusayn huko Shíráz Mei 23, 1844. Hata miezi mitatu ilikuwa haijapita baada ya tukio hili la kihistoria, Bahá'u'lláh alipokea gombo kutoka kwa Báb lililokuwa na baadhi ya Maandiko Yake. Yeye mara moja alishuhudia juu ya ukweli wa Ufunuo wa Báb na akainuka kuendeleza Mafundisho Yake. Hadithi kuhusu namna Bahá'u'lláh alivyopokea gombo hilo ni kama ifuatavyo.

Muda mfupi baada ya Báb kuteua wanafunzi Wake wateule, zile Herufi kumi na nane za Walio Hai, Yeye Aliwaita kuja mbele Yake na kuwapa maagizo ya kutawanyika na kufundisha Ujumbe mpya. Alimpa kila mmoja jukumu maalum, Akiwapa jukumu baadhi yao kwenda kwenye majimbo walikozaliwa kama maeneo ya jitihada zao. Kati ya roho hizi kumi na nane zilizobarikiwa, Quddús alichaguliwa kuambatana Naye katika hija Yake huko Makka, ambako Alihitaji kutangaza Ujumbe Wake. Kwa Mullá Ḥusayn, yule wa kwanza kumwamini Yeye, Alimwambia maneno haya: "Usihuzunike kwamba hukuchaguliwa kuambatana Nami katika safari Yangu ya hija huko Hijáz. Badala yake, Nikuagiza kwenye ule mji ambao umehifadhi Fumbo lenye utakatifu mkubwa mno, kiasi kwamba, siyo Hijáz wala Shíráz inaweza kutumaini kushindana nao."[8] Yeye Alimpa Mullá Ḥusayn gombo na kumuagiza kwenda Ṭihrán. Alimwambia amsihi Mungu ili awezeshwe kuutambua mwanga wa siri iliyofichwa katika mji ule na kuingia katika uwepo wa Mpendwa.

Mullá Ḥusayn aliondoka kwenda kutekeleza jukumu lake na, baada ya kupita miji kadhaa, aliwasili Ṭihrán. Hapo alichukua chumba katika shule ya mafunzo ya kidini. Mojawapo ya vitendo vyake vya kwanza ilikuwa ni kuutangaza Ujumbe wa Báb kwa mkuu wa shule hiyo, ambaye aliukataa kwa ufidhuli. Hata hivyo, mwanafunzi mmoja kijana aliyasikia mazungumzo yao bila kukusudia na aliguswa mno na maneno ya msafiri huyu. Aliamua kumtembelea usiku wa manane ili kujifunza zaidi juu ya ujumbe alioutangaza kwa shauku kubwa mno. Mullá Ḥusayn alimpokea kijana huyo na akazungumza naye kwa heshima na wema mkuu. Alimwambia mwanafunzi huyo kwamba sasa ameelewa kwa nini alifika mahali pale. Mkuu wa shule aliukataa kwa dharau Ujumbe aliokuwa ameuleta. "Tumaini langu," Mullá Ḥusayn alisema, "ni kwamba mwanafunzi wake angeweza, tofauti na mwalimu wake, kuutambua ukweli wa ujumbe."[9]

Wakati wa mazungumzo yao, Mullá Husayn alimuuliza mwanafunzi huyo alitokea wapi. Yeye alimjibu kwamba alitokea wilaya ya Núr, katika jimbo la Mázindarán. "Hebu niambie," Mullá Ḥusayn aliuliza, "leo hii miongoni mwa familia ya marehemu Mírzá Buzurg-i-Núrí, ambaye alikuwa anasifika kwa tabia yake, ucheshi wake, na mafanikio yake ya kisanii na kielimu, kuna yeyote ambaye amejithibitisha kuwa mwenye uwezo wa kudumisha tunu za hali ya juu za kaya hiyo mashuhuri?"[10]

"Naam," yeye alijibu, "miongoni mwa watoto wake wa kiume waishio hivi sasa, mmoja amejipambanua Mwenyewe kwa zile sifa zilizombainisha baba Yake. Kwa maisha Yake maadilifu, mafanikio Yake ya hali ya juu, wema Wake wa upendo na ukarimu Wake, yeye amethibitibika kuwa wa uzao bora wa baba bora." "Yeye ana kazi gani?" Mullá Ḥusayn aliuliza. "Yeye huwafariji wenye huzuni na huwalisha wenye njaa." "Na vipi kuhusu cheo na daraja lake?" "Hana chochote, zaidi ya kufanya urafiki na masikini na wageni." "Jina lake nani?" "Husayn-'Alí."[11]

Kwa kila jibu, Mullá Ḥusayn alijawa na furaha zaidi. "Yeye hutumiaje muda Wake?" aliuliza zaidi. "Hutembea nyikani na hufurahia uzuri wa mashambani." "Ana umri gani?" "Miaka Ishirini na minane." Uso wa Mullá Ḥusayn uling'aa kwa ridhaa na furaha pale

alipomuuliza yule kijana: “Nadhani unakutana Naye mara nyingi?” “Natembelea nyumbani Kwake mara kwa mara,” yeye alijibu. “Utaweza kumpelekea amana kutoka kwangu?” “Bila shaka kabisa,” lilikuwa jibu lake. Kisha Mullá Ḥusayn akampa lile gombo likiwa limezungushiwa kitambaa na kumuomba kuliwasilisha kwa Bahá’u’lláh alfajiri siku iliyofuata. “Kama akiridhia kunijibu,” Mullá Ḥusayn aliongezea, “kwa hisani yako utaweza kunijulisha jibu Lake?”[12] Yule mwanafunzi alilichukua lile gombo na, alfajiri, aliinuka kutimiza ombi la Mullá Ḥusayn.

Wakati akikaribia nyumba ya Bahá’u’lláh, alimuona ndugu Yake, Mírzá Músá, amesimama kwenye lango na akamuelezea sababu ya ziara yake. Mírzá Músá alimpeleka yule kijana hadi mbele ya Bahá’u’lláh, na lile gombo likawekwa mbele Yake. Bahá’u’lláh aliwaambia waketi. Baada ya kulifungua lile gombo, akaanza kusoma kwa sauti baadhi ya vifungu vyake. Alipomaliza kusoma ukurasa mmoja tu, akamgeukia ndugu yake na kusema: “Músá, úna la kusema? Kwa kweli nasema, yeyote anayeiamini Qur’an na kutambua asili yake Takatifu na bado akasita, japo kwa kitambo kidogo, kukubali kwamba maneno haya yanayosisimua roho yamejaliwa uwezo ule ule uhuishao, kwa hakika kabisa amekosea katika uamuzi wake na amepotea kutoka njia ya haki.”[13] Akimruhusu yule kijana kuondoka mbele Yake, Bahá’u’lláh alimuomba kumpelekea Mullá Ḥusayn, kibonge cha sukari na kifurushi cha majani ya chai, kama zawadi kutoka Kwake, na kumpelekea shukrani na upendo Wake.

Akiwa amejawa na furaha, yule kijana aliinuka na kuharakia kurudi kwa Mullá Ḥusayn. Akawasilisha ile zawadi na ujumbe kutoka kwa Bahá’u’lláh. Hakuna maneno yawezayo kuelezea furaha ya Mullá Ḥusayn alipovipokea. Akiinamisha kichwa chake, aliipokea ile zawadi na kuibusu kwa upendo mkubwa. Kisha akamkumbatia yule kijana, akayabusu macho yake, na akasema: “Rafiki yangu mpendwa sana! Naomba kwamba kama vile ulivyoufurahisha moyo wangu, Mungu akujalie furaha ya milele na kujaza moyo wako kwa furaha isiyo na kikomo.”[14] Yule kijana alishangazwa sana na mwenendo wa Mullá Ḥusayn. Ni nini, alistaajabu, kinaweza kuwa asili ya fundo lililoziunganisha roho hizi mbili? Ni nini kinaweza kuwa chanzo cha urafiki kati yao? Kwa nini Mullá Ḥusayn ilimbidi aonesha furaha kama hiyo alipopokea ile zawadi ndogo kabisa kutoka kwa Bahá’u’lláh? Yule kijana alikabiliwa na fumbo ambalo hakuweza kulifumbua.

Siku chache baadaye, Mullá Ḥusayn aliondoka kwenda Khurásán, jimbo lililoko kaskazini mashariki mwa Iran. Wakati akimuaga yule mwanafunzi kijana kutoka Núr, alimwambia: “Usimnong’one kwa yeyote yale uliyoyasikia na kuyashuhudia. Acha hii iwe siri iliyofichwa kifuani mwako. Usilifichue jina Lake, kwani wale wenye husuda na daraja lake watainuka kumdhuru. Katika nyakati zako za taamuli, omba kwamba Mwenyezi amlinde, ili, kupitia Kwake, Aweze kuwainua walio dhalili, awatajirishe masikini, na kuwakomboa walioanguka. Siri ya mambo imefichwa kutoka machoni petu. Jukumu letu ni kupaza mwito wa Siku Mpya na kutangaza Ujumbe huu Mtakatifu kwa watu wote. Roho nyingi, katika mji huu, zitamwaga damu zao katika njia hii. Damu hiyo itaumwagilia Mti wa Mungu, itaufanya ustawi, na kuwafunika wanadamu wote.”[15]

1. Báb alifanya nini baada ya kuwateua wale Herufi kumi na nane za Walio Hai? ____

   ______________________________________________________________

2. Báb alimchagua nani kuambatana Naye katika safari Yake ya hija huko Makka? ___

   ______________________________________________________________

3. Je, Hijáz hurejelea kwenye nchi gani? ____________________________________

4. Kwa Mullá Ḥusayn, yule wa kwanza kumwamini Yeye, Báb Alimwambia maneno haya: "__________________ kwamba hukuchaguliwa kuambatana Nami katika _______________________________ huko _____________ . Badala yake, Nikuagiza kwenye ule mji ambao umehifadhi ____________ lenye _______________ mkubwa mno, kiasi kwamba, siyo _____________ wala ____________ inaweza kutumaini ___________________________ ."

5. Báb Alimpa nini Mullá Ḥusayn? _________________________________________

_____________________________________________________________________

6. Alipofika Ṭihrán Mullá Ḥusayn alichukua chumba katika shule ya mafunzo ya kidini. Jinsi gani mkuu wa shule alivyojibu kuhusu Ujumbe wa Báb? _________________

_____________________________________________________________________

7. Kwa nini Mungu alimuongoza Mullá Ḥusayn kwenye shule hiyo? ______________

_____________________________________________________________________

8. Yule mwanafunzi aliyeukubali Ujumbe wa Báb alikuwa anatokea wapi? _________

_____________________________________________________________________

9. Makazi ya mababu Zake ya Bahá'u'lláh yalikuwa wapi? ______________________

10. Kama ilivyoelezwa na yule mwanafunzi kutoka Núr, alipokuwa akijibu maswali ya Mullá Ḥusayn:

   – Baba Yake alijulikana kwa sifa gani bainifu? ___________________________

   _______________________________________________________________

   – Bahá'u'lláh alikuwa akijishughulisha na nini? __________________________

   _______________________________________________________________

   – Ni lipi lilikuwa daraja na cheo Chake? ________________________________

   _______________________________________________________________

   – Yeye aliutumiaje muda Wake? ______________________________________

   _______________________________________________________________

11. Mullá Ḥusayn alimuomba yule mwanafunzi kutoka Núr afanye nini? ____________

_____________________________________________________________________

12. Baada ya kumaliza kusoma ukurasa mmoja tu wa lile gombo lililotumwa na Báb, Bahá'u'lláh alisema: "Kwa kweli nasema, yeyote anayeiamini ______________ na kutambua _____________ yake _______________ na bado _____________ , japo kwa _____________________________ , kukubali kwamba _____________ haya yanayosisimua roho yamejaliwa ___________ ule ule ___________ , kwa hakika kabisa _________________ katika _______________ wake na _________________ kutoka njia ya _____________ ."

13. Mullá Ḥusayn aliipokeaje ile zawadi kutoka kwa Bahá'u'lláh? _________________
______________________________________________________________________

14. Kitu gani kilimshangaza yule mwanafunzi kijana kuhusu mwenendo wa Mullá Ḥusayn pale alipopokea zawadi? _______________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

15. Simulia kwa maneno yako mwenyewe kile ambacho Mullá Ḥusayn alimwambia yule mwanafunzi kutoka Núr wakati alipokuwa akimuaga.

______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 4

Báb humtaja Bahá'u'lláh kama "Yule Ambaye Mungu atamdhihirisha". Maandiko ya Báb, kikiwemo Kitabu Chake Kitakatifu kabisa, Bayán, kina marejeleo mengi mno

yanayomsifu Yule ambaye Mungu atamdhihirisha. Hapo chini kuna mateuzi machache tu kutoka Maandiko ya Báb ambayo hutupa kianga cha Daraja la Bahá'u'lláh na uhusiano kati ya Wadhihirishaji hawa Pacha.

> **"Na ujue kwa hakika kwamba kwa Paradiso humaanisha utambuzi wa, na utii kwa Yule Ambaye Mungu atamdhihirisha, na kwa moto, uenzi wa zile roho ambazo zingeshindwa kumtii Yeye au kujiweka chini ya ridhaa Yake njema."[16]**

> **". . . takasa sikio lako ili lisisikie mtajo wowote zaidi ya Mungu, na takasa jicho lako ili lisione kingine ila Mungu, na dhamira yako ili isione chochote kile zaidi ya Mungu, na ulimi wako ili usitangaze chochote ila Mungu, na mkono wako ili usiandike chochote kile isipokuwa maneno ya Mungu, na ufahamu wako ili usielewe chochote ila Mungu, na moyo wako ili usiendekeze tamaa yoyote ila Mungu, na hali kadhalika takasa vitendo vyako vyote na shughuli zako ili uweze kulelewa katika paradiso ya upendo safi, na pengine utaweza kuufikia uwepo wa Yeye Ambaye Mungu atamdhihirisha, ukipambwa kwa usafi ambao Yeye huupenda sana, na uweze kutakaswa kutoka yeyote ambaye amekengeuka kutoka Kwake na hamsaidii Yeye."[17]**

> **"Sema, kwa kweli, ridhaa njema ya Yeye Ambaye Mungu atamdhihirisha ni ridhaa njema ya Mungu, wakati maudhi kwa Yeye Ambaye Mungu atamdhihirisha si kingine ila maudhi kwa Mungu."[18]**

1. Nani "Yeye Ambaye Mungu atamdhihirisha" humrejelea? ____________________

2. Báb anawahimiza wafuasi Wake kujiandaa ili wakubaliwe mbele ya Yeye Ambaye Mungu atamdhihirisha. Je, Aliwaambia wafanye nini?

   ______________________________________________________________
   ______________________________________________________________
   ______________________________________________________________
   ______________________________________________________________
   ______________________________________________________________
   ______________________________________________________________
   ______________________________________________________________

3. Chagua mojawapo kati ya nukuu hapo juu na uikariri.

## SEHEMU YA 5

Tangu pale Bahá'u'lláh alipoushuhudia ukweli wa Ufunuo wa Báb, Yeye aliinuka kuutangaza. Ziara ya kwanza aliyoifanya ilikuwa ni nyumbani kwa mababu Zake huko Núr, katika jimbo la Mázindarán. Huko alikwenda kwenye makazi ya ukoo Wake katika kijiji cha Tákur.

Habari za kuwasili kwa Bahá'u'lláh huko Tákur zilienea kwa haraka katika eneo lote. Wengi wa maafisa na waheshimiwa wa eneo hilo walikuja kumsalimu na wakati huo huo kupata habari za Mfalme, baraza lake na masuala ya nchi. Lakini Bahá'u'lláh alijibu maswali yao kwa shauku ndogo. Yeye kwa haraka alibadili mada na kuanza kuelezea, kwa ufasaha kabisa, Ujumbe uliotangazwa na Báb. Maneno Yake yalikuwa ya kusadikisha mno na hoja Zake za busara mno kiasi kwamba wote walishangazwa. Wale waliomsikiliza walishangazwa kwamba hata mtu mwenye daraja la juu kama Lake, angevutiwa sana na mambo ambayo kwa kawaida yaliwahusu makasisi na viongozi wa dini. Shauku Yake na kina cha ujuzi Wake punde vilivutia idadi kubwa ya watu kwenye Hoja ya Báb, wakiwemo watu mashuhuri na watu wa ukoo Wake Mwenyewe. Hakuna yeyote aliyefika mbele Yake angeweza kujizuia kushawishika kwa maneno Yake matamu au kuthubutu kupinga ukweli wa maelezo Yake, hata mmoja isipokuwa mjomba Wake Mwenyewe.

Mjomba huyu alifanya kila lililowezekana kumpinga Bahá'u'lláh na ukweli wa Ujumbe ambao alikuwa ameuleta. Alipotambua kwamba asingeweza kufanya hivyo, alikwenda kwa kasisi mashuhuri wa Kiislamu na kuomba msaada wake. Yeye alilalamika kwamba Bahá'u'lláh alikuja Núr na, ingawa hakuwa miongoni mwa makasisi, alikuwa akizungumzia mambo ya kidini. Alimtahadharisha kasisi huyo kwamba kila mtu aliyekwenda mbele ya Bahá'u'lláh alipumbazwa Naye na kukumbwa na nguvu ya maneno Yake. "Sijui kama ni mchawi," yeye alisema, "au kama anachanganya na chai dawa fulani ya ajabu ambayo humfanya kila anayekunywa chai hiyo kuwa mhanga wa uchawi wake."[19]

Akijua kwamba kamwe asingeweza kufanikiwa kushindana na Bahá'u'lláh, yule kasisi alipuuzia maombi ya mjomba huyo. Lakini Ujumbe wa Báb uliendelea kuenea kama moto nyikani, katika wilaya nzima. Wakiingiwa na taharuki, wafuasi wa yule kasisi walianza kumshinikiza achukue hatua ya namna fulani. Hatimaye aliamua kuwatuma wanafunzi wake wawili wenye weledi mkubwa kumtembelea Bahá'u'lláh na kuchunguza asili ya Ujumbe aliokuwa akiueneza. Hii ndiyo hadithi ya kile kilichotokea, pale wale wawakilishi wawili walipokwenda mbele ya Bahá'u'lláh.

Walipowasili huko Tákur na kuambiwa kwamba Bahá'u'lláh ashaondoka kwenda kwenye nyumba Yake ya majira ya baridi, wale wawakilishi wa kasisi waliamua kumfuata huko. Walipowasili, walimkuta Bahá'u'lláh akishughulika na kufunua fasiri juu ya mojawapo ya sura za Qur'an. Walipoketi na kumsikiliza, walivutiwa mno kwa ufasaha wa maelezo Yake kwa namna isiyo ya kawaida alivyozungumza. Mmojawapo wa wale wawakilishi, akishindwa kujizuia, aliinuka kutoka kwenye kiti chake na akaenda nyuma ya chumba hicho na katika hali ya heshima na unyenyekevu, alisimama tuli karibu na mlango. Huku akitetemeka na macho yakiwa yamejaa machozi, alimwambia mwenzi wake: "Sina uwezo wa kumhoji Bahá'u'lláh. Maswali niliyopanga kumuuliza yametoweka ghafla katika kumbukumbu yangu. Upo huru kuendelea na uchunguzi wako au kurejea peke yako kwa mwalimu wetu na kumjulisha juu ya hali ambamo nimejikuta mwenyewe. Mwambie kwa niaba yangu kwamba kamwe siwezi kurejea tena kwake. Siwezi kukiacha tena kizingiti hiki." Lakini yule mwakilishi mwingine vile vile akipumbazwa na maneno ya Bahá'u'lláh naye alifuata mfano wa rafiki yake. "Nimeacha kumtambua mwalimu wangu," lilikuwa jibu lake. "Wakati huu huu, nimeapa kwa Mungu kutoa siku zilizobaki za maisha yangu kwa ajili ya kumtumikia Bahá'u'lláh, Bwana wangu wa kweli na wa pekee."[20]

Habari za kubadilika kwa wanafunzi wa yule kasisi zilienea kwa haraka miongoni mwa watu wa Núr. Watu mashuhuri, maafisa wa serikali, viongozi wa kidini, wafanya biashara na wakulima walisongamana mbele ya Bahá'u'lláh. Mamia waliletwa chini ya bendera ya Hoja

ya Bab. Hakuna yeyote, isipokuwa Bahá'u'lláh, walakini alijyeua kwamba mateso mabaya sana punde yangefuata, mateso ambayo yangeikata mizizi yenyewe hasa ya miche hii mingi michnga na iliyochipuka hivi karibuni.

1. Bahá'u'lláh alifanya nini baada ya kushuhudia juu ya ukweli wa ufunuo wa Báb? __

 ______________________________________________________________________

2. Bahá'u'lláh alipokelewaje na wakazi wa Núr? ______________________________

 ______________________________________________________________________

3. Kwa nini baadhi ya watu walishangazwa na jinsi Bahá'u'lláh alivyojibu maswali yao?

 ______________________________________________________________________

 ______________________________________________________________________

 ______________________________________________________________________

4. Mjomba Wake Bahá'u'lláh alifanya nini pale Bahá'u'lláh alipoanza kutangaza Hoja ya Báb? ______________________________________________________________

 ______________________________________________________________________

 ______________________________________________________________________

 ______________________________________________________________________

5. Kwa nini yule kasisi maarufu wa Kiislamu alipuuzia ombi la mjomba wa Bahá'u'lláh?

 ______________________________________________________________________

 ______________________________________________________________________

6. Yule kasisi hatimaye aliamua kufanya nini pale aliposhinikizwa na wafuasi wake?

 ______________________________________________________________________

 ______________________________________________________________________

7. Kwa maneno yako mwenyewe simulia hadithi ya wale wawakilishi wawili wa yule kasisi ambao walikwenda mbele ya Bahá'u'lláh.

 ______________________________________________________________________

 ______________________________________________________________________

 ______________________________________________________________________

 ______________________________________________________________________

 ______________________________________________________________________

 ______________________________________________________________________

 ______________________________________________________________________

 ______________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

8. Je, mazungumzo ya wale wawakilishi wawili yalikuwa na matokeo gani juu ya maendeleo ya Hoja ya Báb huko Núr? ________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 6

Kile ambacho Bahá'u'lláh alifanya katika wilaya ya Núr, ndicho anachotuambia tufanye—kuinuka na kutangaza Hoja ya Mungu. Hebu basi tujifunze na kutafakari juu ya maneno yafuatayo ya Bahá'u'lláh, tukikumbuka kwamba baada ya kuukubali Ufunuo wa Báb, kitendo Chake cha kwanza kilikuwa kuinuka na kushiriki Ujumbe na mamia kwa mamia ya roho.

> **"Ewe msafiri katika njia ya Mungu! Twaa sehemu yako ya bahari ya neema Yake, na usijinyime mwenyewe vile vitu ambavyo vimefichika katika vina vyake. Uwe miongoni mwa wale ambao wametwaa kutoka hazina zake. Tone la umande kutoka bahari hii, kama lingedondokea juu ya vile vyote viliyomo mbinguni na duniani, lingetosheleza kuwatajirisha kwa fadhili za Mungu, Mweza, Mjua—Vyote, Mwenye Hekima—Kabisa. Kwa mikono ya kujikana teka kutoka maji yake yatiayo uzima, na unyunyizie kwayo viumbe vyote, ili viweze kutakaswa kutokana na vizuizi vyote vya kibinadamu na viweze kukaribia kiti chenye nguvu cha Mungu, Mahali hapa pang'aapo na kutukuzwa.**
>
> **"Usihuzunike ikiwa utaifanya wewe pekee yako. Acha Mungu awe atoshelezaye vyote kwako. Zungumza na Roho Wake kwa ukaribu kabisa, na uwe miongoni mwa wale wenye shukurani. Tangaza Hoja ya Bwana wako kwa wote walioko mbinguni na duniani. Ikiwa mtu yeyote akiitika mwito wako, muwekee wazi mbele yake lulu za hekima za Bwana, Mungu wako, ambazo Roho Wake**

**amekushushia, na uwe miongoni mwa wale ambao kwa kweli huamini. Na ikiwa yeyote ataikataa zawadi yako, geukia mbali kutoka kwake, na weka tumaini na imani yako kwa Bwana, Mungu wako, Bwana wa malimwengu yote.”**[21]

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Bahá’u’lláh hutuambia tutwae sehemu yetu ______________________________ ______________________ .

   b. Tusijinyime wenyewe ______________________________________________ ______________________________________ .

   c. Tone la umande kutoka bahari ya neema Yake, kama lingedondokea juu ya vyote viliyoko mbinguni na duniani, lingetosheleza ____________________________ _________________________________________________________________ ______________________________________ .

   d. Tunaambiwa kuteka _______________________ na _____________________ , kunyunyizia ______________________________________________________ .

   e. Tusihuzunike ikiwa ________________________________________________ .

   f. Tuzungumze ________________________________________________ na tuwe wenye __________________________ .

   g. Tuntangaze _______________________________________________________ ______________________________________ .

   h. Ikiwa mtu yeyote akiitika mwito wetu, Bahá’u’lláh hutuambia _________ _________________________________________________________________ _____________________________________________ .

   i. Ikiwa mtu yeyote akiikataa zawadi yetu, tunapaswa _________________ _________________________________________________________________ ________________________________________________________________ .

## SEHEMU YA 7

Ufunuo Mtakatifu ni endelevu. Mungu hufunua Mapenzi Yake hatua kwa hatua kupitia Wadhihirishaji Wake Ambao huja wakati hadi wakati kadiri jamii ya wanadamu inavyoendelea kutoka hatua moja hadi nyingine. Huku akithibitisha baadhi ya kweli za msingi, kila Mdhihirishaji huleta seti mpya ya sheria na amri zinazolingana na uwezo wa jamii ya wanadamu na hubatilisha zingine, ambazo hazihitajiki tena, zilizoletwa na Yule Aliyekuja kabla Yake. Walakini, inaweza kuwa vigumu kwa watu kuacha ya kale, na aghalabu mwanzoni hata wanafunzi Wake wa karibu kabisa, hawawezi kuufahamu maana kamili ya Ufunuo Wake.

Wao huendelea kushikilia desturi na mazoea ya kidini ambayo vizazi vimeyafuata kwa mamia ya miaka. Ni baada tu ya muda kupita ndipo huelewa kwamba Mdhihirishaji mpya ameweka sheria mpya kwa ajili ya hatua inayofuata ya ukuaji wa jamii ya wanadamu.

Hivi ndivyo ilivyokuwa kuhusu Ufunuo wa Báb. Waislamu, ambao miongoni mwao Báb alitokea, waliamini kwamba hakuna hata "herufi" moja kutoka mafundisho ya Mtume Muhammad ingeweza kubadilishwa hadi mwisho wa ulimwengu. Kwa hiyo, Báb aliruhusu Ujumbe Wake kamili ujulikane tu hatua kwa hatua. Katika miaka ya mwanzoni ya Utume Wake, hakuna mabadiliko yoyote yaliyofanywa katika sheria za Uislamu. Lakini, kama mjuavyo, baadaye alipokuwa amefungwa katika ngome ya Máh-Kú, Báb alifunua seti mpya ya sheria katika Bayán ya Kiajemi. Sasa wakati ulikuwa umewadia kwa wafuasi Wake kuachana kabisa na ya kale na kutangaza Daraja Lake la kweli kama Mdhihirishaji wa Mungu. Hili lilifanyika katika Mkutano wa Badasht.

Badasht ni kijiji kilichopo mbali kidogo kutoka Ṭihrán katika kaskazini mashariki mwa nchi hiyo. Mkutano wa Badasht ulifanyika mwezi Julai 1848. Wafuasi themanini na mmoja mashuhuri kabisa wa Báb walikusanyika katika mkutanno huu. Washiriki wakuu walikuwa Bahá'u'lláh, Quddús na Ṭáhirih.

Ingawa Bahá'u'lláh tayari alikuwa anaheshimika sana na Wabábí wenzake, ambao walitambua ujuzi na hekima Yake na walimtazamia Yeye kwa ajili ya kupata mwongozo, katika mkutano huo ukuu na utukufu Wake vilidhihirika kwa kiwango kikubwa zaidi. Kwa hakika, nafasi Yake pale ilikuwa ya mkataa. Yeye alikodi bustani ambamo mkutano huo ulifanyika, na kwa siku ishirini na mbili, wale wote waliokuwa wamekusanyika walifurahia ukarimu Wake mkubwa. Kila siku Bahá'u'lláh alifunua Waraka mmoja ili usomwe mbele ya kundi zima lililokusanyika. Kila mmoja alimpa jina jipya. Aliwapa Ṭáhirih na Quddús, majina ya heshima ambayo kwayo watafahamika katika historia nzima. Jina la heshima Ṭáhirih humaanisha "Yule Msafi", na Quddús humaanisha "Mtakatifu". Yeye Mwenyewe, tangu wakati ule na kuendelea, atajulikana kwa jina la Bahá. Baadaye Báb alifunua Waraka maalum kwa kila mmoja miongoni mwa wale ambao walikuwa wamehudhuria mkutano huo, akiwaita kwa majina ambayo walikuwa wameyapokea kwenye tukio hilo.

Siku moja Bahá'u'lláh hakuweza kutoka kitandani Mwake kutokana na ugomjwa, na kila mmoja alikusanyika mbele Yake. Ndipo, ghafla, Ṭáhirih, ambaye alionekana kuwa kiini cha usafi na ubikira, alitokea mbele yao bila ushungi ambapo, kwa mujibu wa itikadi za Kiislamu huko Iran, wanawake wote iliwabidi wavae hadharani. Baadhi ya Wabábí waliokuwepo waliona kwamba alikuwa amejiaibisha mwenyewe na Imani yao changa. Quddús alionekana kughadhibishwa wazi wazi. Lakini Ṭáhirih, bila kutetereka na aking'aa kwa furaha, aliwahutubia wenzi wake kwa ufasaha. Aliwasihi kuachana na yaliyopita—pamoja na itikadi zake za kidini, mila na taratibu zake. Mvutano uliotokea kati ya Quddús na Ṭáhirih ulitulizwa kwa uingiliaji kati wa Bahá'u'lláh. Wakati wachache wa wafuasi wa Báb waliiacha Imani kama matokeo ya tangazo hili, wengi walibakia imara na walijawa na shauku mpya. Bahá'u'lláh kwa umahiri alilitumia tukio hilo kusherehekea mapambazuko ya Siku mpya. Ṭáhirih kwa kitendo chake cha ujasiri, alikuwa amepiga ile baragumu kutangaza mwisho wa Imani ya kale na mwanzo wa Imani mpya.

Mkutano wa Badasht pia uliashiria mwanzo wa hatua ya ghasia kubwa kabisa katika ukuaji wa Imani ya Kibábí. Punde mateso ya wafuasi Wake yangefikia viwango vipya vya ukali, na wengi wangeuawa kishuhidi. Ilikuwa kana kwamba ule mkutano ulikuwa mkusanyiko

wa kuagana, ambapo kutoka hapo wangekwenda kufanya vitendo vya ushujaa mkubwa, na kuungana tena tu katika milki za kiroho.

Wale waliokuwepo kwenye mkutano huo waliondoka pamoja kwenda Mázindarán. Walakini waliposimama kupumzika nje ya kijiji kimoja, walishambuliwa na wakazi wa kijiji hicho ambao hawakujua dhamira zao za kweli. Wabábí walilazimika kukimbia na kutawanyika sehemu mbali mbali. Bahá'u'lláh aliendelea na safari Yake kuelekea Núr huko Mázindarán.

Habari za Mkutano wa Badasht punde zilifika Ṭihrán, na mfalme na mawaziri wake walikuja kufahamu matukio yaliyofanyika na nafasi ambayo Bahá'u'lláh alikuwa nayo katika mkutano huo. Mfalme, ambaye alikuwa dhaifu kutokana na maradhi ambayo punde yangechukua maisha yake, alishauriwa na waziri mkuu aamuru kukamatwa kwa Bahá'u'lláh. Hivyo, amri ilipelekwa kwa mmojawapo wa maafisa wa Mázindarán, ikimuagiza kumkamata Bahá'u'lláh na kumleta katika mji mkuu. Ilitokea kwamba, ile amri ilifika siku moja kabla afisa huyo huyo alikuwa amkaribishe na kumfanyia tafrija Bahá'u'lláh ambaye alikuwa anampenda sana. Alifadhaika sana na aliamua kutomwambia yeyote. Siku iliyofuata habari zilifika huko Mázindarán kwamba mfalme alikuwa amefariki; amri ya kumkamata ikawa sio halali tena.

1. Mkutano wa Badasht ulikuwa na kusudi gani? ______________________________

   ______________________________________________________________

2. Mkutano wa Badasht ulifanyika lini? ______________________________

3. Mkutano wa Badasht ulidumu kwa siku ngapia? ______________________________

4. Wafuasi wangapi wa Báb walihudhuria mkutano huo? ______________________

5. Nani walikuwa washiriki wakuu? ______________________________

   ______________________________________________________________

6. Nani alikuwa Mtu muhimu kabisa miongoni mwa wale waliokuwepo? ___________

7. Jina "Ṭáhirih" lina maana gani? ______________________________

8. Jina "Quddús" lina maana gani? ______________________________

9. Kwa maneno yako mwenyewe, simulia matukio yaliyotokea siku ambayo Ṭáhirih alijitokeza bila ushungi katika ule mkutano.

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

   ______________________________________________________________

10. Kitendo cha kishujaa cha Ṭáhirih katika ule mkutano kiliashiria nini? ___________

11. Serikali ilifanya nini ilipata habari za ule mkusanyiko huko Badasht? ____________

12. Eleza nini kilitokea baada ya serikali kutoa amri ya kukamatwa kwa Bahá'u'lláh.

## SEHEMU YA 8

Mkutano wa Badasht uliashiria kuambuka kwa mambo ya zamani na kuanza kwa mapya. Kifungu kinachofuata kutoka Maandiko ya 'Abdu'l-Bahá kinaelezea jinsi, wakati hadi wakati tangu zama, dini ya Mungu inavyopaswa kuhuishwa. Tafakari juu ya maana ya kifungu hiki kulingana na yale ambayo umekwisha jifunza juu ya Mkutano wa Badasht.

> **"Kutoka mbegu ya uhalisia dini hukua hadi kuwa mti ambao hupata majani na matawi, maua na matunda. Baada ya muda mti huu hufikia katika hali ya kuoza. Majani, na maua hunyauka na kuharibika; mti huwa dhaifu na usio na matunda. Si busara kwamba mtu ashikilie mti wa zamani, akidai kwamba nguvu zake za uhai hazipungui, matunda yake hayana kifani, uhai wake ni wa milele. Mbegu ya uhalisia lazima ipandwe tena katika mioyo ya watu ili kwamba mti mpya uweze kukua humo na matunda mapya matakatifu yauburudishe ulimwengu. Kwa njia hii mataifa na watu wanaotofautiana katika dini sasa wataletwa katika umoja, uigaji utaachwa, na udugu wa wote katika uhalisia wake wenyewe utaanzishwa. Mambo ya vita na ugomvi yatakoma miongoni mwa jamii ya wanadamu; wote watapatana kama watumishi wa Mungu. Kwa kuwa wote wanahifadhiwa chini ya**

**mti wa majaliwa na rehema Yake. Mungu ni mwema kwa wote; Yeye ni Mtoaji wa baraka kwa wote sawa sawa, kama vile Yesu Kristo alivyotamka kwamba Mungu 'hutuma mvua kwa wenye haki na wasio na haki'—ndio kusema kwamba, rehema ya Mungu ni ya wote. Jamii nzima ya binadamu ipo chini ya ulinzi wa upendo na fadhili Yake, na kwa wote ameonesha njia ya uongozi na maendeleo."[22]**

## SEHEMU YA 9

Náṣiri'd-Dín Sháh, mfalme aliyekalia kiti cha enzi mnamo 1848, alikuwa katili zaidi kuliko baba yake, mfalme aliyetangulia. Tangu mwanzo wa utawala wake, mateso ya Wabábí yaliongezeka mno. Báb Mwenyewe aliuawa kishahidi mnamo Julai 1850 huko Tabríz. Wafuasi Wake waliodhulumiwa, ambao walishuhudia vifo vya huzuni vya maelfu ya waumini wenzao, sasa walikuwa wamempoteza Mpendwa kabisa wa mioyo yao. Katika fikra zao, wengi walimlaumu mfalme kutokana na ukatili uliolundikwa juu yao kwa miaka mingi iliyopita. Lakini licha ya hisia hizi, waliendelea kuwa watakia mema wa serikali na watu. Nguvu zao zilielekezwa kwenye kueneza Imani mpya kupitia nguvu za matendo mema na hoja za kusadikisha. Kulikuwepo, walakini, kikundi kidogo, kilichosukumwa na hasira kali, ambacho kilikuwa kikitawaliwa na mawazo ya hatari. Katika hali ya kukata tamaa, hawa wapumbavu wachache waliamini kwamba wangeweza kubadilisha hatma ya jamii ya Kibábí kwa kuushambulia udhalimu kwenye mzizi wake. Walianza kupanga njama za kumuua Mfalme.

Dhamira za kikundi hicho ziliwasilishwa kwa Bahá'u'lláh na mmoja wa viongozi wake. Bahá'u'lláh alimshauri kwa maneno ya wazi kabisa kwamba waachane na mpango wao huo. Aliwaonya kwamba kitendo kama hicho kingeleta maafa mapya kwa wafuasi wa Báb ambao tayari walikuwa wamejawa na huzuni. Lakini wale wapanga-njama walikuwa katika hali ya uchungu mkubwa, na moto wa kulipiza kisasi ulichaga mno mioyoni mwao, kiasi kwamba hata nasaha za Bahá'u'lláh hazikuweza kuwazuia. Wao waliendelea kufanya kitendo ambacho daima kitafikiriwa kuwa doa kwenye kurasa za historia ya Kibábí, vinginevyo isipambwe kwa chochote bali kwa matendo safi, yasiyo na ubinafsi na ya kishujaa.

Tarehe 15 Augusti 1852, mfalme aliyaacha makazi yake ya majira ya joto karibu na Ṭihrán akiwa amepanda farasi kwenda katika matembezi yake ya asubuhi. Mlinzi wake binafsi alitembea hatua chache mbele yake, hali ya hewa ilikuwa tulivu, na mambo yote yalikuwa shwari. Halafu, akimshangaza kila mmoja, kijana mmoja, aliyekuwa akingojea kando ya barabara akijifanya kuwa mtazamaji mwenye ombi kwa Mfalme, alijaribu kumuua. Mtu huyu alikuwa mpumbavu mno kiasi kwamba bastola aliyotumia ilikuwa na risasi ndogo ambazo zilikuwa hazifai kabisa kwa kusudi alilodhamiria. Mfalme alijeruhiwa kidogo tu, lakini ghadhabu iliyosababishwa na jaribio juu ya maisha yake iliwapa maadui wa Imani fursa ya kuwachochea watu kufanya vitendo vya ukatili visivyofikirika dhidi ya Wabábí.

Kijana huyu mwenye nuksi aliuawa papo hapo; mwili wake ulifungwa kwenye mkia wa nyumbu na kukokotwa hadi Ṭihrán, ambako ulikatwa vipande viwili na kuning'inizwa kwa ajili ya umma kuuona. Risasi iliyoyeyushwa ilimiminwa ndani ya koo la mshirika wake—hii ilikuwa tu baada ya kuteswa kwanza kikatili, na bado akakataa kutoa majina ya yeyote kati ya marafiki zake. Sahibu wake alivuliwa nguo zake, mishumaa iliyowashwa iliwekwa ndani ya matundu yaliyotobolewa kwenye mwili wake, na akatembezwa mbele ya umati wa watu ambao walimzomea na kumlaani.

Kilichofuata hakiwezi kuelezeka. Serikali, makasisi, na wasaidizi wao wajinga waliinuka kuwaangamiza Wabábí. Malango ya kuingilia mjini yalifungwa, na hakuna aliyeruhusiwa kuondoka bila kuhojiwa. Wabábí walisakwa nyumba hadi nyumba, wakakamatwa na kuuawa kwa ukatili wa kutisha mno kiasi kwamba hauwezi kuelezwa katika kurasa hizi.

Siku ile lilipofanyika jaribio dhidi ya maisha ya mfalme, Bahá'u'lláh alikuwa mgeni wa ndugu wa waziri mkuu katika kijiji jirani na Ṭihrán. Habari za janga hili punde zilimfikia, na alishauriwa ajifiche hadi hapo dhoruba itakapopita. Mama yake mfalme alimlaumu Bahá'u'lláh kwa jaribio dhidi ya maisha ya mwanae na alitaka akamatwe. Lakini Bahá'u'lláh alikataa kwenda kujificha; badala yake, siku iliyofuata, alipanda farasi Wake na kuelekea kwenye makao makuu ya mfalme. Mfalme na baraza lake walishangazwa walipojua juu ya kukaribia kwa Bahá'u'lláh. Ingewezekanaje kwa mtu anayetuhumiwa kwa kosa la kutisha kama hilo, badala ya kukimbilia mbali, apande farasi kwa kujiamini, na kuelekea kwenye hatari? Mfalme mara moja aliamuru kukamatwa kwa Bahá'u'lláh. Jitihada za baadhi ya marafiki Zake ambao walijaribu kumpatia hifadhi katika nyumba ya waziri mkuu zilishindikana. Alikamatwa katika kijiji cha Shimírán, kama kilometa 30 hivi kutoka mji mkuu, na alifungwa kwa minyororo.

Akitembea kwa miguu na akichomwa na mionzi mikali ya jua la katikati ya kiangazi, Bahá'u'lláh aliletwa kutoka Shimírán hadi Ṭihrán. Makundi yaliyokuwa yameambiwa kwamba Yeye alikuwa adui wa mfalme wao, yalimrushia matusi njia nzima. Kisa cha yule ajuza aliyetamani kumtupia jiwe Bahá'u'lláh, kinatoa picha ya hasira kali ya ule umati siku hiyo na huonesha upendo uliokuwa ndani ya moyo Wake alipokuwa anakabiliana na maafa ya kuhuzunisha kabisa.

Bahá'u'lláh alipokuwa analikaribia gereza lililokuwa chini ya ardhi ambako angefungwa, yule ajuza mnyonge alijipenyeza katikati ya ule umati akiwa na jiwe mkononi mwake. Alionekana kuwa mwenye dhamira na msimamo mkali ambao ni wanawake wachache tu wa rika lake wangeweza kuthubutu kuwa nao. Mwili wake wote ulitetemeka kwa ghadhabu. Alisonga mbele na kuinua mkono wake akijitayarisha kutupa lile jiwe. "Nawaomba," aliwasihi, wakati akiwakimbilia wale ambao walikuwa wakimpeleka Bahá'u'lláh kwenye gereza hilo, "nipeni nafasi nimpige jiwe usoni!" "Msimfanye mwanamke huyu avunjke moyo," yalikuwa maneno ya Bahá'u'lláh kwa walinzi Wake, alipomuona akimkimbilia. "Msimkataze kile anachofikiri kama kitendo kistahilicho sifa machoni pa Mungu."[23]

1. Mfalme aliyekalia kiti cha enzi mnamo 1848 aliitwa nani? ____________________

______________________________________________________________________

2. Kukalia kiti cha enzi kwa Náṣiri'd-Dín Sháh kulikuwa na athari gani juu ya vitendo walivyofanyiwa Wabábí? ______________________________________________

______________________________________________________________________

3. Wabábí walijihisije kwa jumla baada ya kifo cha kishahidi cha Báb? ____________

______________________________________________________________________

4. Kundi lililokuwa limedhamiria kumuua mfalme lilikuwa katika hali gani kiakili? __

5. Bahá'u'lláh alimwambia nini yule kiongozi wa kikundi hicho pindi alipojua dhamira zao? ______

6. Jaribio la maisha ya mfalme lilitokea tarehe ngapi? ______

7. Nini hatma ya wale waliodiriki kufanya mauaji hayo? ______

8. Lile jaribio la mauaji lilikuwa na matokeo gani kwa jumuiya ya Wabábí?

9. Bahá'u'lláh alikuwa wapi alipopata habari za jaribio dhidi ya maisha ya mfalme?

10. Bahá'u'lláh alifanya nini baada ya kupokea habari za jaribio la mauaji hayo? ______

11. Bahá'u'lláh alikamatwa katika kijiji gani? ______

12. Maadam Bahá’u’lláh hakuwa mnyonge mbele ya maadui Zake, kwa nini basi unafikiri Alijiruhusu kukamatwa, ilhali akijua hatari aliyokuwa akienda kukutana nayo? ____

13. Katika hali zipi Bahá’u’lláh aliletwa kutoka Shimírán hadi Ṭehrán? ______________

14. Kwa maneno yako mwenyewe, kisa cha yule ajuza aliyetaka kumtupia jiwe Bahá’u’lláh alipokuwa akiopelekwa na walinzi kwenye lile gereza la shimoni. Kisa hiki hutufunza nini?

## SEHEMU YA 10

Katika maisha Yake yote, Bahá’u’lláh alizungukwa na maadui wakitaka kumdhuru. Lakini kamwe Yeye hakujaribu kujificha; kamwe hakujilinda. Kinyume chake, wakati wote Yeye alikuwa akionekana mbele ya macho ya watu na aliyahimili kwa utulivu na amani mashabulio ya wale waliompinga. Ingawa walidhamiria kuuzima mwanga Wake, walishindwa kufanya hivyo, na siku hadi siku utukufu Wake ulizidi kuwa mwangavu.

> **"Hata kwa kitambo kidogo Mdhulimiwa huyu kamwe hakuwahi kujificha. Bali wakati wote Yeye alibakia thabiti na kuonekana mbele ya macho ya watu wote. Kamwe hatutarudi nyuma, wala hatutatafuta kimbilio. Kwa ukweli ni wale watu wapumbavu ndio hukimbia kutoka machoni Petu. . . Sifa ziwe kwa Mungu! Hoja ambayo Mdhulumiwa huyu ni Mchukuzi wake husimama juu mno kama mbingu na hung'aa kwa wangavu kama jua. Maficho hayana nafasi katika daraja hili, wala nafasi kwa ajili ya hofu au ukimya."[24]**

> **"Akiwa wazi na bila kujificha, Mdhulumiwa huyu, nyakati zote, ametangaza mbele ya watu wote wa ulimwengu kile ambacho kitasaidia kama ufunguo wa kufungua milango ya sayansi, ya sanaa, ya elimu, ya hali njema, ya ustawi na ukwasi. Si maovu aliyotendewa na wadhalimu yalifanikiwa kuinyamazisha sauti kali ya Kalamu Iliyotukuka Kabisa, wala mashaka ya wapotovu au ya wachochezi yaliweza kumzuia Yeye kufunua Neno Lililotukuka Kabisa."[25]**

Elezea kwa maneno yako mwenyewe jinsi tunavyopaswa kuwa mbele ya majaribu tunapofanya kazi ya kuilinda Hoja ya Bahá'u'lláh.

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 11

Síyáh-Chál, jina la gereza ambako Bahá'u'lláh alipelekwa siku ile ya maafa mnamo 1852, humaanisha "shimo jeusi". Mwanzoni lilikuwa shimo la maji taka kwa ajili ya mojawapo ya mahamamu huko Ṭihrán, wakati huo lilikuwa gereza la ardhini ambamo wahalifu wabaya kabisa walifungwa.

Ili kulifikia gereza hilo, mtu ilibidi apitishwe katika njia nyembamba yenye giza totoro na kisha kushuka ngazi tatu za wima. Likiwa limetandwa na giza totoro, lilikuwa la baridi mithili ya barafu, na sakafu ilifunikwa kwa uchafu na wadudu wanaotambaa. Bahá'u'lláh Mwenyewe huelezea hali mbaya sana ya mahali hapo alikokuwa amefungwa:

> **"Tulipowasili, kwanza Tulipitishwa kwenye ushoroba mwembamba wenye giza totoro kutoka hapo Tukashuka ngazi tatu za wima hadi tukafika mahali pa kifungo tulipokuwa Tumepangiwa. Shimo hilo lilikuwa limetandwa na giza totoro, kukiwa na wafungwa wenzetu takriban roho mia moja na hamsini: wezi, wauaji na maharamia. Ingawa tulisongamana shimo hilo halikuwa na pa kutokea isipokuwa ile njia Tuliyoitumia kuingia. Hakuna kalamu iwezayo kufafanua hali ya mahali pale, wala ulimi wowote uwezao kuelezea harufu yake ya kukirihisha.**

**Wengi wa watu hawa, hawakuwa na nguo wala matandiko ya kulalia. Mungu pekee ndiye ajuaye kilichotusibu ndani ya mahali pale pananukapo na pa kuhuzunisha kabisa!”[26]**

Katika mazingira haya ya kikatili, Bahá’u’lláh na Wabábí kadhaa walifungwa na mfalme. Miguu ya Bahá’u’lláh iliwekwa ndani ya kiunzi cha miti na mnyororo mzito wenye takriban kilo 50 ulizungushiwa shingoni Mwake. Kwa siku tatu za kwanza usiku na mchana hawakupewa chochote cha kula au kunywa. Familia ya Bahá’u’lláh iliandaa chakula kwa ajili Yake na kuwaomba wale walinzi wampelekee. Ingawa mwanzoni walikataa, hatimaye walikubali maombi yao. Lakini, hata baada ya hayo, hakuna aliyeweza kuwa na hakika kwamba chakula hicho kilimfikia au kama angekubali kukila wakati wafungwa Wenzake wakiwa na njaa.

Bahá’u’lláh na Wenzake, pia wakiwa katika viunzi vya miti na minyororo, wote walibanana katika chumba kimoja kidogo. Walikuwa wamewekwa katika safu mbili, zikitazamana. Bahá’u’lláh aliwafundisha kukariri baadhi ya aya ambazo, kila usiku, waliziimba kwa juhudi kubwa. “Mungu hunitosheleza; Yeye kwa kweli ni Mtosheleza—Vyote,” safu moja iliimba, na nyingine iliitikia: “Kwake Yeye acha waaminio waamini.” Mapema alfajiri, kibwagizo cha sauti zao zenye furaha kiliweza kusikika. Sauti ya uimbaji wao ilikuwa yenye nguvu mno kiasi kwamba iliyafikia masikio ya mfalme, ambaye jumba lake halikuwa mbali kutoka Síyáh-Chál. “Sauti hii ina maana gani?” ilitaarifiwa kuwa aliuliza. “Ni wimbo ambao Wabábí wanaimba gerezani mwao, lilikuwa jibu,”[27] Mfalme akanyamaza.

Kila siku, askari magereza waliingia katika chumba cha gereza na kuita jina la mmoja wa Wabábí, wakimuamuru kuinuka na kuwafuata hadi chini ya kiunzi cha kunyongea. Kwa shauku kubwa, yule mwenye jina hilo aliitikia wito huo! Minyororo yake ikiwa imeondolewa, aliruka na, katika hali ya furaha isiyozuilika, alimsogelea Bahá’u’lláh na kumkumbatia. Halafu alimkumbatia kila mmoja wa wafungwa wenzake na kwenda, kwa moyo uliojawa na matumaini na furaha, kukutana na kifo kilichokuwa kinamsubiri. Mara baada ya kifo cha kishahidi cha kila moja ya roho hizi shujaa, yule muuaji, ambaye alitokea kumpenda Bahá’u’lláh alimwendea na kumjulisha juu ya hali ya kifo cha shahidi huyo, na juu ya furaha aliyoionesha hadi mwisho kabisa na maumivu aliyoyapata.

1. Gereza ambamo Bahá’u’lláh alifungiwa liliitwaje? ____________________________

   ____________________________________________________________

2. Nini maana ya “Síyáh-Chál”? ____________________________________

3. Mwanzoni Síyáh-Chál ilitumika kwa kazi gani? ______________________

   ____________________________________________________________

4. Elezea hali ya Síyáh-Chál.

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

5. Baada ya kuwasili huko Síyáh-Chál kitu gani kilikuwa kimezungushiwa shingoni mwa Bahá'u'lláh?

6. Nini kiliibana miguuni Mwake?

7. Bahá'u'lláh na wenzi Wake waliwekwaje katika chumba chao cha gereza?

8. Bahá'u'lláh aliwafundisha kufanya nini?

9. Je, safu moja ya Wabábí iliimba nini usiku kucha?

10. Safu nyingine iliitikiaje?

11. Je, kuimba kwao kulikuwa na matokeo gani juu ya mfalme?

12. Kila siku wale askari magereza walikuja kwenye chumba ambako Bahá'u'lláh na wenzi Wake walifungwa na kuita jina la mmoja wa Wabábí. Kwa maneno yako mwenyewe, elezea nini kilitokea baada ya hapo.

13. Kwa nini unafikiri Wabábí walikuwa wenye furaha licha ya hali mbaya sana ya kifungo chao?

## SEHEMU YA 12

Kuna dhana ya kina sana ambayo kila mwanafunzi wa historia ya Kibahá'í sharti aifahamu, yaani, kwamba Hoja ya Mungu huendelea mbele kupitia mfululizo wa hali ya hatari na ushindi. Pale nguvu za ujinga, udhalimu, ukatili na ushupabu wa kidini inapoishambulia Hoja, zikisababisha hatari, kiwango kinachoshabihiana cha uwezo wake wa kiasili huachiliwa, na kuzishinda nguvu hizo, na ukiipeleka mbele Hoja kupata ushindi mpya, ambao papo hapo au baadaye husababisha upinzani mpya ambao haukuwahi kufikiriwa hapo kabla, ambao husaidia, kwa mara nyingine tena, uachiliwaji wa kiwango kingine zaidi cha uwezo wake Mtakatifu. Hivyo ndivyo Hoja ya Mungu inavyojongea kutoka hali ya hatari hadi ushindi na tena hali ya hatari na tena ushindi, na hakuna nguvu duniani inayoweza kuzuia mwendo wake.

Kipindi kifupi cha Utumishi wa Báb tayari kilikuwa kimeifuata njia kama hiyo. Walakini mchunguzi wa kawaida angedhani kwamba hali ya hatari ya wakati huu isingeweza kushindika: Báb alikuwa amekwishauawa kishahidi. Maelfu ya wafuasi Wake walikuwa wamekwishauawa kwa mauaji ya kinyama. Wanafunzi Wake bora kabisa walikuwa ameshauawa kishahidi na Yule pekee Ambaye angeweza kufufua matumaini alikuwa kwenye minyororo katika gereza lenye giza kabisa. Kwa hakika hatari ilikuwa kubwa mno, lakini ule ushindi uliofuata ulikuwa mtukufu kabisa.

Ndani ya Síyáh-Chál, Mungu alimjulisha Bahá'u'lláh ukuu wa Daraja Lake. Akiwa amegubiikwa na utusitusi, akivuta hewa mbaya kabisa, miguu Yake ikiwa katika viunzi na shingo Yake ikielemewa na mnyororo mkubwa kabisa, Bahá'u'lláh alipokea wito wa kwanza wa ufunuo wa Mungu ndani ya roho Yake. Katika hali hizi za kutisha, yule "Roho Mkuu Kabisa" alijifunua mwenyewe Kwake, akimuamuru kuinuka na kunena wazi Neno la Mungu.

Kwa wakati huo, Yeye alihisi kama vile kitu fulani kikitiririka kutoka utosi wa kichwa Chake hadi kifuani Mwake, kama vile maporomoko yenye nguvu yanavyoanguka juu ya ardhi kutoka kilele cha mlima mrefu. Yeye Alimuona Mwanamwali wa Mbinguni akining'inia mbele Yake, akizungumza na nafsi Yake ya ndani na ya nje, akimtaja Yeye kama Mpendwa sana wa malimwengu, Uzuri wa Mungu, na nguvu ya enzi ya Mungu. Alihakikishiwa kwamba atafanywa mshindi kwa Yeye Mwenyewe na kwa Kalamu Yake, na kwa msaada wa wale ambao Mungu atawainua.

Hivyo kutoka katika giza la Shimo Jeusi lilichomoza Jua la Ukweli. Ahadi ya Báb ilikuwa imetimizwa. Ufunuo wa Kibahá'í ulizaliwa. Lakini Bahá'u'lláh hakumfahamisha

yeyote juu ya kile kilichokuwa kimetokea. Yeye alisubiri saa iliyopangwa, iliyoamriwa na Mungu, kuufanya Ujumbe Wake ujulikane.

1. Eleza kwa maneno yako mwenyewe jinsi hali ya hatari ilivyokuwa mbaya ambamo Jumuiya ya Kibábí ilijikuta wakati wa kifungo cha Bahá'u'lláh.

____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________

2. Ni ushindi gani ambao ulifuata baada ya hatari hii kubwa kabisa? ________________

____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________
____________________________________________________________

## SEHEMU YA 13

Jamii ya wanadamu ina bahati ya kupata tukio hili la maana mno katika historia ya dini lililooandikwa kwa maneno ya Bahá'u'lláh Mwenyewe. Someni vifungu kutoka kwenye Maandiko Yake hapo chini na jazeni nafasi katika sentensi zinazofuata kila kimoja.

Akikumbuka jinsi Ufunuo wa Mungu ulivyoijaza kwanza roho Yake, Bahá'u'lláh husema:

> **"Usiku mmoja, katika ndoto, maneno haya yaliyotukuka yalisikika kila upande: 'Kwa kweli, Tutakufanya mshindi kwa Wewe Mwenyewe na kwa Kalamu Yako. Usihuzunike kwa yale yaliyokupata, wala usiogope, kwa kuwa Wewe u katika usalama. Hivi punde Mungu atainua hazina za dunia – watu ambao watakusaidia Wewe kupitia Wewe Mwenyewe na kupitia Jina Lako, ambalo kwalo Mungu ameihuisha mioyo ya wale ambao wamemtambua Yeye.'"**[28]

Katika kifungu hiki, Bahá'u'lláh hutuambia kwamba Usiku mmoja, katika ndoto, maneno haya yaliyotukuka yalisikika kila upande: "Kwa kweli, Tutakufanya ______________ kwa _____________ Mwenyewe na kwa ________________ Yako. Usihuzunike kwa yale ________________ , wala _____________ , kwa kuwa Wewe u ___________________ . Hivi punde Mungu ___________________________ za dunia – ___________ ambao watakusaidia Wewe kupitia ________________________ na kupitia ___________________ , ambalo kwalo Mungu __________________ mioyo ya wale ambao ____________________ Yeye."

Katika kifungu kingine Bahá'u'lláh huelezea athari ya Ufunuo wa Mungu kwenye nafsi Yake:

> **"Katika siku zile nilipokuwa ndani ya gereza la Tihrán, ingawa uzito wa kuumiza wa minyororo, na hewa iliyojaa harufu mbaya vilinipa usingizi kidogo tu, hata hivyo katika vile vipindi vya usingizi wa mang'amung'amu, nilihisi kama vile kitu fulani kikitiririka kutoka utosi wa kichwa Changu hadi kifuani Mwangu, kama vile maporomoko yenye nguvu yanavyoanguka juu ya ardhi kutoka kilele cha mlima mrefu. Kila kiungo cha mwili Wangu, matokeo yake, kiliwashwa moto. Wakati huo ulimi Wangu ulitongoa yale ambayo hakuna mtu angeweza kustahimilifu kuyasikia."[29]**

Bahá'u'lláh husema kwamba, katika siku zile alipokuwa ndani ya _________ la Ṭihrán, ingawa ________________________ wa ____________ , na ____________________________ vilimpa ____________ kidogo tu, ingawa alisinzia kidogo hata hivyo katika vile vipindi vya ____________________________ , Alihisi kama vile ________________________ kutoka ____________ wa ____________________ hadi ____________ Mwake. Matokeo yake, kila kiungo cha mwili Wake ____________________ . Wakati huo Bahá'u'lláh alitongoa yale ambayo ____________________________________________________________ .

Tena katika kifungu kingine Yeye anaelezea jinsi Mwanamwali, akiashiria "Roho Mkuu Kabisa," alivyomtokea:

> **"Nikiwa Nimezingirwa na taabu Nilisikia sauti nzuri kabisa, ya ajabu kabisa, ikiita juu ya kichwa Changu. Nikigeuza uso Wangu, Nilimuona Mwanamwali—mfano halisi wa kumbukumbu ya jina la Bwana Wangu—akining'inia hewani mbele Yangu. Alikuwa mwenye furaha sana katika roho yake hasa kwamba wajihi wake uling'aa kwa pambo la ridhaa njema ya Mungu, na mashavu yake yalimeremeta kwa wangavu wa Mwenye—Rehema Kabisa. Kati ya mbingu na ardhi alikuwa akipaza wito ambao uliivutia mioyo na akili za watu. Alikuwa akiipasha nafsi Yangu ya ndani na ya nje habari njema ambazo ziliifurahisha roho Yangu, na roho za watumishi waheshimiwao wa Mungu. Akionesha kwa kidole chake kwenye kichwa Changu, yeye aliwaambia wote walioko mbinguni na wote waliopo duniani, akisema: 'Kwa Mungu! Huyu ndiye Mpendwa sana wa malimwengu, na bado hamfahamu. Huu ndio Uzuri wa Mungu miongoni mwenu, na uwezo wa enzi Yake ndani mwenu, laiti tu mngelielewa. Hili ndilo Fumbo la Mungu na Hazina**

**Yake, Hoja ya Mungu na utukufu Wake kwa wote walio katika falme za Ufunuo na za muumbo, laiti mngekuwa miongoni mwa wale wanaotambua.'"[30]**

Bahá'u'lláh anatuambia kwamba, Alipokuwa amezingirwa na taabu Yeye __________ ______________________________ , ______________________ , ikiita juu ya kichwa Chake. Alipogeuza uso Wake, Bahá'u'lláh alimuona Mwanamwali akining'inia ________________ ________________________ . Uso wa Mwanamwali __________________________ kwa _____________ la __________________________ ya _______________ , na mashavu yake yalimeremeta kwa _______________________ . Mwanamwali alikuwa akiipasha nafsi Yake ya ___________ na ya ___________ habari njema ambazo ziliifurahisha ______________ Yake, na roho za _______________________________ wa Mungu. Akionesha kidole chake kwenye kichwa cha Bahá'u'lláh, yeye aliwaambia maneno haya wote walioko ______________ na wote waliopo _________________________ , akisema: "Kwa Mungu! Huyu ndiye __________________________ wa ___________________ , na bado hamfahamu. Huu ndio ___________________________ miongoni mwenu, na ___________________________ ndani mwenu, laiti tu mngelielewa. Hili _______________________________ na ____________ Yake, _________________________ na ______________ Wake kwa wote walio katika falme za _____________ na za ____________ , laiti mngekuwa miongoni mwa wale wanaotambua."

## SEHEMU YA 14

Dhana ya hali ya hatari na ushindi ni ya muhimu sana kwamba inafaa kwako kusita hapa kidogo na kutafakari juu ya nguvu ya Hoja, ambayo inaweza kukishinda kila kizuizi katika njia yake. Ili kukusaidia kufanya hivyo, inapendekezwa kwamba usome nukuu hapo chini—moja kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh na nyingine kutoka barua iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi—na ujibu swali linalofuata.

> **"Tazama jinsi gani katika Kipindi hiki Kitakatifu wale wasiofaa na wajinga wamedhani kwa matumaini ya kijinga kwamba kwa njia kama vile mauaji ya kinyama, uporaji na uhamisho wanaweza kuizima Taa ambayo Mkono wa nguvu ya Mungu umeiwasha, au kuzuia mng'ao wa milele wa Nyota ya Mchana. Jinsi gani wanaonekana hawatambui kabisa ukweli huu kwamba mateso kama hayo ndio mafuta ambayo huchochea mwale wa Taa hii! Hiyo ndiyo nguvu ibadilishayo ya Mungu. Yeye hubadili chochote akipendacho; Yeye kwa kweli ana nguvu juu ya vitu vyote."[31]**

> **"Hoja hii, kama ilivyo kila Hoja Takatifu, haiwezi kusimikwa ipasavyo vinginevyo ikabiliane na kuzishinda kishujaa zile nguvu zote za upinzani zinazoishambulia. Historia ya Imani yenyewe ni uthibitisho tosha wa jambo hilo. Majaribu na mateso daima yamekuwa, na yataendelea kuwa, ndio fungu la wateule wa Mungu. Lakini haya, wao sharti wayachukulie kama baraka zilizofichwa, kwa kuwa kupitia hayo imani yao itahuishwa, kutakaswa na kuimarishwa. Bahá'u'lláh**

**hulinganisha majaribu yaumizayo kama haya na mafuta ambayo huchochea taa ya Hoja ya Mungu.”[32]**

Uelewa kwamba Imani huendelea mbele kupitia mfululizo wa hali ya hatari na ushindi utakusaidiaje wewe katika dhanira yako kutembea njia ya huduma kwa Hoja na kwa wanadamu?

## SEHEMU YA 15

Wakati Bahá’u’lláh akibakia kwenye minyororo huko Síyáh-Chál, maadui Zake walikuwa wakijishughulisha kupata hukumu Yake ya kifo kutoka kwa mfalme. Walakini, Bahá’u’lláh alipendwa na watu wakubwa kwa wadogo kadhalika na asingeweza kuuawa kirahisi. Ushahidi ulihitajika ambao ungemhusisha Yeye na jaribio dhidi ya maisha ya mfalme. Kadiri walivyoendelea kutafuta ushahidi, ndivyo ilivyokuwa dhahiri zaidi kwamba Yeye hakuwa na hatia kabisa. Waliposhindwa kupata hukumu ya mauaji Yake, maadui hawa katili waliamua kukitia sumu chakula Chake. Sumu hiyo ilikuwa kali mno, hata hivyo, kwamba matokeo yake ya mwanzoni yalitambuliwa kwa haraka na Bahá’u’lláh aliacha kula kile chakula. Hatimaye, mamlaka hazikuwa na chaguo lingine bali kumwachilia huru kutoka gerezani, walifanya hili kwa sharti tu kwamba aondoke nchini humo na kwenda uhamishoni.

Bahá’u’lláh alistahimili miezi minne gerezani. Sasa alikuwa mgonjwa na dhaifu. Hali za kinyama za lile gereza, mnyororo wa takriban kilo 50 uliozungushwa shingoni Mwake, na mwishowe ile sumu, vilimuacha katika hali ya kudhoofika kiasi kwamba aliendelea kuwa kitanda Mwake chini ya uangalizi makini. Zile tepe za mnyororo zilichimba na kusababisha vidonda shingoni Mwake, ingawa baada ya muda vilipona, makovu yalibakia hadi mwisho wa uhai Wake. Katikati ya yote haya, familia Yake ililazimika kujiandaa kwa ajili ya safari ngumu ndani ya muda wa mwezi mmoja. Bahá’u’lláh alikuwa amepewa uhuru kuchagua mahali pa uhamisho Wake. Yeye alichagua Baghdád, wakati huo ulikuwa mji katika Himaya ya Ottoman na leo ni mji mkuu wa ‘Iráq.

Safari hiyo ilianza 12 Januari 1853 hadi 8 Aprili ya mwaka huo huo. Ilikuwa katikati ya majira ya baridi, na Bahá’u’lláh na familia Yake walilazimika kusafiri kupitia magharibi mwa Iran ambapo nyakati za kipupwe huwa baridi hasa. Vyakula walivyokuwa navyo kwa ajili ya safari havikutosha, na iliwalazimu kuridhika na chakula kidogo. Lakini kikundi hiki kidogo

cha wasafiri kililindwa na Mwenyezi Mungu Mwenyewe, na kwa kupitia msaada Wake usioshindwa, waliwasili huko Baghdád salama salimini.

Iran ilikuwa imejinyima yenyewe baraka ya kuwepo kwa Bahá'u'lláh na ilimshurutisha kuondoka, na kamwe kutorudi tena katika nchi Yake ya kuzaliwa. 'Iráq sasa ilibidi iwe maskani kwa ile Nafsi yenye thamini kabisa juu ya sayari. Mwanahistoria mashuhuri wa Kibahá'í ana maneno haya ya kusema kuhusu uhamisho wa Bahá'u'lláh kutoka Iran:

> "Kadiri Bahá'u'lláh alivyokaribia mpakani, kipindi kimoja kilifikia tamati yake. Je, watu wa Iran walitambua hasara waliyoipata? Wakiwa wamebobea katika ujinga, wakididimia katika ushupavu wa kidini, wakipofushwa na ubaguzi, wakiongozwa na watu wenye ubinafsi wa kujinufaisha, wakighilibiwa na uwongo, hali yao ilikuwa sio kuona na kutambua. Na hivyo ndivyo Mkombozi wa ulimwengu alivyoondoka miongoni mwao. Yule Ambaye wakati fulani alipendwa na kuheshimiwa na matajiri kwa masikini, wa daraja la juu na la chini, mwana mfalme kwa mkulima kadhalika hivi sasa alitelekezwa na watu wale wale ambao wakati wote Yeye aliwakarimu kwa rehema tele, upendo, haki na hisani mno. Iran ilipoteza kuwepo kwa Bahá'u'lláh, lakini je, roho Yake ingeweza kukosa kuwepo katika nchi hiyo au katika nchi nyingine yoyote?"[33]

1. Kwa nini maadui wa Bahá'u'lláh walishindwa kupata hukumu ya kifo Chake? ____

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

2. Maadui wa Bahá'u'lláh hawakufanikiwa katika njama zao kumhusisha Yeye na jaribio dhidi ya maisha ya mfalme. Kisha walifanya nini? ____________________

_______________________________________________

_______________________________________________

3. Ni kwa miezi mingapi Bahá'u'lláh alikuwa ndani ya Síyáh-Chál? ____________

4. Aliachiliwa kwa masharti gani? ______________________________

_______________________________________________

5. Bahá'u'lláh alichagua mji gani kama mahali pa uhamisho Wake? ____________

6. Wakati ule mji wa Baghdád ulikuwa sehemu ya himaya gani? Sasa ni mji mkuu wa nchi gani? ________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

7. Bahá'u'lláh na familia Yake walianza safari yao ya kwenda Baghdád tarehe ngapi? Tarehe ngapi, takriban miezi mitatu baadaye, safari yao iliishia? ________________

________________________________________________________________

8. Elezea hali ya safari hiyo.

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

## SEHEMU YA 16

Sala ifuatayo iliyofunuliwa na Bahá'u'lláh inatupa kianga juu ya mateso Aliyoyapata huko Síyáh-Chál na taabu Alizozistahimili katika miezi kadhaa iliyofuatia baadaye kidogo.

> **"Mungu Wangu, Bwana Wangu, Haja Yangu! . . . Wewe umeumba atomu hii ya vumbi kupitia nguvu ikamilishayo ya uwezo Wako, na kumlea Yeye kwa mikono Yako ambayo hakuna awezayo kuifunga minyororo. . . . Wewe ulikusudia kwa ajili Yake majaribu na taabu ambazo hakuna ulimi uwezao kuelezea, wala yoyote ya Nyaraka Zako kusimulia ipasavyo. Koo ambalo Wewe umelizoesha mguso wa hariri, mwishowe, umelifumbatia kwa minyororo mizito, na mwili ambao uliustarehesha kwa zari na mahameli Wewe hatimaye umeufanya utwezwe ndani ya gereza la shimoni. Amri Yako imenifunga kwa pingu zisizohesabika, na kunitupia minyororo shingoni Mwangu ambayo hakuna awezaye kuikata. Miaka kadhaa imepita wakati ambamo mateso, kama vile manyunyu ya rehema, yameninyeshea. . . . Ni siku ngapi wakati ambamo uzito wa minyororo na pingu haukuniwezesha kupumzika, na ni nyingi jinsi gani siku ambamo nimenyimwa amani na utulivu, kwa sababu ya kile ambacho kwacho mikono na ndimi za watu imenitesa! Vyote viwili mkate na maji ambavyo Wewe, kupitia rehema Yako ikumbatiayo vyote, umeviruhusu kwa wanyama wa kondeni, kwa muda, mtumishi huyu alinyimwa, na mambo ambayo wamekataa kuwafanyia wale ambao wamejiondoa kutoka Hoja Yako, hayo hayo wameruhusu nifanyiwe Mimi, hadi, hatimaye, amri Yako isiyoweza kutanguliwa, na amri Yako yenye mamlaka ilipompa wito mtumishi huyu kuondoka Uajemi, akiambatana na watu kadhaa wenye miili dhaifu na watoto wenye umri mchanga, katika kipindi ambamo baridi ni kali mno kiasi kwamba mtu hawezi hata kuongea, na barafu na theluji ni nyingi mno kiasi kwamba haiwezekani kusogea."**[34]

Pengine ungependa kukariri sala hiyo hapo juu. Lakini hata kama unaisoma mara kadhaa, baadhi ya maelezo kuhusu mateso ya Bahá'u'lláh yataingia akilini mwako. Ni yapi baadhi ya maelezo haya?

## SEHEMU YA 17

Huko Baghdád, Bahá'u'lláh alikodi nyumba katika mtaa wa zamani wa mji huo. Miezi kadhaa baada ya kuwasili Kwake, idadi iliyokuwa inaongezeka ya Wabábí walikwenda Baghdád. Kwa bahati mbaya, wengi walikuwa wamekwishazama katika hali ya kutia huruma; walikuwa wamechanganyikiwa na kufadhaishwa, na baadhi walikuwa wakifanya vitendo visivyostahili kwa mfuasi wa Báb. Bahá'u'lláh aliwapokea wale wote waliowasili kwa upendo mkubwa mno na aliwasaidia kutakasa mioyo yao na kuhuisha roho zao. Chini ya ushawishi Wake, ustawi wa jamii ya Kibábí ulianza kubadilika na matumaini yalichanua tena. Lakini ole, hali ya hatari tena ilikuwa inanyemelea. Wakati huu chanzo chake kilikuwa ndani ya jumuiya yenyewe; chanzo cha balaa hilo hakuwa mwingine ila ndugu wa kambo wa Bahá'u'lláh Mwenyewe, Mírzá Yaḥyá, ambaye alidai kuwa mrithi wa Báb.

Kwa kweli, Báb hakuona haja ya kumtaja mrithi, kwa kuwa Yeye alijua fika kwamba yule Mwahidiwa wa Zama Zote punde tu angetokea. Alichokuwa amefanya kutokana na ushauri wa Bahá'u'lláh na mfuasi mmoja mwaminifu, ni kumteua Mírzá Yaḥyá, kama mkubwa kwa jina tu. Hili lilimuwezesha Bahá'u'lláh kuendeleza Hoja katika hali ya usalama kiasi. Mírzá Yaḥyá alikuwa amepata upendo mwingi na msaada kutoka kwa Bahá'u'lláh katika kipindi chote cha maisha yake mwanzoni, lakini alionesha kuwa mwenye kutaka makuu na mwoga. Kuuawa kishahidi kwa Báb kulimshtua mno kiasi kwamba karibu apoteze imani yake. Alitangatanga kwa muda kama darweshi katika milima ya Mázindarán, mwenendo wake ukiwa wa kuaibisha mno kiasi kwamba baadhi ya Wabábí wa eneo hilo walizimika kuiacha Hoja. Akificha utambulisho wake mara kwa mara, hatimaye alikuja Baghdád, na baada ya kujipatia kiasi cha fedha cha kufanya biashara kutoka kwa Bahá'u'lláh, alikuwa akiishi kwa jina jipya katika mojawapo ya ujirani wa mji huo.

Kuongezeka kwa heshima na upendo aliokuwa akioneshwa Bahá'u'lláh na wafuasi wa Báb, hali kadhalika hadhi Yake iliyokuwa ikiongezeka miongoni mwa maafisa wa mji huo, vilikuwa na athari mbaya kwa Mírzá Yaḥyá. Wivu wake uliamshwa na moto wake uliwaka kwa nguvu mno kiasi kwamba uliteketeza kila dalili ya mwenendo mwema. Akiwa na mshirika asiye na haya zaidi kuliko yeye mwenyewe, Mírzá Yaḥyá alianza kupanda mbegu za mashaka miongoni mwa Wabábí kuhusu dhamira za Bahá'u'lláh. Kwa mara nyingine tena mawingu ya tuhuma, hofu na mawazo ya kipuuzi yalishuka juu ya jumuiya ya Kibábí. Kpindi kifupi cha amani na utulivu kilifikia mwisho na, siku hadi siku, mateso ya Bahá'u'lláh yaliendelea kuongezeka.

Asubuhi ya 10 Aprili 1854, familia ya Bahá'u'lláh iliamka na kukuta kwamba Yeye alikuwa ameondoka. Aliuacha mji huo bila kumwambia yeyote kusudi Lake au alikokuwa anakwenda. Alipotambua hatma ya vitendo vya Mírzá Yaḥyá, Bahá'u'lláh aliamua kuondoka na kwenda kwenye milima ya Kurdistan, kaskazini mashariki mwa Ba<u>gh</u>dád. "Kusudi moja tu la kuondoka Kwetu", Yeye Mwenyewe baadaye alisema, "lilikuwa kuepuka kuwa sababu ya mafarakano miongoni mwa waaminifu, chanzo cha vurugu kwa wenzi Wetu, njia ya madhara kwa roho yoyote, au chanzo cha huzuni kwa moyo wowote."[35]

Huko nyikani, mbali kidogo kutoka mji wa Sulaymáníyyih, Bahá'u'lláh aliishi peke Yake akizungumza na Mungu. Yeye aliridhika na chakula kidogo tu. Wakati mwingine alipokea maziwa kutoka kwa wachungaji wa maeneo jirani na, mara chache alikwenda mjini kupata mahitaji machache muhimu ya maisha. Walakini, hata wakati wa kukutana huku kwa muda mfupi na watu wa eneo hilo, ukuu wa Bahá'u'lláh haukuweza kufichka kutoka machoni pao. Upendo na hekima Yake viliwavutia wakazi wa Sulaymáníyyih na umaarufu Wake ulianza kuenea katika maeneo ya karibu. Habari za mtu mwenye hekima na ufasaha usio wa kawaida aliyekuwa akiishi katika eneo hilo la Kurdistán hatimaye zilifika Ba<u>gh</u>dád. Familia Yake, ikitambua kwamba Mtu huyu asingekuwa mwingine zaidi ya Bahá'u'lláh, ilimtuma muumini mwaminifu kwenda kumsihi arudi. Bahá'u'lláh alikubali ombi lao, hivyo akimaliza miaka miwili ya kujitenga Kwake kwa hiari.

1. Wale Wabábí waliokwenda Ba<u>gh</u>dád baada ya Bahá'u'lláh kuwasili katika mji huo walikuwa katika hali gani? ____________________

   ____________________

2. Kwa nini walikuwa wameangukia katika hali kama hiyo? ____________________

   ____________________

   ____________________

3. Nini kilianza kutokea katika jumuiya ya Wabábí chini ya ushawishi wa Bahá'u'lláh?

   ____________________

   ____________________

4. Je, Báb alikuwa amemtaja mtaja mrithi? Kwa nini hakufanya hivyo? ____________________

   ____________________

   ____________________

5. Báb alimtaja nani kama mkubwa kwa jina tu? ______________________________

6. Upi ulikuwa uhusiano wa Mírzá Yaḥyá na Bahá'u'lláh? ______________________

7. Elezea tabia ya Mírzá Yaḥyá: ______________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________

8. Mírzá Yaḥyá alifanya nini baada ya Báb kuuawa? ___________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________

9. Je, heshima na upendo uliokuwa ukiongezeka ambao Bahá'u'lláh alikuwa akioneshwa na wafuasi wa Báb, hali kadhalika hadhi Yake iliyokuwa ikiongezeka miongoni mwa maafisa wa mji, vilikuwa na athari gani juu ya Mírzá Yaḥyá? __________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________

10. Je, Bahá'u'lláh alifanya nini alipoona hatma ya vitendo vya Mírzá Yaḥyá? _______
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________

11. Je, Bahá'u'lláh aliondoka kwenda eneo gani? ______________________________

12. Bahá'u'lláh hutuambia kwamba kusudi moja tu la kuondoka Kwake lilikuwa kuepuka kuwa sababu ya ____________________________________________ , chanzo cha ________________________________ , njia ya ____________________________ , au chanzo cha ____________________________________ .

13. Bahá'u'lláh alifanya nini katika nyika ya Kurdistan? _________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________

14. Kujitenga kwa Bahá'u'lláh kutoka Ba<u>gh</u>dád kulidumu kwa muda gani? __________

15. Ni hali gani zilizomfanya arudi? ____________________

____________________

____________________

## SEHEMU YA 18

Kila Mdhihirishaji wa Mungu hufanya Agano na wafuasi Wake. Wafuasi wa Báb walikuwa wameingia katika Agano Naye kwamba wangemtafuta na kumkubali Yeye Ambaye Mungu angemdhihirisha na kuishi kwa kutii amri Zake. Ingawa Bahá'u'lláh alikuwa bado hajawaambia wengine kwamba Yeye ndiye Yule aliyeahidiwa na Báb, ukuu Wake ulikuwa ukiongezeka zaidi na zaidi kila siku ipitayo, na wachache hata walianza kulitambua Daraja Lake. Mírzá Yaḥyá ambaye hakuwa kipofu kwa ukuu wa enzi na utukufu wa Bahá'u'lláh, alieendelea kuchochea fitina miongoni mwa Wabábí. Miaka iliyofuata, kama ulivyoona, njama zake dhidi ya Bahá'u'lláh ziliongezeka kwa ukubwa zaidi na zaidi, hadi mwishowe yeye alivunja Agano la Báb wazi wazi. Akirejelea kwenye ghasia na taabu zilizokuwa zinawasubiri, Bahá'u'lláh aliwatahadharisha wenzi Wake waaminifu:

> **"Siku za majaribu sasa zimewadia. Bahari za mafarakano na taabu zinasukasuka, na Beramu za Mashaka, katika kila pembe na kila kona, zinajishughulisha kuchochea fitina na kuwaongoza watu kwenye maangamizi kabisa. . . . Msiache sauti ya baadhi ya askari wa ukanaji itie mashaka miongoni mwenu, wala msijiruhusu kuwa wasiomjali Yule Ambaye ni Ukweli, kwa kuwa katika kila Kipindi Kitakatifu ushindani kama huo umekuwa ukianzishwa. Mungu, walakini, atasimamisha Imani Yake, na kudhihirisha mwanga Wake ingawa wachochezi wa maasi huuchukia sana. . . . Ilindeni sana kila siku Hoja ya Mungu. . . . Wote ni mateka mikononi Mwake. Hakuna mahali pa yeyote kukimbilia. Usifikirie Hoja ya Mungu ni kitu chepesi, ambamo mtu yeyote anaweza kuzifurahisha haja zake. Katika maeneo mbalimbali roho kadhaa katika wakati huu, zimeendeleza dai hili hili. Muda unakaribia ambapo. . . kila mmoja wao atakuwa amekwishaangamia na kupotea, la, atakuwa si kitu na atakuwa kitu kisichokumbukwa, kama vile vumbi lenyewe."[36]**

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Bahá'u'lláh Aliwaambia wenzi Wake wasiache ____________ ya baadhi ya ____________ itie ____________ .

   b. Aliwatahadharisha wasijiruhusu kuwa ____________ Yule ____________ ____________ .

   c. Aliwahakikishia wenzi Wake kwamba Mungu atasimamisha ____________ ____________ na kudhihirisha ____________ hata kama maadui wa Hoha huukataa.

   d. Mtu asifikirie kuwa Hoja ya Mungu ni ____________ ambamo anaweza ____________ zake.

e. Muda utafika ambapo wale wote walioenda kinyume na Imani watakuwa __________________ na ______________ . Kama vile vumbi lenyewe watakuwa si kitu cha _____________________ .

2. Bahá'u'lláh anawaita wale wanaotaka kutia mashaka kama "askari wa ukanaji". Je, wanakana nini?

## SEHEMU YA 19

Wakati wa kutokuwepo kwa Bahá'u'lláh kwa kipindi cha miaka miwili, ustawi wa Imani ulikuwa umefikia kiwango cha chini kabisa cha historia yake. Kama ilivyotarajiwa, Mírzá Yaḥyá alikuwa amejithibitisha mwenyewe kuwa hakuwa na uwezo wa kuongoza hata jumuiya ndogo kabisa huko Baghdád. Katika sehemu mbalimbali, Wabábí kadhaa walikuwa wakijihusisha katika shughuli ambazo zilileta aibu kwa Hoja yenye thamani ya Báb. Hivyo, kwa mara nyingine tena, Bahá'u'lláh alichukua jukumu la kuihuisha jumuiya hiyo. Kuwasili Kwake mnamo Machi 1856 kulitangazwa kwa waumini, na mlango Wake ulifunguliwa kwa wale wote waliotamani sana ukweli. Ile nyumba ya kawaida ambamo Yeye aliishi pamoja na familia Yake ikawa kituo cha kukutania watafutaji na wageni. Kila mmoja aliyekuja mbele Yake alibadilishwa na nguvu ya maneno Yake matamu na yenye upendo. Wale waliopata baraka ya kuishi katika ujirani wa karibu na Yeye walihisi kana kwamba walikuwa paradiso. Waligeuka kuwa muumbo mpya, waliojitenga kabisa na mambo ya ulimwengu huu. Hivi ndivyo jinsi Nabíl, mwanahistoria mkuu wa Enzi ya mwanzoni ya Kibahá'í, alivyoezea hali ya roho hizo:

> "SikSiku nyingi wakati wa usiku si chini ya watu kumi walijikimu kwa tende zenye thamani isiyozidi 'penny' moja. Hakuna aliyejua hasa viatu vilikuwa vya nani, makanzu au majoho yaliyokuwemo ndani ya nyumba zao yalikuwa ya nani. Yeyote aliyekwenda dukani aliweza kudai kuwa viatu miguuni mwao vilikuwa vyake, na yeyote aliyekuja mbele ya Bahá'u'lláh aliweza kuthibithisha kuwa kanzu na joho alilokuwa amevaa wakati huo ni lake. Majina yao wenyewe waliyasahau, ndani ya mioyo yao kila kitu kilikuwa kimeondolewa isipokuwa upendo wa kumwabudu Mpendwa wao. . . . Ah, kwa furaha ya siku zile, na nderemo na maajabu ya saa zile!"[37]

Bahá'u'lláh alikaa huko Baghdád kwa miaka saba baada ya kurudi Kwake kutoka Sulaymáníyyih. Wakati wote huo, Yeye aliendelea kuficha Daraja Lake kama Mdhihirishaji wa Mungu kwa Siku hii. Walakini upendo Mtakatifu ulimiminika kutoka Kwake kwa kiasi ambacho mioyo pokevu haikuwa na jinsi ila tu kuguswa nao. Miongozo aliyofunua katika mazungumzo na katika aya na Nyaraka zilizoandikwa ilibadilisha tabia ya Wabábí ambao walikuwa wameachwa bila mchungaji kwa muda mrefu sana. Hii ni miaka ambamo Yeye alifunua Kitabu cha Yakini, ambamo alielezea asili ya Ufunuo wa Mungu kwa maneno yaliyo wazi kabisa kiasi kwamba misingi ya vipengele vya imani vilivyobuniwa na watu wa wakati uliopita vilitupiliwa. Ni katika kipindi hiki hiki kwamba Yeye alifunua, huku akiwa anatembeatembea kwenye kingo za mto Tigris akiwa amezama katika tafakari, Maneno Yaliyofichwa, yanayopendwa na kila mmoja wetu kama mwongozo kwa ajili ya ukuaji wetu wa kiroho. Kasi ambayo kwayo aya Takatifu zilitiririka kutoka kwenye Kalamu Yake ilikuwa ya kushangaza. Hivi ndivyo jinsi Yeye Mwenyewe anavyokizungumzia kipindi kile chenye nguvu isiyo ya kawaida:

**“. . . Tulifunua kama mvua kubwa, kwa msaada wa Mungu na Neema na rehema Yake Takatifu, aya Zetu, na kuzituma katika maeneo mbalimbali ya ulimwengu. Tuliwasihi watu wote, hususan watu hawa, kwa kupitia ushauri Wetu wa hekima na maonyo yenye upendo, na tuliwakataza kujihusisha na uchochezi, mizozo, migogoro na ugomvi. Matokeo ya hili, na kwa neema ya Mungu, ukaidi na upuuzi vilibadilishwa kuwa ucha Mungu na ufahamu, na silaha zilibadilishwa kuwa zana za amani.”[38]**

Ile miaka saba ya maisha ya Bahá’u’lláh huko Baghdád ilionesha kipindi cha ushindi adhimu. Ilikuwa itarajiwe, hivyo, kwamba punde au baadaye hali ya hatari sharti itokee, ambayo baadaye ingefuatiwa na ushindi mkubwa zaidi. Kuongezeka kwa hadhi ya Bahá’u’lláh hakukupita bila kuonwa na maadui wa Imani. Mwenye juhudi kabisa miongoni mwao alikuwa Sheikh mmoja ambaye alitumia kila njia alizokuwa nazo kuwasadikishia maafisa wa Serikali zote mbili za Uajemi na Uturuki, na vile vile makasisi, kuinuka kumpinga Yeye.

Kwa miaka mingi, jitihada za Sheikh huyo zilizuiwa na hekima ya Bahá’u’lláh na ubora wa maneno na vitendo Vyake. Wakati mmoja, Sheikh huyu aliwaita pamoja makasisi mashuhuri kabisa wa eneo hilo akiwa na nia ya kupata kauli ya pamoja ya kumshutumu Bahá’u’lláh. Wote walikuwa tayari kuanzisha mashambulizi dhidi ya kikundi hiki kidogo cha wahamishwa hapo Baghdád ili kuiangamiza Imani kwenye kiini chake. Kwa mshangao, walakini, yule mwenye daraja la juu kabisa miongoni mwao, mtu ambaye alijulikana kwa haki na uchaji wake, alikataa kutoa hukumu iliyohitajika dhidi ya Wabábí. Yeye alikiambia kile kikundi kwamba, kwa ufahamu wake, jumuiya ya Kibábí haikufanya chochote ambacho kingesweza kuhalalisha kitendo kama hicho na akaondoka katika ule mkusanyiko.

Kwa kuwa mpango wao wa awali ulishindwa, kikundi hicho kiliamua kumtuma mtu mwenye elimu kwenda kwa Bahá’u’lláh na kumpelekeaa maswali kadhaa kwa ajili ya kuupima elimu Yake. Baada ya kusikia majibu ya Bahá’u’lláh kwa yale maswali, mjumbe huyu kwa niaba ya kile kikundi cha makasisi, alikubali upana wa elimu Yake. Lakini basi, yeye alisema, ili kumridhisha kila muhusika juu ya ukweli wa Ujumbe Wake, Yeye inabidi awafanyie muujiza. “Ingawa huna haki kuomba jambo hili”, Bahá’u’lláh alijibu, “kwa kuwa Mungu ndiye anayewajaribu viumbe Wake, na wao hawapaswi kumjaribu Mungu, bado ninaruhusu na kukubali ombi hili.”[39] Walakini, Yeye alimpa yule mjumbe sharti moja: kwanza wale makasisi sharti wachague muujiza mmoja na waandike kwamba, baada ya kufanyika kwake, wasiwe tena na shaka juu Yake na wakubali na kukiri ukweli wa Hoja Yake. Waifunge hati hii na kuipeleka Kwake.

Jibu hili la wazi na lenye changamoto lilimuathiri sana yule mjumbe. Aliinuka mara moja, akalibusu goti la Bahá’u’lláh na kuondoka. Aliuwasilisha ule ujumbe wa Bahá’u’lláh kwa kile kikundi cha makasisi. Walilumbana juu ya hili kwa siku tatu, lakini hawakuweza kufikia uamuzi wowote. Hatimaye, hawakuwa na chaguo lingine ila kuachana na jambo hilo.

Bado maadui hawa katili wa Imani hawakuacha njama zao dhidi ya Bahá’u’lláh. Waliendelea kuchochea fitina na kupotosha dhamira Yake kwa mamlaka, hadi hatimaye, katika majira ya machipuko ya mwaka 1863, juhudi zao zilizaa matunda, na hali nyingine ya hatari ikafuata.

1. Je, jumuiya ya Kibábí ilikuwa katika hali gani wakati Bahá’u’lláh aliporejea Baghdád?

______________________________________________

______________________________________________

2. Je, Mírzá Yaḥyá aliweza kujithibitisha mwenyewe kuwa na uwezo wa kuongoza jumuiya? ______________________________________________

3. Kurejea kwa Bahá’u’lláh huko Baghdád kulikuwa na matokeo gani juu ya Wabábí?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

4. Ukichota kutoka maelezo ya Nabíl, sema maneno machache kuhusu hali ya wale walioishi katika ujirani wa karibu na Bahá’u’lláh.

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

5. Je, Bahá’u’lláh alikaa huko Baghdád kwa miaka mingapi baada ya kurejea Kwake kutoka Sulaymáníyyih? ______________________________________________

6. Taja vitabu viwili vilivyofunuliwa na Bahá’u’lláh katika ile miaka saba huko Baghdád:

______________________________________________

______________________________________________

7. Ni ipi dhamira kuu ya Kitabu cha Yakini? ______________________________________________

______________________________________________

8. Mada za aina gani zinazoongelewa katika Maneno Yaliyofichwa? ______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

9. Kamilisha sentensi zifuatazo:

a. Bahá'u'lláh hutuambia kwamba kwa ____________ wa Mungu na ____________ na ____________ Yake, Yeye alifunua aya Zake kama ________________ .

b. Alizituma aya hizi katika ______________________________________________ .

c. Katika aya hizi, Yeye ______________ wanadamu wote kwa kupitia ____________ Wake na ____________________________ .

d. Yeye aliwakataza _________________ na ________________ , ________________ , ______________ , na _________________ .

e. Matokeo ya hili, na kwa neema ya Mungu ______________ na _______________ , vilibadilishwa kuwa __________________ na ________________ na _____________ zilibadilishwa kuwa ______________ za _______________ .

10. Hadhi ya Bahá'u'lláh ilivyo kuwa ikiongezeka iliwaathirije maadui wa Imani? ____

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

11. Kifungu hiki cha maneno "shutuma ya pamoja" kina maana gani? _______________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

12. Kwa maneno yako mwenyewe simulia hadithi ya kile kikundi cha makasisi na yule mjumbe waliyemtuma kwa Bahá'u'lláh huko Baghdád.

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 20

Kadiri unavyoendelea na ujifunzaji wako wa Imani, utasoma Kitabu cha Yakini na utatafakari juu ya maana ya kina ya mada zake nyingi. Hadi sasa tayari unakifahamu kitabu cha Maneno Yaliyofichwa. Kitabu hiki kitakuwa mwenzi wako kwa maisha yako yote, na mwongozo mtakatifu uliomo humo utakuwa na athari kubwa juu ya maendeleo yako ya kiroho. Hadi hapa unapotafakari juu ya kipindi cha maisha ya Bahá'u'lláh huko Baghdád, wakati ambapo vitabu hivi viwili vilifunuliwa, pengine ungependa kukariri kifungu cha ufunguzi cha kila kitabu. Kitabu cha Yakini huanza kwa maneno haya:

> **"Hakuna mtu atakayezifikia fuko za bahari ya ufahamu wa kweli isipokuwa amejitenga na vyote vilivyomo mbinguni na duniani. Takaseni roho zenu, Enyi watu wa ulimwengu, ili huenda mtaweze kulifikia lile daraja ambalo Mungu amelikusudia kwa ajili yenu na hivyo kuingia katika lile hekalu ambalo, kulingana na vipindi vitatatifu vya Mjalia, limeinuliwa katika mbingu ya Bayán."**[40]

Na kifungu cha ufunguzi cha Maneno Yaliyofichwa husomeka:

> **"Hiki ndicho kile kilichoshuka kutoka milki ya utukufu, kutamkwa na ulimi wenye uwezo na nguvu na kufunuliwa kwa Mitume wa kale. Tumechukua kiini chake cha ndani tu na kukivisha vazi la ufupisho kama ishara ya neema kwa wanyofu ili waweze kubakia waaminifu kwa Agano la Mungu, waweze kutimiza katika maisha yao uaminifu Wake, na katika milki ya roho wapate kito cha njema takatifu."**[41]

## SEHEMU YA 21

Kuelekea mwisho wa kukaa Kwake huko Baghdád, Bahá'u'lláh mara kwa mara alianza kuzungumzia juu ya mitihani na majaribu yaliyokuwa mbele yao. Ndoto ambayo wakati mmoja aliwasimulia wenzi Wake ilisababisha majonzi makubwa. "Niliwaona," Aliandika katika Waraka mmoja: "Mitume na Wajumbe wakiwa wamekusanyika na kukaa karibu Yangu, wakipiga kite, wakilia na kuomboleza kwa sauti. Nikistaajabu, Nilliwauliza sababu, ndipo

kuomboleza na kilio chao vikaongezeka zaidi, na wakaniambia: ‘Tunakulilia Wewe, Ewe Fumbo Kuu Kabisa, Ewe Hekalu la Umilele!’ Walilia kwa kile kilio kiasi kwamba Mimi pia nililia pamoja nao. Ndipo Umati wa juu uliponiambia ukisema: ‘. . . Muda si mrefu utaona kwa macho Yako mwenyewe kile ambacho hakuna Mtume amepata kukiona. . . Uwe na subira, uwe na subira.’. . . Waliendelea kunisemesha usiku kucha hadi karibu na mapambazuko.”[42]

Mapema katika majira ya machipuko ya 1863, Bahá’u’lláh alifunua Waraka wa Baharia Mtakatifu ambao, katika lugha ya mafumbo, alibashiri matukio ya siku zijazo na akazungumzia juu ya usaliti na utengano. Waraka huu ulisomwa kwa marafiki waliokusanyika mbele Yake. Bahari za huzuni zilisukasuka mioyoni mwao kwa kuwa walihisi kwamba Yeye ilipaswa achukuliwe kutoka kwao. Baadaye siku hiyo hiyo, tarishi alimpelekea Bahá’u’lláh taarifa ikimuomba akafanye mahojiano na gavana wa Baghdád. Siku iliyofuata, alipofika kwa ajili ya mahojiano hayo, Bahá’u’lláh alipewa barua kutoka kwa waziri mkuu wa himaya ya Ottoman, ikiwa imeandikwa kwa namna ya adabu, ilimtaka Bahá’u’lláh kusafiri hadi mji mkuu wa Uturuki, Constantinople. Kikundi cha walinzi wapanda farasi kiliamriwa kumsindikiza kwa ajili ya ulinzi Wake. Bahá’u’lláh alikubali ombi hilo mara moja, lakini alikataa kupokea fedha ambazo serikali ilitoa kwa ajili ya safari Zake. Mwakilishi wa gavana alisisitiza kwamba azikubali, akisema kwamba mamlaka zingehisi kukosewa kama asingefanya hivyo. Hatimaye, alichukua kiasi kikubwa cha fedha na papo hapo akazigawa miongoni mwa masikini wa mji huo.

Habari za uhamisho wa Bahá’u’lláh kutoka Baghdád ziliitikisa jumuiya ya Wabábí. Zile roho aminifu, ambazo mioyo yao ilikuwa imejifungamanisha sana na Uwepo Wake mwangavu, zilielemewa na huzuni. Mwanzoni, hakuna aliyeweza kulala wala kula. Pole pole, walakini, walitulizwa kwa maneno mema na ya huruma ya Bahá’u’lláh na walikubali kuwa wengi mno watanyimwa baraka ya kuandamana Naye katika hatua iliyofuata ya uhamisho Wake. Kama dalili ya upendo Wake, Yeye aliandika, kwa mkono Wake mwenyewe Waraka kwa kila mmoja wa waumini walioishi katika mji huo—mwanamume, mwanamke na mtoto.

Katika viunga vya Baghdád, kulikuwa na bustani nzuri iliyojaa mawaridi, na waridi lilikuwa ua lipendwalo sana na Bahá’u’lláh. Mchana wa tarehe 22 Aprili, aliondoka mjini na kuingia ndani ya bustani hii. Waumini, na kwa hakika idadi kubwa ya watu wa Baghdád, walipatwa na huzuni. Jumuiya ya Wabábí, sasa ikiwa imehuishwa kabisa kupitia utangalizi wa upendo wa Bahá’u’lláh, ilikuwa imeingia tena katika hali nyingine ya hatari. Ni upi ungekuwa mustakabali wa Imani hii changa ambayo Tumaini lake pekee lilikuwa linahamishwa kwenda mahali ambako ni mbali mno kutoka wengi wa wafuasi wake? Jibu lililokuwa likiwangojea wale marafiki waliovunjika mioyo ambao walikusanyika kumuaga lilikuwa la kushangaza ajabu. Bahá’u’lláh alipasulia mbali tando ambazo zilificha Daraja Lake halisi na akatangaza kwamba Yeye ndiye alikuwa Yule Mwahidiwa wa Zama zote.

Bahá’u’lláh alikaa katika bustani hiyo, ijulikanayo leo kama Bustani ya Riḍván, kwa muda wa siku kumi na mbili kabla ya kuondoka kwenda Constantinople. Maadui Zake walikuwa wamejaribu kuipa pigo kubwa Hoja Yake kwa kumtenganisha Yeye na kundi la wafuasi wake. Mungu, walakini, alikugeuza kuagana huko kuwa tukio la furaha kubwa mno. Tangazo la Utume Wake lilianzisha uhai mpya katika roho za wenzi Wake. Hii ndiyo ilikuwa Siku ya Siku ambayo kwayo Báb alikuwa amewaandaa. Bahá’u’lláh Mwenyewe husema kwamba katika Siku hiyo “vitu vyote vilivyoumbwa vilizamishwa katika bahari ya utakaso.”[43]

Kuna tondoti kidogo zijulikanazo juu ya mazungumzo ambayo Bahá'u'lláh aliyafanya na mmiminiko wa wageni aliowapokea katika Bustani ya Riḍván. Maneno yafuatayo ya mwanahistoria Nabíl yanatupa kianga tu juu ya utukufu wa siku zile:

> "Kila siku, kabla ya saa ya mapambazuko watunza bustani walichuma mawaridi ambayo yalikuwa yamepangiliwa kwa mstari pembezoni mwa njia nne za bustani, na waliyalundika katikati ya sakafu ya hema Lake lililobarikiwa. Lile lundo lilikuwa kubwa mno kiasi kwamba pale wenzi Wake walipokusanyika kunywa chai yao ya asubuhi mbele Yake, wale waliokaa upande mmoja walishindwa kuwaona waliokaa upande wa pili. Mawaridi yote haya, Bahá'u'lláh kwa mikono Yake mwenyewe, aliyakabidhi kwa wale Aliowaaga kutoka mbele Yake kila asubuhi ili wawapelekee, kwa niaba Yake, marafiki Zake wa Kiarabu na wa Kiajemi mjini humo. . . . Usiku mmoja, usiku wa tisa wa mwezi mwandamo, nilitokea kuwa mmoja wa wale waliolinda kando ya hema Lake lililobarikiwa. Saa sita ya usiku ilipokaribia, nilimuona akitoka katika hema Lake, akapita karibu na mahali ambapo baadhi ya wenzi Wake walikuwa wamelala, na akaanza kutembea akipanda na kushuka katika zile njia za bustani zenye kingo za maua zilizokuwa zinaangaziwa na mwezi. Shorwe waliimba kwa sauti kubwa mno kila upande kiasi kwamba ni wale tu waliokuwa karibu Naye ndio waliweza kuisikia kwa uwazi sauti Yake. Aliendelea kutembea tembea hadi aliposita katikati ya mojawapo ya njia hizi, akisema: 'Fikiria shorwe hawa. Ni mkubwa mno upendo wao kwa mawaridi haya kiasi kwamba, bila kulala tangu machweo hadi mapambazuko, wao huimba nyimbo zao na kuzungumza kwa shauku kali na kusudi la ibada yao. Inawezekanaje basi, kwamba wale wanaodai kuwa wanawaka kwa uzuri wa Mpendwa mfano wa mawaridi wangeweza kuchagua kulala?' Kwa siku tatu mfululizo nililinda na kulizunguka hema Lake lililobarikiwa. Kila wakati nilipopita karibu na kitanda alipolala, nilimkuta macho, na kila siku, tangu asubuhi hadi jioni, nilimuona akijishughulisha bila kukoma katika mazungumzo na mmiminiko wa wageni uliokuwa ukiendelea kumiminika kutoka Ba<u>gh</u>dád. Hata mara moja sikuweza kugundua katika maneno aliyoyasema dalili yoyote ya udanganyifu."[44]

Leo, Siku Kuu ya Riḍván inasherehekewa kila mwaka kote ulimwenguni kuadhimisha Tangazo la Utume wa Bahá'u'lláh. Zikidumu kwa siku kumi na mbili, ni siku kuu takatifu kabisa na muhimu kabisa kati ya siku kuu zote za Kibahá'í.

1. Simulia kwa maneno yako mwenyewe, ile ndoto aliyoota Bahá'u'lláh kuelekea mwishoni mwa kukaa Kwake huko Ba<u>gh</u>dád.

   ______________________________________________
   ______________________________________________
   ______________________________________________
   ______________________________________________
   ______________________________________________
   ______________________________________________

2. Ile ndoto ilikuwa na maana gani? ______________________

   ______________________________________________
   ______________________________________________

3. Lini Bahá’u’lláh alifunua ule Waraka wa Baharia Mtakatifu? ____________________

________________________________________________________________________

4. Waraka wa Baharia Mtakatifu ulitabiri nini? __________________________________

________________________________________________________________________

5. Je, yule tarishi kutoka serikalini alimpelekea nini Bahá’u’lláh siku ile Waraka uliposomwa kwa marafiki waliokusanyika mbele Yake? ________________________

________________________________________________________________________

6. Kitu gani kiliwasilishwa kwa Bahá’u’lláh siku iliyofuata? _______________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

7. Je, serikali iliamua kumpeleka wapi Bahá’u’lláh? ______________________________

________________________________________________________________________

8. Je, Bahá’u’lláh alifanya nini na kile kiasi cha fedha ambacho serikali ilikuwa imempa kwa ajili ya safari Zake? __________________________________________________

________________________________________________________________________

9. Je, jumuiya ya wafuasi ilizipokeaje zile habari za kukaribia kuondoka kwa Bahá’u’lláh? _____________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

10. Bahá’u’lláh alifanya nini kama ishara ya upendo Wake kwa waumini huko Ba<u>gh</u>dád?

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

11. Ile bustani ambamo Bahá’u’lláh alitangaza Utume Wake sasa inajulikana kwa jina gani? _________________________________________________________________

12. Alikaa katika bustani hii kwa siku ngapi? ______________________________________

13. Kuhusu zile siku tukufu ambazo Bahá’u’lláh alikaa katika Bustani ya Riḍván, Nabíl hutusimulia:

a. Kila siku, saa ya alfajiri, watunza bustani ______________________________ ____________________________________________________ na __________ ____________________________________________________________ .

b. Lile lundo la mawaridi lilikuwa kubwa mno, kiasi kwamba wenzi wa Bahá'u'lláh ____________________________________________ mbele Yake wasingeweza ____________________________________________________________ .

c. Mawaridi yote haya Bahá'u'lláh, kwa mikono Yake mwenyewe, aliyakabidhi kwa wale aliowaaga kutoka mbele Yake kila siku asubuhi kuwapelekea, kwa niaba Yake, ________________________________________________________ .

d. Usiku mmoja, Nabíl alitokea kuwa mmoja wa wale ambao _________________ ____________________________________________________________ .

e. Saa sita ya usiku ilipokaribia, Nabíl alimuona Bahá'u'lláh akitoka _________________________ , akapita karibu na ________________________ ______________ , na Akaanza _______________________________________ .

f. ___________________________ kwa sauti kubwa mno kiasi kwamba ni wale tu waliokuwa karibu na Bahá'u'lláh ndio waliweza __________________________ .

g. Bahá'u'lláh aliendelea kutembea tembea hadi, __________________________ , Yeye alisema: "Fikiria _____________ hawa. Ni mkubwa mno _______________ wao kwa ______________________ kiasi kwamba, _________________ tangu ______________________________ , wao _____________________ zao na ________________________________________________ . Inawezekanaje basi, ____________ wale ______________ kuwa __________________________ _________________________________________________________ kuchagua ____________ ?"

h. Kwa siku tatu mfululizo Nabíl ____________________________________ ____________________________________________ .

i. Kila wakati Nabíl alipopita karibu na kitanda ambapo Bahá'u'lláh alikuwa amelala, yeye _________________ , na kila siku, tangu asubuhi hadi jioni, yeye _________________________________________________________________ ________________________________________________________ .

j. Hata mara moja Nabíl hakuweza kugundua katika maneno aliyoyasema Bahá'u'lláh _____________________________________________________ .

14. Je, maadui wa Imani walikuwa wakijaribu kutimiza nini kwa kumtenganisha Bahá’u’lláh na kundi la waumini, na Mungu alikusudia nini badala yake? _________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

15. Ni siku kuu gani ambayo tunaiadhimisha leo kama kumbukizi ya Tangazo la Utume wa Bahá’u’lláh? ________________________________________________

16. Je, Siku kuu ya Riḍván hudumu kwa muda gani na lini inasherehekewa? _________

______________________________________________________________________________

17. Sasa kwa kuwa umemaliza mafunzo juu ya uhamisho wa Bahá’u’lláh kutoka Iran hadi ‘Iráq, andaa na toa mazungumzo mafupi juu ya kipindi hiki cha maisha Yake.

## SEHEMU YA 22

Hapo chini kuna vifungu kutoka Waraka uliofunuliwa na Bahá’u’lláh. Visome vifungu hivyo kwa sauti katika kikundi chako na wakati unapofanya hivyo, kumbuka Tangazo la Bahá’u’lláh katika Bustani ya Riḍván na acha Maneno Yake yaujaze furaha moyo wako.

> **“Majira Matakatifu ya machipuko yamefika, Ewe Kalamu Uliyetukuka kabisa, kwa kuwa Siku kuu ya Mwenye Rehema—Kabisa inakaribia haraka. Changamka na litukuze, mbele ya muumbo mzima, jina la Mungu, na tukuza sifa Yake, kwa namna ambayo vitu vyote vilivyoumbwa viweze kuongoka na kuhuishwa. Sema, na usinyamaze. Nyota ya mchana ya furaha kuu inang’aa juu ya upeo wa jina Letu, Mwenye-Furaha kuu, kwa kuwa ufalme wa majina ya Mungu umepambwa kwa pambo la jina la Bwana wako, Muumba wa mbingu. Inuka mbele ya mataifa ya dunia, na jihami kwa silaha ya uwezo wa Jina hili Kuu Kabisa, na usiwe miongoni mwa wale wanaokawia. . . .**

> **“Je, unaweza kumgundua mwingine yeyote ila Mimi, Ewe Kalamu, katika Siku hii? Nini kimetokea kwa muumbo na muonekano wake? Vipi kuhusu majina na ufalme wao? Vimeenda wapi viumbe vyote, viwe vinavyoonekana au visivyoonekana? Vipi kuhusu siri zilizofichwa za ulimwengu na funuo zake? Tazama, muumbo mzima umepita! Hakuna kilichosalia isipokuwa Uso Wangu, Adumuy—Daima, Ang’aaye, Mtukufu—Kabisa.**

> **“Hii ni Siku ambamo hakuna kinachoweza kuonekana isipokuwa wangavu wa Mwanga ambao hung’aa kutoka uso wa Bwana Wako, Mwenye Neema, Mkarimu—Kabisa. Kwa kweli, tumesababisha kila roho kupoteza uhai kutokana na enzi Yetu isiyozuilika na ishindayo vyote. Ndipo tukaumba muumbo mpya,**

**kama dalili ya neema Yetu kwa wanadamu. Mimi, kwa kweli ni Mkarimu— Kabisa, Mkale wa Siku. . . .**

**"Sema: Hii ndiyo ile Paradiso ambayo juu ya majani yake, divai ya matamshi imechapisha ushuhuda: 'Yule aliyekuwa amefichwa kutoka macho ya watu amefunuliwa, akizungukwa na enzi na nguvu!' Hii ndiyo ile Paradiso, ambayo mchakacho wa majani yake hutangaza: 'Enyi ambao huishi mbinguni na duniani! Kimetokea kile ambacho kamwe hakipata kutokea hapo kabla. Yule Ambaye, tangu milele, alikuwa ameuficha Uso Wake kutoka machoni pa muumbo sasa amekuja.' Kutoka upepo mwanana uvumao ambao huvuma katikati ya matawi yake sauti hutokea: 'Yule Ambaye ni Bwana Mwenye—enzi wa vyote amedhihirishwa. Ufalme ni wa Mungu,' ambapo kutoka maji yake yatiririkayo, mvumo unaweza kusikika: 'Macho yote yamefurahishwa, kwa kuwa Yule Ambaye hakuna aliyewahi kumuona, Ambaye siri yake hakuna aliyeigundua, ameuinua utando wa utukufu, na kuufunua wajihi wa Uzuri.'**

**"Ndani ya Paradiso hii, na kutoka vilele vya vyumba vyake ya juu kabisa, Wanawali wa Mbinguni wamepaza sauti na kupiga kelele: 'Shangilieni, enyi wakazi wa milki za juu, kwa kuwa vidole vya Yule Ambaye ni Mkale wa Siku vinagonga, kwa jina la Mtukufu Kabisa, Kengele Kuu Kabisa, ndani kabisa ya kiini cha mbingu. Mikono ya fadhili imezungusha kikombe cha uzima wa milele. Jongea na kunywa tani yako. Kunyweni kwa ladha yenye afya, Enyi ambao ni mifano hasa ya shauku, enyi ambao ni mifano halisi ya matamanio makali!'"[45]**

## SEHEMU YA 23

Bahá'u'lláh, familia Yake na kile kikundi kidogo walioambatana nao walikaa huko Constantinople kwa miezi minne tu. Serikali ya Uajemi iliendeleza kutoka mbali mateso kwa Yule Ambaye ushawishi Wake uliokuwa unaongezeka waliuona dhairi kama tishio. Balozi wake katika baraza la Sulṭáni—mtawala wa Himaya ya Ottoman—alianzisha kampeni yenye mpangilio dhidi ya Bahá'u'lláh. Mazingira ambamo Sulṭáni, mawaziri wake na washirika wao waliishi yalikuwa yale ya usaliti, njama na unafiki. Bahá'u'lláh alikataa kujihusisha kwa chochote na wajumbe wa baraza na shabaha zao zisizofaa. Hili lilirahisisha zaidi kazi ya yule Balozi wa Uajemi kuzijaza akili za wenye mamlaka tuhuma na uwongo. Juhudi zake zisizokoma zilifanikiwa na hatimaye amri ilitolewa kumhamisha Bahá'u'lláh kwenda kwenye mji wa Adrianople, mbali zaidi kutoka mpaka wa Uajemi.

BahBahá'u'lláh alipokea amri hii kwa ujasiri usio wa kawaida. Papo hapo alifunua Waraka mrefu ambamo alimuandikia Sulṭáni mwenyewe, akimkemea yeye na mawaziri wake, na kuonesha uchanga wao na uwezo wao mdogo. Waraka huo uliwasilishwa kwa waziri mkuu Sultan ukiwa ndani ya bahasha iliyofungwa. Inasemekana kwamba alipoifungua ile barua na kuanza kuisoma, alikwajuka na akasema: "Ni kama vile Mfalme wa Wafalme alikuwa akitoa amri yake kwa mfalme wake wa daraja la chini kabisa na akirekebisha mwenendo wake."[46]

Ile safari ya siku kumi na mbili kutoka Constantinople hadi Adrianople ilikuwa ngumu sana kwa Bahá'u'lláh na familia Yake, ambao sasa walikuwa katika uhamisho wao wa tatu. Ilikuwa ni mwezi wa Desemba na hali ya hewa ilikuwa ya baridi mno. Hata kupata maji kutoka

chemchemi njiani mwao iliwalazimu kuwasha moto ili kuyeyusha barafu. Wengi wa wahamishwa hawa hawakuwa na nguo zinazofaa kujikinga na hali mbaya ya hewa kama hiyo.

Bahá'u'lláh aliingia Adrianople mnamo 12 Desemba 1863 na alikaa katika mji huo kwa jumla ya miaka minne na nusu. Kipindi hiki tena kilikuwa kimojawapo cha hali ya hatari ya kuumiza na ushindi wa fahari sana. Kadiri ushawishi wa Bahá'u'lláh ulivyoongezeka, ndivyo moto wa wivu ulivyowaka kwa ukali zaidi katika moyo wa Mírzá Yaḥyá. Akawa jasiri zaidi na zaidi katika upinzani wake na alijaribu kila awezavyo kuwazuia Wabábí wasimkubali Mdhihirishaji wa Mungu kwa Siku hii. Matatizo aliyoyasabisha si tu yalileta shida ndani ya jumuiya yenyewe, bali pia yaliwapa silaha maadui wa nje wa Imani ambazo walizitumia kuanzisha mashambulizi zaidi dhidi ya Bahá'u'lláh na wafuasi Wake. Usaliti wa Mírzá Yaḥyá ulionekana kutokuwa na mipaka. Yeye hata aliamua kumtilia sumu Bahá'u'lláh, na baada ya njama na jitihada kubwa hatimaye alifanikisha kusudi lake. Athari ya ile sumu kwa Bahá'u'lláh ilikuwa kubwa, na ingawa alipona, alibakia na mkono unaotetemeka hadi mwisho wa maisha Yake.

Adrianople, bila shaka, haitakumbukwa kwa vitendo vya aibu vya Mírzá Yaḥyá, bali kwa ushindi mkuu ambao Bahá'u'lláh aliupata katika mji ule. Ilikuwa ni kutokea hapo kwamba Bahá'u'lláh alituma Nyaraka Zake nyingi alizowaandikia wafalme na watawala wa ulimwengu na aliitangaza Imani Yake kwa marefu na mapana.

Tangazo Lake la kwa umma lilikuwa ni hatua ya tatu ya mchakato uliokuwa ukiendelea hatua kwa hatua ambao kupitia humo Utume Wake ulifanywa ujulikane kwa wanadamu. Hatua ya kwanza ilianza katika gereza la Síyáh-Chál huko Ṭihrán wakati Roho Takatifu ilipojifunua yenyewe kwa Bahá'u'lláh na kumtangaziia kwamba Yeye alikuwa Mchukuzi wa Ujumbe wa Mungu kwa siku hii. Ingawa kuzaliwa kwa Ufunuo Wake kulibakia bila kujulikana kwa miaka kumi, kama mapambazuko, kulichochea roho zilizokuwa zimelala, kukiamsha zile pokevu na kuziandaa kumtambua Bahá'u'lláh. Hatua ya pili iliwekwa wazi katika Bustani ya Riḍván, ambako Yeye alitangaza Utume Wake kwa baadhi ya marafiki waliokuwa wamekusanyika kumuaga. Sasa idadi ndogo ya roho zilizopendelewa zililitambua Daraja Lake. Hatua ya tatu ilikuwa tangazo la Utume Wake kwa watu wote. Ilianzia Constantinople, na ikachapuzwa huko Adrianople, na kufikia vilele vyake vya juu kabisa huko 'Akká, mahali palipofuata na pa mwisho pa uhamisho Wake.

1. Bahá'u'lláh alikaa huko Constantinople kwa muda gani? ______________________

2. Kwa nini kukaa Kwake huko kulikuwa kwa muda mfupi hivyo? ________________

   ______________________________________________________________________

   ______________________________________________________________________

3. Kwa nini Bahá'u'lláh hakujihusisha na masuala ya baraza la Sulṭán alipokuwa anaishi katika mji mkuu? ______________________________________________________

   ______________________________________________________________________

4. Balozi wa Uajemi alitumiaje fursa hii ya kukataa kwa Bahá'u'lláh kujihusisha na masuala ya wajumbe wa baraza na shabaha zao zisizofaa? _____________________

5. Je, Yeye alihamishiwa wapi baadaye? ____________________

6. Kwa nini Serikali ya Uajemi ilitaka apelekwe mbali zaidi kutoka mipaka yake? ____

7. Bahá'u'lláh alifanya nini alipopokea habari za uhamisho Wake kutoka Constantinople?

8. Waziri mkuu wa Sultani alisema nini alipoisoma ile barua ya Bahá'u'lláh? ____

9. Bahá'u'lláh aliwasili lini huko Adrianople? ____________________

10. Ni kwa muda gani alikaa katika mji huo? ____________________

11. Ni tukio gani muhimu kabisa lililotukia huko Adrianople? ____________________

12. Tangazo la Utume wa Bahá'u'lláh kwa wanadamu lilipitia hatua ngapi? ____

13. Ipi ilikuwa hatua ya kwanza? ____________________

14. Ipi ilikuwa hatua ya pili? ____________________

15. Ipi ilikuwa hatua ya tatu? ____________________

## SEHEMU YA 24

Upinzani wa wazi wa Mírzá Yaḥyá dhidi ya Bahá'u'lláh huko Adrianople ulisababisha msukosuko mkubwa miongoni mwa kikundi kidogo cha wahamishwa, ambao wengi wao ndio kwanza walikuwa wanaanza kupata kianga cha Daraja la Bahá'u'lláh. Hii iliwapa maadui wa Hoja, ambao nyuma yao kulikuwa na nguvu ya serikali mbili—ya Uajemi na ya Ottoman—fursa waliyoihitaji kuipa pigo lingine Imani changa ya Mungu. Ghafla asubuhi moja nyumba ya Bahá'u'lláh ilizingirwa na askari, na kila mmoja aliambiwa ajiandae kuondoka mara moja. Kwa muda, hakuna aliyejua hatma yao ingekuwaje. Hofu kubwa katika mioyo ya wengi ilikuwa kutenganishwa na Mpendwa wao, kwa sababu kulikuwa na tetesi kwamba Bahá'u'lláh na familia Yake wangehamishwa kwenda sehemu moja na wengine wangelazimishwa kutawanyika. Mwishowe, ikawa wazi kwamba Bahá'u'lláh angehamishiwa kwenye mji-gereza wa 'Akká, na Mírzá Yaḥyá kwenye kisiwa cha Cyprus. Wengi wa wahamishwa hawa, takriban watu sabini, walipelekwa 'Akká, wakiwemo pia wafuasi wawili waovu kabisa wa Mírzá Yaḥyá. Kwa upande mwingine, wanne miongoni mwa wenzi wa Bahá'u'lláh, walihamishwa pamoja na kundi la Mírzá Yaḥyá kwenda Cyprus.

Bahá'u'lláh na familia Yake waliondoka Adrianople mnamo 12 Agosti 1868, na baada ya safari ya taabu kwa nchi kavu na baharini, waliwasili huko 'Akká mnamo tarehe 31 Agosti. Wakazi wa 'Akká walizoea kuwasili kwa wafungwa, kwa kuwa mji huo ulitumiwa na watawala wa Ottoman kama mahali pa uhamisho kwa wahalifu na wachochezi. Wakati huu, waliambiwa kwamba hao wapya wanaowasili walikuwa maadui wa Serikali, wa Mungu na dini Yake. Sulṭáni aliamuru wawekwe katika kifungo kikali, akiamini kwamba ukali wa hali ngumu za 'Akká hatimaye ungewaangamiza. Amri ya Sulṭáni ilisomwa hadharani msikitini, na ilieleweka kwa wote kwamba hawa Waajemi wamehukumiwa kifungo cha kudumu na kwamba ushirikiano nao ulikatazwa kabisa.

Baada ya kushuka kutoka chomboni huko 'Akká, wahamishwa walipelekwa kwenye kambi ya jeshi, mojawapo ya sehemu yake ndio ingekuwa gereza lao. Usiku wa kwanza, walinyimwa chakula na kinywaji, na tangu hapo na kuendelea kila mmoja aligawiwa mikate mitatu isiyo na ubora kila siku. Punde, kila mmoja akaugua, isipokuwa wawili, na baada ya muda mfupi, watatu miongoni mwao walifariki. Walinzi walikataa kuwazika wale marehemu bila kulipwa gharama zilizohitajika. Zulia dogo la sala lililotumiwa na Bahá'u'lláh liliuzwa, na kiasi cha fedha kilichopatikana walipewa wale walinzi. Baadaye, ilijulikana kwamba hawakutimiza ahadi yao na waliwazika wale marehemu bila kuwaosha, bila sanda na bila majeneza. Kwa kweli walikuwa wemepewa maradufu ya kiasi kilichohitajika kwa ajili ya yale mazishi.

Ingawa hali za kifungo pole pole ziliboreshwa, miaka ya mwanzoni huko 'Akká ilikuwa kipindi cha mateso makali kwa Bahá'u'lláh. Yale aliyokuwa ameyastahimili huko Síyáh-Chál alikuwa amesababishiwa na maadui wa nje wa Imani tu. Ile ghasia ya kule Adrianople kwa asili yake ilikuwa ya ndani. Hali ya hatari ya ile miaka ya mwanzoni huko 'Akká, walakini, ililetwa na nguvu za maadui wa Imani wa nje na wa ndani pia. Yeye Mwenyewe amekielezea kipindi hiki kwa maneno kama yafuatayo:

> **"Ujue kwamba baada ya kuwasili Kwetu Mahali hapa, tuliamua kupaita 'Gereza Kuu Kabisa'. Ingawa hapo awali katika nchi nyingine (Tihran) tuliwekwa katika minyororo na pingu, bado tulikataa kupaita kwa jina hilo. Sema: Fikirini juu ya jambo hilo, Enyi mliojaliwa ufahamu!"[47]**

Licha ya amri ya Sulṭán kwamba asiwepo yeyote wa kushirikiana na Bahá'u'lláh na familia Yake, idadi ya waumini huko Uajemi walifanya safari ndefu ya kwenda 'Akká,

aghalabu kwa miguu, wakitumaini kwamba wangeweza kuruhusiwa kufika mbele Yake. Zilipowasili, roho hizi zilizojitoa, zikishindwa kumkaribia Yeye, zilisimama mbali zikilitazama gereza Lake, ziliridhika kuona japo kidogo tu mwili Wake kupitia nondo za dirisha Lake. Mpungo wa mkono Wake uliobarikiwa ilikuwa zawadi tosha kwa safari ya miezi kadhaa, na wengi wao hapo walirejea nyumbani, wakishukuru kwa baraka waliyoipata.

Tukio la kuhuzunisha mno katika kipindi hiki ni kifo cha ghafla cha Mírzá Mihdí mwanae Bahá'u'lláh, aliyejulikana kama Tawi Safi Kabisa. Jioni moja alikuwa juu ya paa la kambi, akitembea tembea akiwa amezama katika sala na tafakari, ndipo alipoanguka kupitia dirisha dogo la kupitisha mwanga lililokuwa juu ya paa hilo, hadi kwenye kasha la mbao lililokuwa sakafuni. Mbavu zake zilichomwa, na ingawa daktari aliitwa, hapakuwa na la kufanya. Ndani ya saa ishirini na mbili alikuwa amekwishafariki. Kabla hajafariki, Bahá'u'lláh alimuuliza Tawi Safi Kabisa kile alichotamani. Yeye alijibu: "Natamani watu wa Bahá waweze kufika mbele Yako." "Na hivyo ndivyo itakavyokuwa," Bahá'u'lláh alisema. "Mungu atajalia matakwa yako."[48]

Japokuwa mateso ya Bahá'u'lláh yalikuwa makali mno katika Gereza Kuu Kabisa, lazima ikumbukwe kwamba uhamisho Wake kwenda 'Akká ulikuwa utimilizo wa unabii wa zamani. Ilikuwa ni huko 'Akká ambako Jua la Ukweli lingewaka kwa miaka ishirini na minne katika utukufu wake wote. Ilikuwa ni katika kipindi hiki wakati akiutembelea Mlima Carmel ulioko karibu na Haifa, ndipo Bahá'u'lláh alimuonesha 'Abdu'l-Bahá mahali ambapo Kaburi Takatifu la Báb baadaye lingejengwa. Huko Bahjí, Mahali Pake pa kupumzika, kwenye viunga vya 'Akká ndipo pangekuwa Mahali Patakatifu Kabisa duniani, ambako waumini kote ulimwenguni wangepageukia wakati wa kusali kila siku. Ni ndani ya mipaka ya Kaburi Takatifu la Báb ndipo makao makuu ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu yangesimikwa. Ile miji pacha ya Haifa na 'Akká ingekuwa makao makuu ya kiroho na kiutawala ya ulimwengu ya Imani ya Kibahá'í. Hivyo, ni kwa maneno haya, katika Waraka uliofunuliwa katika miaka ya mwanzoni ya kukaa Adrianople, Bahá'u'lláh alidokezea juu ya uhamisho Wake kwenda 'Akká:

> **"Baada ya kuwasili Kwetu Tulikaribishwa kwa beramu za mwangaza, ambapo Sauti ya Roho iliita ikisema: 'Punde vyote viishivyo duniani vitaandikishwa chini ya beramu hizi.'"[49]**

1. Jinsi gani maadui wa nje wa Imani huko Adrianople walitumia matatizo yaliyosababishwa na Mírzá Yaḥyá kwa manufaa yao? ________________________

   ______________________________________________________________________

2. Uhamisho uliofuata wa Bahá'u'lláh ulikuwa wapi? __________________________

3. Je, Mírzá Yaḥyá alipelekwa wapi? ________________________________________

4. Je, wangapi waliambatana na Bahá'u'lláh kwenda 'Akká? ____________________

5. Je, unafikiri kwa nini baadhi ya wafuasi wa Bahá'u'lláh walipelekwa Cyprus pamoja na Mírzá Yaḥyá na wawili kati ya wasaidizi wa Yahyá walipelekwa 'Akká? ______

   ______________________________________________________________________

   ______________________________________________________________________

6. Tarehe ngapi Bahá'u'lláh aliondoka Adrianople? ______________________________

7. Tarehe ngapi aliwasili huko 'Akká? ________________________________________

8. Ni amri gani Sulṭáni alitoa kuhusu kifungo cha Bahá'u'lláh na wale waliokuwa wakiambatana Naye? ________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________

9. Watu wa 'Akká walijuaje kuhusu amri hizo? _________________________________
________________________________________________________________________

10. Bahá'u'lláh na wenzi Wake walipelekwa wapi walipowasili huko 'Akká? ________
________________________________________________________________________

11. Elezea kwa maneno machache hali za siku zao za mwanzoni humo gerezani: _______
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________

12. Ni kwa jina gani Bahá'u'lláh aliita 'Akká? ____________________________________

13. Ni tukio gani la kuhuzunisha kabisa lililotokea wakati wa miaka ya mwanzoni huko 'Akká? ________________________________________________________________

14. Ni katika mazingira gani mahujaji wa mwanzoni walivyokuwa wakifika 'Akká? ___
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________

15. Kwa maneno yako mwenyewe elezea mazingira ya kifo cha Tawi Safi Kabisa.

________________________________________________________________________
________________________________________________________________________
________________________________________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

________________________________________

16. Kwa miaka mingapi Bahá’u’lláh alikaa huko ‘Akká na katika viunga vyake? ______

17. Bahá’u’lláh alimuonesha nini ‘Abdu’l-Bahá walipokuwa wanatembea juu ya Mlima Carmel huko Haifa? ____________________________

18. Mahali Patakatifu Kabisa duniani ni nini na pako wapi? ____________________

________________________________________

19. Je, makao makuu ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu yako wapi api? ___________

________________________________________

20. Je, makao makuu ya kiroho na kiutawala ya ulimwengu ya Imani ya Kibahá’í yapo wapi? __________________________________

________________________________________

21. Je, unajua mahujaji hufanya nini hivi leo wanapotembelea Haifa na ‘Akká? Pengine ungependa kumuuliza rafiki mmoja katika jumuiya yenu ambaye amewahi kwenda Nchi Takatifu kuhiji akusimulie juu ya hilo.

## SEHEMU YA 25

Huko ‘Akká Bahá’u’lláh aliendeleza tangazo Lake kwa watu wote. Hapa kuna baadhi ya vifungu ambavyo Yeye aliwaandikia wafalme na watawala wa ulimwengu kutokea Adrianople na ‘Akká:

Kwa Mfalme wa Ufaransa, Napoleon III:

**“Ewe Mfalme wa Paris! Mwambie kasisi asipige tena kengele. Kwa Mungu, Yule wa Kweli! Kengele Yenye Nguvu Kabisa imetokea katika umbo la Yule Ambaye ni Jina Kuu Kabisa . . .”**[50]

Kwa Nicolaevitch Alexander II Czar wa Urusi:

**“Inuka wewe miongoni mwa watu kwa jina la Hoja hii ishurutishayo vyote, na yaite, basi, mataifa kwa Mungu, Aliyetukuka, Aliye mkuu.”**[51]

Kwa Malkia Victoria wa Uingereza:

**"Weka kando tamaa yako, na elekeza basi moyo wako kwa Bwana wako, Mkale wa Siku. Tunakutaja wewe kwa ajili ya Mungu, na kutamani kwamba jina lako liweze kutukuzwa kupitia kumbukumbu yako kwa Mungu, Muumba wa dunia na mbingu."**[52]

Kwa William I, Mfalme wa Prussia:

**"Jihadhari kiburi kisije kikakuzuia kutambua Chimbuko la Ufunuo Mtakatifu, tamaa za kidunia zisije zikakufungia nje kama vile utando, kutoka kwa Bwana wa Kiti cha enzi juu na chini duniani."**[53]

Kwa Francis-Joseph, Mfalme wa Austria:

**"Fumbua macho yako, ili uweze kuutazama Maono haya matukufu, na kumtambua Yule Ambaye unamuita wakati wa mchana na katika majira ya usiku, na kazia macho kwenye Mwanga ambao huwaka juu ya Upeo huu ung'aao."**[54]

Kwa Sulṭáni 'Abdu'l-'Azíz wa Himaya ya Ottoman:

**"UsiwUsiweke kando hofu ya Mungu, na uwe miongoni mwa wale ambao hutenda kwa uadilifu. Wakusanye kando yako wale mawaziri ambao kutoka kwao unaweza kuona manukato ya imani na haki, na shauriana nao, na uchague chochote kile kilicho bora kabisa machoni pako, na uwe miongoni mwa wale ambao hutenda kwa ukarimu."**[55]

Kwa Náṣiri'd-Dín Sháh wa Uajemi:

**"Tunaomba kwamba, kutokana na ukarimu Wake—atukuzwe Yeye—Yeye aweze kuuahilia huru, kupitia kifungo hiki, shingo za watu kutoka kwenye minyororo na pingu, na kuwafanya wageukie kwa nyuso aminifu, kuelekea Wajihi Wake, Yule Ambaye ni Mwenye nguvu, Mkarimu. Yeye yu tayari kumjibu yeyote amuitaye, na Yeye yu karibu na wale wazungumzao Naye."**[56]

Kwa watawala wa Amerika na Marais wa Jamhuri zake:

**"Waunganisheni kwa mikono ya haki waliokatishwa tamaa, na mpondeni dhalimu ambaye hustawi kwa fimbo ya amri za Bwana Wenu, Muamuru, Mwenye Hekima—Kabisa."**[57]

Kwa Papa Pius IX:

**"Neno ambalo Mwana alilificha limedhihirishwa. Limetelemshwa katika umbo la hekalu la kibinadamu katika siku hii. Abarikiwe Bwana Ambaye ni Baba! Yeye, kwa kweli, amekuja kwa mataifa katika enzi Yake kuu kabisa."**[58]

Kwa shirika zima la watawa wa Kanisa la Kikristo:

**“Enyi kundi la watawa! Msijitenge wenyewe makanisani na kwenye makazi ya watawa. Tokeni mara moja kwa idhini Yangu, na jishughulisheni na kile kitakachozinufaisha roho zenu na roho za watu.”**[59]

## SEHEMU YA 26

Miezi minne baada ya kifo cha ghafla cha Tawi Safi Kabisa, Bahá’u’lláh na wenzi Wake ililazimika waondolewe kutoka kambini ili kupisha vikosi vya jeshi. Yeye na familia Yake walihamishiwa katika nyumba kadhaa kwa vipindi vifupi vifupi na hatimaye walihamia katika nyumba ijulikanayo leo kama Nyumba ya ‘Abbúd. Waliendelea kuwa chini ya ulinzi na walizungukwa na watu ambao, wakishawishika na amri za Sulṭán, hawakuwa rafiki na waliwaonesha uhasama kwao.

Kadiri muda ulivyopita, walakini, watu wa ‘Akká walikuja kutambua utovu wa hatia wa kikundi hiki kidogo cha wahamishwa kutoka Uajemi, na masharti ya kifungo chao yalilegezwa. Sehemu kubwa ya mabadiliko ilisababishwa na ‘Abdu’l-Bahá, Ambaye alikuwa akikutana sana na wakazi wa mji huo na aliweza kuwaonesha nia ya kweli ya Wabahá’i na asili ya mafundisho ya Baba Yake. Hatimaye, Bahá’u’lláh alikuwa akitoka mjini ‘Akká na kutembelea maeneo ya karibu karibu. Baada ya kuzuiwa kwa muda mrefu sana ndani ya kuta za mji wa ukiwa, Bahá’u’lláh sasa alikuwa akitumia muda huko mashambani na kufurahia uzuri na uoto wa asili ambao Aliupenda mno.

Miaka ya mwisho ya maisha ya Bahá’u’lláh ilitumiwa ndani ya Kasri la Bahjí, nje kidogo tu ya ‘Akká. Likiwa limejengwa wakati Yeye alipokuwa amefungwa ndani ya kuta za mji huo, lilitelekezwa na mwenyewe wakati wa mlipuko wa ugonjwa katika eneo hilo. ‘Abdu’l-Bahá aliweza kulipata kwa ajili ya Baba Yake mpendwa, kwanza kwa kulikodi na baadaye kulinunua moja kwa moja.

Hadi wakati huu mtazamo wa watu, siyo tu wa ‘Akká, bali pia maeneo ya jirani ya Syria na Lebanon, juu ya Bahá’u’lláh na wafuasi Wake ulikuwa umebadilika kabisa. Ingawa amri ya Sulṭán ilikuwa bado haijaondolewa, na kwa utaratibu bado alikuwa mfungwa kwa kifungo chenye masharti makali, kwa uhalisi, Yeye alikuwa akistahiwa na kuheshimiwa kama mfalme. Hata maafisa wa eneo hilo walikuwa wakimwendea kupata ushauri na mawaidha Yake. Hivyo ndivyo ilivyo nguvu ya Ufunuo wa Bahá’u’lláh ya kubadilisha mioyo ya watu.

Katika miaka hiyo huko ‘Akká na Bahjí, Bahá’u’lláh alifunua vitabu vingi zaidi na zaidi vya mwongozo ambao ungeiwezesha jamii ya wanadamu kuujenga ustaarabu mtukufu wa ulimwengu. Chenye nguvu kabisa kati ya vitabu vilivyotiririka kutoka kwenye Kalamu Yake kilikuwa Kitáb-i-Aqdas, Kitabu Kitakatifu Kabisa cha Kipindi Chake Kitakatifu, kilichofunuliwa katika Nyumba ya ‘Abbúd mnamo 1873 hivi. Shoghi Effendi, akirejelea kwenye Maandiko ya Bahá’u’lláh katika Nchi Takatifu, anaeleza:

**“Maandiko ya Bahá’u’lláh katika kipindi hiki, kama tukichunguza uwanda mpana ambao yanaukumbatia, huonekana kuwa yanaangukia katika makundi matatu tofauti. La kwanza hujumuisha yale maandiko ambayo hufanya mfuatano wa tangazo la Utume Wake huko Adrianople. La pili hujumuisha sheria na amri za Kipindi Chake Kitakatifu, ambazo, kwa sehemu kubwa, zimeandikwa katika Kitáb-i-Aqdas, Kitabu Chake Kitakatifu Kabisa. Kwa lile la tatu sharti**

**lijumuishe zile Nyaraka ambazo kwa sehemu hutangaza wazi na kwa sehemu huhakikisha tena yale mafundisho na kanuni za kimsingi ambazo huunda msingi wa Kipindi hicho Kitakatifu."[60]**

Upanuzi mkubwa wa Imani ya Bahá'u'lláh katika ulimwengu wa Magharibi haukuanza wakati wa uhai Wake mwenyewe, upanuzi huu ilibidi ungojee kipindi cha Utumishi wa 'Abdu'l-Bahá. Mafundisho Yake, walakini, yalikuwa yametambulishwa katika nchi za Magharibi, na watu wachache huko walikuwa wakifahamu juu ya Mfungwa wa 'Akká Ambaye alikuwa na mvuto wa ajabu kwa wale aliokutana nao. Katika majira ya machipuko ya mwaka 1890, kuelekea mwishoni mwa maisha ya Bahá'u'lláh, Edward Granville Browne, mwanazuoni maarufu kutoka Cambridge, Uingereza, alikuja kukutana Naye. Vifungu vifuatavyo hutoka kwenye kumbukumbu yake ya mahojiano hayo ya kihistoria:

". . . mwongozaji wangu alisimama kidogo wakati nilipokuwa navua viatu vyangu. Kisha, kwa mkono wake haraka aliivuta pazia, nilipopita akairudishia; nami nikajikuta ndani ya chumba kikubwa, upande wa juu kulikuwa na kiti kisicho na egemeo, ambapo mkabala na mlango kulikuwa na viti viwili au vitatu. Ingawa kwa mbali nilikuwa nahisi ni wapi nilikokuwa naelekea na ni nani ningemuona (maana sikuwa nimeelezwa wazi wazi), ilipita sekunde moja au mbili hivi kabla ya kutambua, kwa mshtuko wa mshangao na hofu, kwa hakika kwamba chumba hicho hakikuwa kitupu. Kwenye kona ambako kile kiti kilikuwa kimegusa ukuta, aliketi mtu wa ajabu na mwenye kuheshimika, akiwa amevaa kofia ya kitambaa cha aina iitwayo táji na madarweshi (lakini yenye urefu na muundo usio wa kawaida), na sehemu ya chini yake ilikuwa imezungushiwa kilemba kidogo cheupe. Uso wa yule niliyemtazama kamwe siwezi kuusahau, ingawa siwezi kuuelezea. Macho yake yapenyezayo yalionekana kusoma hadi ndani ndani kabisa ya nafsi ya mtu; nguvu na mamlaka vilikaa kwenye lile paji lake pana; huku mikunjo mikubwa kwenye paji la uso na uso wake vikionesha umri ambao nywele na ndevu nyeusi ti zenye ufahari wa kipekee zilizoshuka hadi karibu na kiunoni zikionekana kukanusha. Hakukuwa na haja ya kuuliza nilikuwa mbele ya nani, nilipoinama mbele ya yule ambaye ndiye kusudi la ibada na upendo ambavyo wafalme wangevionea husuda na watawala wangevitamani bila kuvipata ng'o!

"Sauti ya upole na yenye heshima iliniambia niketi, na kisha ikaendelea: — **'Sifa iwe kwa Mungu kwamba umefanikiwa kufika! . . . Umekuja kumuona mfungwa na mhamishwa. . . . Tunatamani tu mambo mema ya ulimwengu na furaha ya mataifa; walakini wao wanadhania sisi ni wachochezi wa ugomvi na maasi tustahilio kifungo na uhamisho . . . Kwamba mataifa yote yawe taifa moja katika imani na watu wote kama ndugu; kwamba mafundo ya huba na umoja miongoni mwa watoto wa watu yaimarishwe; kwamba tofauti za kidini zikome, na tofauti za kimbari zifutwe—kuna madhara gani katika hili? . . . Walakini hivyo ndivyo itakavyokuwa; ugomvi huu usio na manufaa; vita hivi viharibifu vitakwisha, na 'Amani Kuu Kabisa' itakuja. . . . Je, ninyi huko Ulaya hamhitaji hili pia? Siyo hiki ambacho Kristo alikitabiri? . . . Walakini tunawaona wafalme na watawala wenu wakifuja hazina zao kwa wingi na kwa uhuru zaidi kwenye mambo yanayoangamiza jamii ya wanadamu kuliko yale ambayo yangesaidia kuleta furaha ya jamii ya wanadamu. . . . ugomvi huu na umwagaji huu wa damu na mafarakano sharti vikome, na watu wote wawe kama ukoo mmoja na familia moja. . . . Acha mtu asijitukuze katika hili, kwamba huipenda nchi yake; bali mwache ajitukuze katika hili, kwamba huipenda aina yake. . . .'"[61]**

1. Ni katika mazingira gani Bahá'u'lláh na wenzi Wake waliondolewa kwenye zile kambi? ______________________________

2. Ni lipi jina la ile nyumba huko 'Akká ambamo Bahá'u'lláh na familia Yake hatimaye walihamia? ______________________________

3. Hali za maisha yao huko 'Akká zilibadilikaje? ______________________________

______________________________

4. Kitu gani kilisababisha mabadiliko haya? ______________________________

______________________________

______________________________

5. Ni lipi jina la lile kasri ambamo Bahá'u'lláh aliishi miaka ya mwishoni mwa maisha Yake? ______________________________

______________________________

6. Ni katika mazingira gani 'Abdu'l-Bahá alilipata kasri la Bahjí? ______________________________

______________________________

7. Ni kitabu gani muhimu kabisa kilichofunuliwa na Bahá'u'lláh katika miaka aliyokuwa huko 'Akká? ______________________________

______________________________

8. Kitabu hiki kilifunuliwa wapi na lini? ______________________________

______________________________

9. Ni yapi makundi matatu ambamo, kama ilivyoelezwa na Shoghi Effendi, maandiko ya Bahá'u'lláh ya kipindi hiki hujikita?

   a. ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

   b. ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

   c. ______________________________

   ______________________________

   ______________________________

10. Ni zipi baadhi ya sheria za Kipindi Kitakatifu cha Bahá'u'lláh? ________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

11. Ni yapi baadhi ya mafundisho na kanuni za Kipindi Chake Kitakatifu? __________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

12. Edward Granville Browne alikuwa nani? ________________________________

______________________________________________________________________

13. Ni maneno gani Edward Granville Browne aliyatumia kuelezea, alipokuwa akiinama mbele ya Bahá'u'lláh, jinsi hali ilivyokuwa mbele Yake? ____________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

14. Kulingana na maneno yaliyoandikwa na Edward Granville Browne:

– Bahá'u'lláh alisema matanio Yake ni yapi? ____________________________

______________________________________________________________________

– Alisema mataifa yote yaweje? ________________________________________

______________________________________________________________________

– Alitamani kitu gani kiimarishwe? ____________________________________

______________________________________________________________________

– Alitoa mwito kitu gani kikomeshwe? __________________________________

– Alitoa mwito kitu gani kifutwe? ______________________________________

– Yeye anatabiri kuwa kitu gani kitakuja kutokea? ________________________

______________________________________________________________________

– Ni katika kitu gani Bahá'u'lláh husema kila mmoja wetu anapaswa kujitukuza?

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 27

Kitáb-i-Aqdas siyo kitabu kikubwa; kina aya 190 tu. Ndani mwake, walakini, kuna sheria na kanuni za msingi kwa ajili ya ustaarabu wa ulimwengu wa siku zijazo. Shoghi Effendi hukiita kama Kitabu Mama cha Kipindi Kitakatifu cha Bahá'u'lláh na Katiba ya Utaratibu Wake Mpya wa Ulimwengu. Utasoma vifungu kutoka Kitáb-i-Aqdas mara kwa mara katika maisha yako yote kadiri unavyojitahidi kufungamanisha fikra na vitendo vyako na amri za Mungu. Kwa sasa, inapendekezwa kwamba ukariri vifungu vitano vya mwanzoni.


> **"Wajibu wa kwanza ulioamriwa na Mungu kwa watumishi Wake ni utambuzi wa Yule Ambaye ndiye Chimbuko la Ufunuo Wake na Chemchemi ya Sheria Zake, Ambaye huwakilisha Uungu katika vyote viwili; Ufalme wa Hoja Yake na ulimwengu wa muumbo. Yeyote atimizaye wajibu huu amefikia mema yote; na yeyote aliyenyimwa hilo amekengeuka, japokuwa awe mwanzilishi wa kila tendo jema. Inampasa kila mmoja afikiaye daraja hili adhimu kabisa, kilele hiki cha utukufu wa juu kabisa, kuzingatia kila agizo la Yule ambaye ndiye Haja ya ulimwengu. Wajibu huu pacha hautenganishiki. Mmoja haukubaliki bila ule mwingine. Hivyo ndivyo ambavyo imeagizwa na Yule Ambaye ndiye Chanzo cha uvuvio Mtakatifu.**
>
> **"Wale ambao Mungu amewajalia umaizi watatambua bila kusita kwamba maagizo yaliyoandikwa na Mungu hufanya njia bora kabisa kwa ajili ya kudumisha utaratibu ulimwenguni na usalama wa watu wake. Yule ambaye huyapa kisogo huhesabiwa miongoni mwa walio duni na wapumbavu. Sisi, kwa kweli, tumewaamuru ninyi kukataa misukumo ya shauku potofu na tamaa zenu ovu, na kutovuka mipaka ambayo Kalamu ya Aliye Juu Kabisa imeiweka, kwa kuwa hizi ndizo pumzi ya uzima kwa vitu vyote vilivyoumbwa. Bahari za hekima Takatifu na tamko Takatifu zimeinuka kwa uwezo wa pumzi ya upepo mwanana wa Mwenye Rehema-Zote. Harakieni kunywa funda lenu, Enyi watu wenye ufahamu! Wale ambao wamekiuka Agano la Mungu kwa kuvunja amri Zake, na wamepotoka ghafla, hawa wamekosea vya kusikitisha mno mbele za Mungu, Mwenye-Vyote, Aliye Juu Kabisa.**
>
> **"Ee enyi watu wa ulimwengu! Mjue kwa hakika kwamba amri Zangu ni taa za majaliwa Yangu ya upendo miongoni mwa watumishi Wangu, na funguo za rehema Yangu kwa viumbe Vyangu. Hivyo ndivyo ambavyo zimeshushwa kutoka mbingu ya Mapenzi ya Bwana wenu, Bwana wa Ufunuo. Laiti mtu yeyote angeonja utamu wa maneno ambayo midomo ya Mwenye Rehema-Zote imedhamiria kuyanena, angeweza, hata kama hazina za dunia zingekuwa katika umiliki wake, kuzikana moja na zote, ili aweze kuthibitisha ukweli wa japo mojawapo tu ya amri Zake, uking'aa juu ya Chimbuko la uangalizi wenye baraka tele na wema Wake wa upendo.**
>
> **"Sema: Kutoka kwenye sheria Zangu harufu nzuri ya vazi Langu iweze kunuswa, na kwa msaada wake, bendera za Ushindi zitasimikwa kwenye vilele vya juu kabisa. Ulimi wa uwezo Wangu, kutoka mbingu ya utukufu Wangu wenye nguvu zote, umeuambia muumbo Wangu maneno haya: "Tiini amri Zangu kwa ajili ya upendo wa uzuri Wangu." Ni mwenye furaha yule mpenzi ambaye amevuta manukato matakatifu ya Mpendwa wake Kabisa kutoka maneno haya, yaliyosheheni marashi ya neema ambayo hakuna ulimi uwezao kuielezea. Kwa**

**uhai Wangu! Yule ambaye amekunywa divai bora ya haki kutoka mikono ya fadhili Yangu yenye baraka tele atazungukia amri Zangu zinazong'aa juu ya Chimbuko la muumbo Wangu.**

**"Msidhani kwamba Tumewafunulieni tu orodha ya sheria. La, bali, Tumefungua Divai bora kwa vidole vyenye uwezo na nguvu. Kwa hili hushuhudia kile ambacho Kalamu ya Ufunuo imekifunua. Taamulini juu ya hili, Enyi watu wenye umaizi!"[62]**

## SEHEMU YA 28

Uhamisho wa mfululizo wa Bahá'u'lláh, ingawa ulifanywa kwa amri za wadhalimu wawili kwa kushirikiana na maofisa fisadi wa kidini, kiuhalisi uliongozwa na Mkono wa Mwenyezi Mungu Mwenyewe. Nguvu zilizoachiliwa na Mdhihirishaji wa Mungu kadiri alivyohamishwa kutoka mahali hadi mahali—kutoka nchi Yake ya asili hadi kwenye fuko za 'Akká ambapo katika viunga vyake yangesimikwa makao makuu ya kiroho na ya kiutawala ya Imani Yake, haziwezi kupimika. Ramani iliyopo hapo chini inayoonesha njia za uhamisho Wake, inafahamika kwenu kutokana na usomaji wenu wa Kitabu cha 2. Kufuatana na umaizi ulioupata katika kitengo hiki, tumia muda kidogo kutafakari juu ya maana za kiroho za yale yaliyotukia katika kila mojawapo ya sehemu muhimu kabisa. Na wakati unapotafakari matukio lukuki yanayohusiana na maisha Yake na kupata kianga zaidi juu ya ukuu na utukufu Wake, uwezo na enzi Yake kuu, kumbuka maneno Yake: "Yeye Ambaye milele amefichwa kutoka macho ya watu kamwe hawezi kujulikana isipokuwa kupitia Mdhihirishaji Wake, na Mdhihirishaji Wake hawezi kutoa uthibitisho mkubwa zaidi wa ukweli wa Utume Wake zaidi ya uthibitisho wa Nafsi Yake Mwenyewe."



## SEHEMU YA 29

Katika kipindi cha miaka ambamo Mdhihirishaji wa Mungu anatembea miongoni mwetu nguvu Zake zisizo za kawaida hutawanya ulimwenguni pote, zikisababisha mabadiliko makubwa katika uhalisi wa vitu vyote vilivyoumbwa. Katika Siku hii Tukufu, Bahá'u'lláh alifunua Neno la Mungu kwa jamii ya wanadamu kwa takriban miaka arobaini, akiujalia ulimwengu wa uwepo nguvu zisizo na kikomo, ambazo kukunjuka kwake kuibua ustaarabu wa uzuri usiofikirika. Miongo hii minne ya Ufunuo mtakatifu uendeleao ilifikia mwisho mnamo 29 Mei 1892.

Miezi tisa kabla ya kupaa kwake, Bahá'u'lláh alionesha matamanio Yake ya kuondoka kutoka ulimwengu huu. Tangu wakati huo na kuendelea, ilizidi kuwa wazi kutokana na aina ya mazungumzo aliyofanya kuwa mwisho wa maisha Yake katika uso huu wa dunia ulikuwa unakaribia. Usiku wa 8 Mei, alipata homa kidogo. Homa iliongezeka siku iliyofuata, lakini halafu ilionekana kutoweka. Aliendelea kuwaruhusu baadhi ya waumini na mahujaji kukutana Naye. Hata hivyo punde ilidhihirika kwamba hakuwa katika hali nzuri. Homa Yake ilirudi, mara hii kali zaidi kuliko mwanzoni, na hali Yake iliendelea kuwa mbaya. Tarehe 29 Mei 1892 saa ya alfajiri, mwaka wa 75 wa maisha Yake, roho Yake ilipaa kutoka ulimwengu huu.

Siku sita kabla hajafariki, aliwaita mbele Yake wote waliokusanyika katika Kasri la Bahjí, kwa ule ambao ungekuwa mkutano wao wa mwisho pamoja Naye. Akiwa amepumzika kitandani, akisaidiwa na mmoja wa watoto Wake wa kiume, Yeye aliwaambia: "Nimefurahishwa sana nanyi nyote," alisema. "Mmetoa huduma nyingi, mmekuwa makini sana katika kazi zenu. Mmekuja hapa kila asubuhi na kila jioni. Mungu awasaidie mbakie wamoja. Aweze kuwasaidia kuitukuza Hoja ya Bwana wa viumbe."[63] Machozi yalimiminika kutoka machoni mwa wale waliokusanyika kando Yake.

Habari za kufariki Kwake mara moja zilipelekwa kwa Sulṭán kwa njia ya simu ya maandishi. Ujumbe huo ulianza kwa maneno haya "Jua la Bahá limetua" na uliendelea kumuarifu Sulṭán juu ya mipango ya kuzika mabaki matakatifu karibu na lile Kasri. Chumba kidogo ndani ya nyumba iliyokuwa karibu sana na upande wa magharibi mwa lile Kasri kilichaguliwa, na muda mfupi baada ya jua kutua siku hiyo hiyo ya kupaa Kwake, Mabaki Yake yalipumzishwa. Nabíl huelezea uchungu wa siku zile kwa maneno haya: "Mimi nafikiri, ghasia ya kiroho iliyoanziwa katika ulimwengu wa vumbi imesababisha malimwengu yote ya Mungu kutetemeka. . . . Ulimi wangu wa ndani na wa nje hauna uwezo wa kuelezea hali ambayo tulikuwemo. . . . Katikati ya mkanganyiko ulioenea umati wa wakazi wa 'Akká na wa vijiji vya jirani, waliosongamana mashambani kuzunguka lile Kasri, walionekana wakiomboleza, wakipiga piga vichwa vyao, na wakilia kwa huzuni."[64]

Kwa juma zima, kulikuwa na mmiminiko usiokoma wa waombolezaji, waliokuja kuonesha huzuni yao kwa familia ya Bahá'u'lláh. Watu mashuhuri kutoka kila matabaka yote ya kijamii, wakiwemo Waislamu, Wakristo na Wayahudi, washairi, makasisi na maofisa wa serikali, waliunganika katika kuonesha masikitiko juu ya kifo Chake na katika kusifia wema na ukuu Wake. Wengi wao hata walitoa heshima yao ya mwisho Kwake kwa maandishi. Heshima kama hizo hizo zilizopokelewa kutoka miji ya ukanda wote, ambapo zote ziliwasilishwa kwa 'Abdu'l-Bahá, ambaye sasa aliiwakilisha Hoja ya Bahá'u'lláh. Walakini, hisia hizi za huzuni, kwa maneno ya Mlinzi zilikuwa, "tone tu zikilinganishwa na bahari ya huzuni na ushuhuda mwingi wa moyo wa ibada usio na kikomo ambao, wakati wa kutua kwa Jua la Ukweli, ulimwagika kutoka mioyo ya maelfu yasiyohesabika ambao walijiunga na Hoja Yake, na

walidhamiria kuinua juu beramu yake huko Uajemi, India, Urusi, 'Iráq, Uturuki, Palestina, Misri na Syria."

Sasa, baada ya kutafakari kwa muda mfupi juu ya aya zilizopo hapo juu, unda kikundi cha watu wawili wawili katika kikundi chenu na pamoja na mwenzake simulieni kwa zamu tukio la kupaa kwa Bahá'u'lláh kwa maneno yenu mwenyewe.

## SEHEMU YA 30

Baada ya kufariki kwa Bahá'u'lláh, Nabíl alichaguliwa na 'Abdu'l-Bahá kuchagua vile vifungu vinavyounda maandiko ya Waraka wa Kuzuru. Waraka huu hutongolewa katika Makaburi Matakatifu ya Bahá'u'lláh na Báb. Pia hutumiwa mara kwa mara katika kuadhimisha kumbukizi Zao. Kupaa kwa Bahá'u'lláh huadhimishwa katika saa za mapema alfajiri tarehe 29 Mei. Kadiri unavyoshiriki katika mikusanyiko kama hii katika jumuiya yako, utayafamu maandiko ya Waraka huu wenye uzuri wa hali ya juu kabisa, kama bado hujafanya hivyo. Kwa hiyo, tunapomaliza kozi hii juu ya maisha ya Bahá'u'lláh, inafaa usome na kutafakari juu ya Waraka huo:

**"Sifa ambayo imepambazuka kutoka Nafsi Yako tukufu, na utukufu ambao umeng'aa kutoka uzuri Wako mwangavu kabisa, viwe juu Yako, Ee ewe ambaye u udhihirisho wa Ukuu, na Mfalme wa Milele, na Bwana wa wote walio mbinguni na duniani! Nashuhudia kwamba kwa kupitia Wewe enzi ya Mungu na milki Yake, na utukufu wa Mungu na ukuu Wake, vilifunuliwa, na Nyota za mchana za wangavu wa kale zimetawanya mng'ao wake katika mbingu ya amri Yako isiyobatilika, na Uzuri wa Yule Asiyeonekana umeangaza juu ya upeo wa muumbo. Nashuhudia zaidi kwamba kwa mjongeo tu wa Kalamu Yako amri Yako 'Uwe' imetekelezwa na Siri iliyofichika ya Mungu imefunuliwa, na viumbe vyote vimetokea na Funuo zote zimetelemshwa.**

**"Nashuhudia, zaidi, kwamba kupitia uzuri Wako uzuri wa Yule Mwabudiwa umefunuliwa na kupitia uso Wako uso wa Yule Atamaniwaye umeng'aa, na kwamba kupitia neno kutoka Kwako Wewe umeamua kati ya viumbe vyote, na kuwafanya wale waliojitoa Kwako kupanda kwenye kilele cha utukufu, na makafiri kuanguka katika lindi kubwa la chini kabisa.**

**"Nashuhudia kwamba yeye Ambaye amekujua Wewe amemjua Mungu, na yeye ambaye amefika mbele yako amefika mbele ya Mungu. Ni nyingi, kwa hiyo, baraka ya yule ambaye amekuamini Wewe, na ishara Zako, na amenyenyekea mwenyewe mbele ya enzi Yako, na ameheshimika kwa kukutana Nawe, na amepata ridhaa njema ya Mapenzi Yako, na kukuzungukia Wewe, na amesimama mbele ya kiti Chako cha enzi. Ole wake yule aliyekukosea Wewe, na amekukana Wewe, na kukataa ishara Zako, na kukaidi enzi Yako, na ameinuka dhidi Yako, na kuonesha kiburi mbele ya uso Wako, na kupinga ushuhuda Wako, na kukimbia kutoka utawala Wako, na milki Yako, na kuhesabiwa pamoja na makafiri ambao majina yao yameandikwa kwa vidole vya amri Yako katika Nyaraka Zako takatifu.**

**"Nipeperushie, basi, Ee Mungu wangu na Mpendwa wangu, kutoka mkono wa kuume wa rehema Yako na Wema Wako wa upendo, pumzi takatifu za fadhili**

**Zako, ili ziniondoe mbali kutoka nafsi yangu mwenyewe na kutoka ulimwengu hadi kwenye vitala vya ukaribu Wako na mbele Yako. Una nguvu Wewe kufanya kile kikupendezacho. Wewe, kwa kweli, u juu kabisa ya vitu vyote.**

**"Kumbukumbu ya Mungu na sifa Yake, na utukufu wa Mungu na fahari Yake, viwe juu Yako, Ewe uliye Uzuri wake! Nashuhudia kwamba jicho la muumbo kamwe halijapata kuona aliyedhulumiwa kama Wewe. Wewe ulizamishwa siku zote za maisha Yako chini ya bahari ya mateso. Kwa wakati mmoja Wewe ulikuwa katika minyororo na pingu; kwa wakati mwingine ulitishwa kwa upanga wa maadui Zako. Walakini, licha ya yote haya, Wewe uliwaamuru watu wote kutii yale yaliyoamriwa Kwako na Yeye Ambaye Yu Mjua—Yote Mwenye Hekima—Kabisa.**

**"Roho yangu iwe dhabihu kwa maovu uliyoyapata, na roho yangu iwe fidia kwa taabu ulizostahimili. Namsihi Mungu kwa Wewe na kwa wale ambao nyuso zao zimeangaziwa kwa ming'ao ya mwanga wa wajihi Wako, na ambao, kwa ajili ya upendo Wako, wametii yote yale waliyoamriwa, kuondoa tando ambazo huja kati Yako na viumbe Wako, na kunijalia mema ya ulimwengu huu na ulimwengu ujao. Wewe, kwa ukweli, u Mweza, Aliye-tukuka—Kabisa, Mwenye Utukufu—Wote , Msamehevu—Daima, Mwenye Huruma—Kabisa.**

**"Uubariki, Ee Bwana Mungu wangu, Mti Mtakatifu wa Lote na majani yake, na matawi yake, na vijitawi vyake na mashina yake, na vichipukizi vyake, kadiri majina Yako bora kabisa yatakavyodumu na Sifa Zako tukufu kabisa zitakavyodumu. Uulinde, basi, dhidi ya madhara ya mshari na majeshi ya wadhalimu. Wewe, kwa ukweli u Mweza, Mwenye Nguvu—Kabisa. Wabariki pia, Ee Bwana Mungu wangu, watumishi wako na vijakazi wako ambao wamekufikia Wewe. Wewe, kwa kweli, u Mkarimu—Kabisa, Ambaye neema Yako haina kikomo. Hakuna Mungu aliyepo ila Wewe, Msamehevu—Daima, Mkarimu—Kabisa."[65]**

## SEHEMU YA 31


Kutokana na tajiriba yako, unajua kwamba utapata nafasi nyingi katika miaka ijayo kusimulia historia ya maisha ya Bahá'u'lláh. Bila shaka umeshiriki historia hiyo mara nyiungi tangu ulipomaliza Kitabu cha 2, ambacho kilikupa maelezo mafupi lakini yaliyokamilika ya maisha Yake, kama mojawapo ya mada za kujiimarisha za kuzichunguza pamoja na marafiki na majirani wakati wa mfuatano wa ziara kwenye kaya zao. Kisa ambacho umekisoma hivi punde, kina tondoti nyingi zaidi kuliko ilivyo katika Kitabu cha 2, na utaweza kuleta ujuzi mpya ulioupata katika majadiliano yenu kuhusu utu wa Bahá'u'lláh, kuhusu matukio ya maisha Yake, kadiri hali inavyoruhusu. Muhimu zaidi hata hivyo, utakuwa ule umaizi ambao umeupata kutokana na matukio hayo, kuhusu asili ya Ufunuo Wake, sifa bainifu za Ujumbe Wake, ukubwa wa nguvu zilizoachiliwa na ujio Wake, na umuhimu wa kipindi hiki katika historia ya mwanadamu. Hali zozote ziwazo—iwe mazungumzo mafupi na mtu ambaye ni mpya kwenye Imani, au uwasilishaji unaofanywa wakati wa ziara za nyumbani katika kijiji au ujirani wako—ni umaizi huu huu ambao hatimaye, katika uchambuzi wa mwisho utaathiri jinsi unavyozungumzia kuhusu Utu wa Bahá'u'lláh na kile unachokiwasilisha kwa msikilizaji. Bila shaka, zitakuwepo nyakati ambapo uwasilishaji wa kawaida tu utahitajika, na kurasa zifuatazo zitaweza kukusaidia katika suala hili.

# Bahá’u’lláh

*Utukufu wa Mungu*




**Bahá'u'lláh alizaliwa 12 Novemba 1817 huko Ṭihrán, mji mkuu wa Iran.**
**Tangu utoto Wake alionesha ishara za ukuu. Alipata mafunzo kidogo nyumbani,**
**lakini hakuhitaji kwenda shule, kwa kuwa alikuwa amejaliwa na Mungu elimu ya kiasili.**



**Usiku mmoja, baba Yake aliota ndoto ambapo alimuona Bahá’u’lláh akiogelea baharini. Nuru ambayo ilitoka katika mwili Wake iliyaangazia yale maji. Nywele Zake ndefu nyeusi zilielea pande zote na kundi kubwa la samaki lilimfuata, kila mmoja aking’ang’ania kwenye ncha ya unywele. Aliogelea kwa uhuru na bila kuzuiwa. Ndoto hii ilikuwa mojawapo ya ishara nyingi za hatma kuu ambayo ilikuwa ikimsubiri Bahá’u’lláh.**



**Baadaye alipokuwa kijana, Bahá'u'lláh alipewa nafasi ya juu katika baraza la mfalme lakini aliikataa. Yeye alitaka kutumia muda Wake katika kuwasaidia wanyonge, wagonjwa na masikini, na kuiendeleza hoja ya haki.**



**Alipokuwa na umri wa miaka 27, Bahá'u'lláh alipokea gombo la Maandiko kutoka kwa Báb, Mjumbe mpya wa Mungu, Ambaye alikuwa akiwaandaa watu kwa ajili ya kuja kwa Mwahidiwa wa Zama Zote. Bahá'u'lláh aliukubali Ujumbe wa Báb na akawa mmoja wa wasaidizi Wake mwenye shauku kabisa.**



**Mamlaka, kwa kutotaka kukubali Ukweli uliotangazwa na Báb, zilianza kuwatesa wale waliomuamini Yeye, na hapo ndipo mateso ya Bahá'u'lláh yalipoanza. Mwaka 1852, alikamatwa na kufungwa minyororo kwenye mojawapo ya magereza ya kuogopesha kabisa ya Ṭihrán.**



**Katika gereza hili, Mungu alimfunulia Bahá'u'lláh kuwa alikuwa Yule aliyeahidiwa na Báb na Mitume wote waliotangulia. Kutoka katika gereza hili la shimoni lenye giza Jua la Ukweli lilichomoza, likiuangazia ulimwengu na kuanzisha Siku mpya katika maisha ya wanadamu.**



**Baada ya miezi minne ya kifungo, serikali ilimuhamisha Bahá'u'lláh kutoka nchi aliyozaliwa. Katika majira ya baridi kali, Bahá'u'lláh na familia Yake walianza safari ndefu kutoka Ṭihrán hadi Ba<u>gh</u>dád.**



**Huko Baghdád, umaarufu wa hekima ya Bahá'u'lláh ulienea pande zote.
Watu wa kila usuli walisongamana nyumbani Kwake, wakitafuta msaada na ushauri Wake.
Serikali, ambayo ilikuwa ikiogopa ushawishi wa Bahá'u'lláh, iliamua
kumuhamishia mbali zaidi kutoka nchi Yake ya kuzaliwa.**



# *Bustani ya Riḍván*
## *Aprili 1863*

**Kabla ya kuondoka Ba<u>gh</u>dád, Bahá’u’lláh alitumia siku kumi na mbili katika bustani nje ya mji, ambapo msururu wa wageni walikuja kumuaga. Katika bustani hii, Bahá’u’lláh Alitangaza kwamba Yeye alikuwa Mdhihirishaji wa Mungu kwa Siku hii. Kwa karne zijazo, kipindi hiki cha siku kumi na mbili za mwezi Aprili zitasherehekewa kama Sikukuu za Riḍván, kumbukumbu ya Tangazo la Bahá’u’lláh la Ujumbre Wake unaokumbatia ulimwengu mzima.**



Sulṭáni ‘Abdu’l-‘Azíz
wa Himaya ya Ottoman



Nicolaevitch Alexander II
Czar wa Urusi



Francis-Joseph,
Mfalme wa Austria



Mfalme wa Wafaransa,
Napoleon III




Náṣiri’d-Dín <u>Sh</u>áh
wa Uajemi



Papa Pius IX




Malkia Victoria
wa Uingereza



William I, Mfalme
wa Prussia

**Mahali palipofuata pa uhamisho wa Bahá’u’lláh palikuwa Constantinople na baadaye, Adrianople, miji yote hii miwili ipo katika Uturuki ya leo. Kutokea Adrianople, Bahá’u’lláh, mfungwa na mhamishwa, Aliandika barua kwa wafalme na watawala wa dunia akiwaamuru kuwa wenye haki na kutumia uwezo wao kukomesha mateso na vita.**



**Huko Adrianople, kama hapo kabla umaarufu wa Bahá’u’lláh ulienea kwa wakazi wa ukanda huo na serikali iliamua kumhamishia tena mbali zaidi kwenye mji-gereza wa ‘Akká. Hili lilikuwa gereza ambapo wahalifu wabaya kabisa na wachochea maasi wa nchi walikuwa wakipelekwa ili kamwe wasisikike tena.**



**Hali za kifungo zilikuwa mbaya kupindukia. Baadhi ya wafuasi wa Bahá'u'lláh walisafiri umbali mrefu kwenda 'Akká lakini hawakuruhusiwa kufika mbele Yake. Waliweza kumuona kidogo tu wakiwa mbali wakati akiwapungia mkono kupitia dirisha la chumba Chake cha gereza.**



**Pole pole mashariti ya kifungo yalilegezwa kadri idadi iliyoongezeka ya watu katika eneo hilo walivyotambua uwezo na ukuu wa enzi wa Bahá'u'lláh. Katika kipindi cha miaka ya mwisho ya maisha Yake, Yeye aliishi katika Kasri la Bahjí nje ya kuta za mji. Akiwa huko 'Akká, Bahá'u'lláh alifunua vitabu vya mwoagozo kwa jamii ya wanadamu kikiwepo Kitáb-i-Aqdas, Kitabu Chake Kitakatifu Kabisa.**



**Mnamo Mei, 1892 Bahá'u'lláh alifariki. Mahali Pake pa Mapumziko huko Bahjí, sasa pakizungukwa na bustani nzuri ndipo Mahali Patakatifu Kabisa duniani. Kila mwaka maelfu ya watu kutoka kote ulimwenguni hutembelea mahali Pake pa mapumziko kutoa heshima zao na kusali na kutaamuli katika mazingira yenye utulivu.**

# MAREJELEO


1. Kutoka mazungumzo yaliyotolewa 18 Aprili 1912, yaliyochapishwa katika *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu: Mazungumzo yaliyotolewa na ‘Abdu’l-Bahá wakati wa Ziara Zake huko Marekani na Canada mnamo 1912* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2012), aya. 2, uk. 34 (toleo la Kiingereza).

2. *Miito ya Bwana wa Majeshi: Nyaraka za Bahá’u’lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 2006), na. 3.14–15, uk. 248 (toleo la Kiingereza).

3. Kama hapo juu, na. 3.16–17, ku. 248–49.

4. *Wanamapambazuko: Masimulizi ya Nabíl ya Siku za Mwanzoni za Ufunuo wa Kibahá’í* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, chapisho la 1932, 2018), uk. 119.

5. Kama hapo juu, ku. 119–20.

6. Bahá’u’lláh, *Waraka kwa Mwana wa Mbwa Mwitu* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, 1988, 2016), uk. 11 (toleo la Kiingereza).

7. *‘Abdu’l- Bahá juu ya Falsafa Takatifu* (Boston: Shirika la Uchapishaji la Tudor, 1918), uk. 53 (toleo la Kiingereza).

8. *Wanamapambazuko*, uk. 96 (toleo la Kiingereza).

9. Kama hapo juu, uk. 104.

10. Kama hapo juu, ku. 104–5.

11. Kama hapo juu, ku. 105–6.

12. Kama hapo juu, uk. 106.

13. Kama hapo juu, uk. 107.

14. Kama hapo juu.

15. Kama hapo juu, ku. 107–8.

16. *Mateuzi kutoka Maandiko ya Báb* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, chapisho la 2006, 2014), na. 3:8.1, ku. 106–7 (toleo la Kiingereza).

17. Kama hapo juu, na. 3:27.1, ku. 126–27.

18. Kama hapo juu, na. 5:21.3, uk. 193.

19. *Wanamapambazuko*, uk. 113 (toleo la Kiingereza).

20. Kama hapo juu, uk. 116.

21. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, chapisho la 1983, 2017), CXXIX, aya. 1–2, ku. 316–17 (toleo la Kiingereza).

22. Kutoka mazungumzo yaliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá, 22 Mei 1912, yaliyochapishwa katika *Uenezaji wa Amani ya Ulimwengu*, aya. 6, ku. 193–94 (toleo la Kiingereza).

23. *Wanamapambazuko*, ku. 607–8 (toleo la Kiingereza).

24. *Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, chapisho la 1988, 2005), na. 4.22, uk. 40 (toleo la Kiingereza).

25. Kama hapo juu, na. 7.40, uk. 96.

26. *Waraka kwa Mwana wa Mbwa Mwitu*, ku. 20–21 (toleo la Kiingereza).

27. *Wanamapambazuko*, uk. 632 (toleo la Kiingereza).

28. *Waraka kwa Mwana wa Mbwa Mwitu*, uk. 21 (toleo la Kiingereza).

29. Kama hapo juu, uk. 22.

30. *Miito ya Bwana wa Majeshi*, na. 1.6, ku. 6–7 (toleo la Kiingereza).

31. *Buga Maandiko ya Bahá'u'lláh*, XXIX, aya. 5, uk. 80 (toleo la Kiingereza).

32. Kutoka barua ya 24 Juni 1936 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi, katika "Hali ya hatari na Ushindi: Makusanyo ya Dondoo kutoka Maandiko ya Kibahá'í", yaliyokusanywa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, yaliyochapishwa katika *Makusanyo ya Makusanyo* (Maryborough: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, Australia, 1991), toleo la. 1, na. 287, uk. 148 (toleo la Kiingereza).

33. H. M. Balyuzi*, Bahá'u'lláh: Mfalme wa Utukufu* (Oxford: George Ronald, chapisho la 1991, 2018), uk. 106 (toleo la Kiingereza).

34. Bahá'u'lláh, ilinukuliwa na Shoghi Effendi, *Mungu Yu Nasi* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, chapisho la 1974, 2019), ku. 169–70 (toleo la Kiingereza).

35. Bahá'u'lláh, *Kitáb-i-Íqán: Kitabu cha Yakini* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, chapisho la 2003, 2018), aya. 278, uk. 231 (toleo la Kiingereza).

36. Bahá'u'lláh, ilinukuliwa katika *Mungu Yu Nasi*, ku. 178–79.

37. Nabíl-i-A'zam, ilinukuliwa katika *Mungu Yu Nasi*, ku. 215–16.

38. *Waraka kwa Mwana wa Mbwa Mwitu*, uk. 22 (toleo la Kiingereza).

39. Bahá'u'lláh, ilinukuliwa katika *Mungu Yu Nasi*, uk. 226 (toleo la Kiingereza).

40. *Kitáb-i-Íqán*, aya. 1, uk. 3 (toleo la Kiingereza).

41. Bahá'u'lláh, *Maneno Yaliyofichwa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, chapisho la 2003, 2012), uk. 3 (toleo la Kiingereza).

42. Bahá'u'lláh, ilinukuliwa katika *Mungu Yu Nasi*, uk. 147 (toleo la Kiingereza).

43. Bahá'u'lláh, katika *Kitáb-i-Aqdas: Kitabu Kitakatifu Kabisa* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá'í, chapisho la 1993, 2013), aya. 75, uk. 48 (toleo la Kiingereza).

44. Nabíl-i-A'zam, ilinukuliwa katika *Mungu Yu Nasi*, ku. 240–41(toleo la Kiingereza).

45. *Buga kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, XIV, aya. 1, 4–5, 11–12, ku. 29–34.

46. *Mungu Yu Nasi*, uk. 252 (toleo la Kiingereza).

47. Bahá'u'lláh, ilinukuliwa katika *Mungu Yu Nasi*, ku. 292–93 (toleo la Kiingereza).

48. H. M. Balyuzi, *Bahá'u'lláh: Mfalme wa Utukufu*, ku. 317–19 (toleo la Kiingereza).

49. Bahá'u'lláh, ilinukuliwa katika *Mungu Yu Nasi*, uk. 292 (toleo la Kiingereza).

50. Tangazo la *Bahá'u'lláh kwa Wafalme na Viongozi wa Ulimwengu* (Haifa: Makao Makuu ya Kibahá'í ya Ulimwengu, chapisho la 1967, 1972), uk. 17 (toleo la Kiingereza).

51. Kama hapo juu, uk. 28.

52. Kama hapo juu, uk. 33.

53. Kama hapo juu, uk. 39.

54. Kama hapo juu, uk. 43.

55. Kama hapo juu, uk. 47.

56. Kama hapo juu, uk. 60.

57. Kama hapo juu, uk. 63.

58. Kama hapo juu, uk. 84.

59. Kama hapo juu, uk. 95.

60. *Mungu Yu Nasi*, uk. 325 (toleo la Kiingereza).

61. Edward Granville Browne, akirekodi maneno ya Bahá'u'lláh, ilinukuliwa na H. M. Balyuzi, *Bahá'u'lláh: Mfalme wa Utukufu*, ku. 378–80 (toleo la Kiingereza).

62. Bahá'u'lláh, katika *Kitáb-i-Aqdas*, aya. 1–5, ku. 21–23.

63. Bahá'u'lláh, ilinukuliwa katika *Mungu Yu Nasi*, ku. 350–51 (toleo la Kiingereza).

64. Nabíl-i-A‘zam, ilinukuliwa katika *Mungu Yu Nasi*, ku. 351–52.

65. Bahá’u’lláh, katika *Sala za Kibahá’í: Mateuzi ya Sala Zilizofunuliwa na Bahá’u’lláh, Báb, na ‘Abdu’l-Bahá* (Wilmette: Shirika la Uchapishaji la Kibahá’í, chapisho la 2002, 2017), ku. 323–27.